Jumanne Aprili 7, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580199
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Wawili wafa maji wakivusha watu Mto Msimbazi D'Salaam

UKURASA 4


Nipashe
TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Dk. John Snow: Daktari aliyeleta mapinduzi
Corona ipo, si wakati wa kuzembea wala kupuuza
Wagonjwa 253 694 wapona corona duniani
Mko wapi wanawake waongoza ndege Tanzania?

UKURASA 13

REPOTI CAG

# Vichwa ngumu sasa kitanzini

**NI** waliofuja fedha za umma, kigogo PAC kuwasilisha majina kwa JPM, mifuko hifadhi jamii, IPTL, TPA, TTCL zaguswa... *Endelea ukurasa 2 & 3*




Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kukabidhi ripoti yake, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



## BAA LA CORONA

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, amelazwa hospitalini ili kufanyiwa vipimo vya ugonjwa wa virusi vya corona, siku 10 baada ya kukutwa ameambukizwa katika ofisi yake. BBC

* Epuka mikusanyiko ya watu
* Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
* Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
* Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo.

## WAGONJWA WA CORONA NCHINI SASA WAFIKIA 24

UKURASA 8

# Makonda aagiza kamata wazururaji kisa corona


UKURASA 4



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store

MICHEZO YONDANI AVUTWA SIMBA UK.32

MAONI, KATUNI UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza kwa njia ya video na Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa ya mipakani kuhusu ugonjwa wa corona akiwa ofisini kwake, Mlimwa jijini Dodoma, jana. Habari Uk. 27. PICHA: OWM

# Vichwa ngumu sasa kitanzini

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2018/19, imewaweka kitanzini vigogo wa mashirika na taasisi za umma, baada ya Bunge kuweka bayana kwamba litawasilisha kwa Rais John Magufuli majina ya waliobainika kuendelea kufuja fedha za umma.

Jana alasiri, ripoti hiyo ilikabidhiwa bungeni na baadaye CAG, Charles Kichere, kukutana na waandishi wa habari na kutoa mukhtasari wake.

Katika mukhtasari huo, CAG Kichere, alibainisha kuwapo kwa dosari nyingi katika ukusanyaji na utumiaji wa fedha za umma pamoja na kutozingatiwa kwa sheria na taratibu katika ukusanyaji na ukusanyaji wa fedha hizo.

Kutokana na hali hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, alisema kamati yake kwa kushirikiana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), itakutana na CAG na kuchambua majina ya vigogo ambao wameonekana kuendelea kufuja fedha za umma ili wayawasilishe kwa Rais Magufuli kwa ajili ya hatua zaidi.

Alisema amesikitika kuona bado nchini ina watendaji wanaoendelea kufuja mali ya umma licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na Rais Magufuli kukusanya mapato na kudhibiti mianya ya ufisadi.

"Nimefuatilia kwa kina ripoti hii ya CAG, ninasikitika kuona bado kuna watendaji wa serikali wanaendelea kucheza na fedha za umma.

"Halafu kuna ambao tulishakaa lakini wameonekana tena. Tutakaa na CAG na kuchambua, tutapeleka majina ya hao vichwa ngumu kwa Rais ili washughulikiwe," alisema.

Katika ripoti yake hiyo ambayo ni ya kwanza tangu ateuliwe na Rais mwaka jana, CAG Kichere ameangazia hesabu za serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika ya umma, miradi ya maendeleo, ukaguzi wa ufanisi, ukaguzi wa mifumo ya Tehama na ripoti 12 za ukaguzi wa ufanisi zinazohusu sekta mbalimbali.

Kichere alibainisha kuwa wakati anakagua hesabu za Jeshi la Polisi, alibaini kiasi cha Sh. milioni 196.13 kililipwa kwa watumishi 11 ambao walishafariki dunia, kufukuzwa kazi au kustaafu kinyume cha matakwa ya Kanuni ya 113(3) ya Kanuni za Fedha za Umma ya Mwaka 2001.

CAG pia alisema amebaini uwapo wa watumishi 638 Ofisi za Tamisemi ilhali mahitaji ni watumishi 504, hivyo kufanya ongezeko la zaidi ya watumishi 134.

Wakati hali ikiwa hivyo Tamisemi, CAG alisema amebaini kuna upungufu wa watumishi 9,660 katika wizara, sekretarieti za mikoa, tume na balozi, hivyo kupata ishara kwamba serikali haijafanya tathmini sahihi ya mahitaji ya watumishi wake.

"Pia, katika mapitio ya taratibu za ununuzi na usimamizi wa mikataba, nilibaini katika mwaka wa fedha 2018/19, taasisi tano za serikali kuu zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 5.46 pasipokuwa na mikataba," alisema.

Alizitaja taasisi hizo kuwa ni Jeshi la Wananchi (JWTZ) Sh. bilioni 4.242, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Sh. miloni 28.667, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Sh. milioni 245.462, Jeshi la Kujenga Tafa (JKT) Sh. milioni 205.677 na Wizara ya Ulinzi kwenye mradi mwingine wa Sh. milioni 737.974.

Pia, alisema amebaini upungufu katika mkataba wa ukusanyaji mapato kwenye Uwanja wa Taifa na Uhuru jijini Dar es Salaam kati ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Selcom Paytech PLC, akisema wizara haina mtaalamu wa Tehama anayesimamia stakabadhi zinazouzwa kupitia mfumo wa kielektroniki.

CAG Kichere alisema ukaguzi wake umebaini matumizi ya Sh. bilioni 5.06 yaliyofanyika bila kuwapo kwa nyaraka toshelezi kulikokwamisha mawada ya ukaguzi wake katika taasisi 39.

Kuhusu ukaguzi wake kwenye balozi, CAG alisema amebaini kuwa Balozi za Tanzania katika nchi za Brazil, Algeria na Sweden zilitumia Sh. bilioni 1.02 kukodi nyumba za makazi, kiasi ambacho kingeepukika kwa kukarabati nyumba za makazi zilizochakaa.

# Mamilioni CUF yakopeshwa redio kiajabu

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini Chama cha Wananchi (CUF) kimekopesha mamilioni ya shilingi kwa kituo cha redio jijini Tanga bila kuzingatia taratibu za kisheria.

Akitoa mukhtasari wa ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2018/19, CAG Charles Kichere, aliwaambia waandishi wa habari jijini hapa jana kuwa amebaini Bodi ya Wadhamini ya CUF ilitoa mkopo wa Sh. milioni 45 Januari 3, 2017 kwa kituo cha redio mkoani huko makubaliano ya kurejesha kwa kipindi cha miaka mitatu mpaka Januari 3, 2020.

Vilevile, CAG alisema chama kiliidhinisha na kutoa mkopo mwingine wa Sh. milioni 35 Februari 16, 2018 kwa kituo hicho cha redio kwa makubaliano ya kulipa kwa kipindi cha miaka miwili mpaka Februari 16, 2020.

"Pia, mkopo mwingine wa Sh. milioni tano ulitolewa kwa kituo hicho Mei 28, 2019 wenye masharti ya urejeshwaji kwa kipindi cha siku 10 kuanzi tarehe ya kutoa mkopo.

"Hata hivyo, mikopo yote haikuwa na dhamana, na hadi kufikia Januari 2020 wakati wa ukaguzi, kiasi chote cha milioni 85 hakikuwa kimerejeshwa.

"Vilevile, nilibaini kuwa katika makubaliano ya mikopo hiyo, kituo hicho cha redio kiliwakilishwa na wakurugenzi wake watatu ambao pia ni wakurugenzi wa CUF. Katika mazingira haya, upo mgongano mkubwa wa kimaslahi kwenye makubaliano yaliyofanyika," alisema.

**CCM YAMFIDIA MPANGAJI**

CAG pia alisema amebaini Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ilimwondoa mpangaji bila kufuata taratibu, na matokeo yake, mpangaji huyo alionyesha nia ya kufungua kesi ya madai ya kulipwa fidia ya Sh. milioni 800.

Hata hivyo, CAG alisema jumuiya hiyo ililipa Sh. milioni 60 kama fidia ya hasara baada ya kufanya mazungumzo nje ya mahakama na suala hilo kumalizika.

Katika ukaguzi wake kuhusu hesabu za mamlaka za serikali za mitaa, CAG alisema amebaini Sh. milioni 167.44 zililipwa kwa watumishi waliokoma utumishi wao kutokana na sababu mbalimbali kama vile kustaafu, kufariki dunia, utoro kazini na kufukuzwa kazi.

HABARI KITAIFA




Kijiko kikiondoa mchanga uliojaa pembeni ya daraja la Jangwani, katika Barabara ya Morogoro, jijini Dar es Salaam jana, kutokana na mafuriko ya Mto Msimbazi yalisababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yadaiwa tril. 2.4/- NSSF, PSSSF

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

DENI la serikali kwa mifuko ya hifadhi ya jamii na bima ya afya limefikia Sh. trilioni 2.42, imeelezwa.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, aliyasema hayo jana jijini hapa alipotoa mukhtasari wa ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19.

Alisema mifuko yote ya hifadhi ya jamii na bima ya afya ina madai makubwa ambayo ni chechefu, mengi ya madai hayo ni kwa serikali na taasisi zake.

Alibainisha kuwa hadi Juni 30, 2019, mifuko hiyo ilikuwa inaidai serikali pamoja na taasisi zake kiasi cha Sh. trilioni 2.42. Kati yake, NSSF Sh. trilioni 1.47, PSSSF Sh. bilioni 731.4 na NHIF Sh. bilioni 220.39.

CAG pia alisema amebaini kutokuwapo uhakika wa urejeshwaji wa mkopo kwa watumishi walioondoka katika Mfuko wa NHIF. Alisema kuwa hadi Juni 30, 2019, mfumo ulikuwa unadai mkopo kwa watumishi walioacha kazi kiasi cha Sh. milioni 974. 2.

Vilevile, alisema amebaini kuwa hadi kufikia Juni 30, 2018, mifuko ya PSSSF na NHIF ilikuwa na jumla ya kiasi cha amana na riba Sh. bilioni 118.8 kilichoiva katika Benki ya Uwekezaji (TIB).

Hata hivyo, alisema amebaini benki hiyo ina tatizo la ukwasi ambao unasababisha kushindwa kulipa amana zilizoiva kwa wakati. Alibainisha kuwa mfuko wa NHIF ulikuwa na kiasi cha Sh. bilioni 16.8 na PSSSF bilioni 95.

CAG pia alisema amebaini taasisi 34 kati ya 148 alizozikagua, zina fedha ambazo zinashikiliwa na wadaiwa sugu zinazofikia Sh. bilioni 224.69.

Alisema mengi ya madeni hayo yanatokana na mauzo ya huduma mbalimbali kwa wateja na anaamini yatapungua kwa kiasi kikubwa ikiwa taasisi zitakusanya mapato kupitia mfumo, kufuata mkakati wa malipo ya kabla ya huduma na kuongeza nguvu katika mbinu za kukusanya madeni.

**DENI LA SERIKALI MSD**

CAG pia alisema amebaini kuwa hadi Juni 30, 2019, deni la serikali kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) limeongezeka kwa kiasi cha Sh. bilioni 16.18 kutoka Sh. bilioni 37.45 za mwaka uliopita.

"Nina mashaka kuwa ukwasi wa bohari unazidi kushuka, hivyo kuathiri utekelezaji wa mipango mbalimbali ikiwamo usambazaji wa dawa na vifaa tiba kwa jamii pamoja na utekelezaji wa mipango yake mbalimbali," alisema.

# TTCL inavyotengeneza hasara mabilioni

**Na Sanula Athanas,**

**DODOMA**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini Shirika la Mawasiliano ya Simu (TTCL), linatengeneza hasara kubwa kutokana na mkataba lililoingia ili kutanua mtandao wake.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, kuhusu mukhtasari wa ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, CAG Charles Kichere, alisema shirika liliingia mkataba na Kampuni ya MIC Tanzania kwa ajili ya kupitisha mawasiliano (roaming) yake kitaifa kuanzia Julai 14, 2018.

Alisema dhumuni lilikuwa kutanua ufikaji wa mtandao nchi nzima na kuongeza mapato, lakini amebaini TTCL ilikuwa ikitoza bei rahisi kwenye vifurushi inavyouza kwa wateja wake kuliko bei ambayo inalipa kwa mujibu wa mkataba.

"Hii imesababisha TTCL ipate hasara ya Sh. bilioni 1.11 katika mkataba wa kupitisha mawasiliano pekee. Pia, kama TTCL itachukua hatua ya kuongeza bei ili kupunguza hasara, kuna uwezekano wa kupoteza mapato kutokana na ushindani mkali uliopo katika soko," alisema.

CAG alibainisha kuwa TTCL inauza kifurushi cha GB moja kwa Sh. 1,500 ilhali inakinunua kwa MIC kwa Sh. 2,500, hivyo kutengeneza hasara ya Sh. 1,000.

Vilevile, alibainisha kuwa mapitio ya michango iliyofanywa na TTCL kwenda kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) yalionyesha ilikuwa ni Sh. bilioni 1.075 ikiwa ni asilimia sita ya mishahara ya watumishi.

Alisema hali hiyo ni kinyume cha Kifungu cha Tisa cha Sheria ya Bima ya Afya ya Mwaka 1999 kinachotaka michango igawanywe sawa kati ya mwajiri na mwajiriwa, hivyo TTCL ilingia gharama ya ziada ya Sh. milioni 537.5 kwa kuchangia asilimia tatu alizopaswa kuchangia mwajiriwa.

**HESLB, TPA MATATANI**

CAG pia alisema alibaini mashirika matatu yalilipa malipo mbalimbali yenye jumla ya Sh. milioni 829.45 kwa watumishi walioacha kazi au kuhama kutokana na sababu mbalimbali.

Katika hilo, alisema Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ililipa kiasi cha Sh. milioni 398.14, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) Sh. milioni 324.01 na Mamlaka ya Bandari (TPA) ikaripoti mikopo ya Sh. milioni 107.3 kama mikopo iliyotolewa kwa watumishi ambao tayari wamekwisha acha kazi.

**POSHO ZA LIKIZO**

CAG Kichere pia alisema amebaini Mamlaka ya Maji Dar es Salaam (Dawasa) ililipa kiasi cha Sh. bilioni 1.58 kama posho za mwezi za ziada kinyume cha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma zinazotaka watumishi kupewa posho ya usafiri wakati wa likizo mara moja kila baada ya miaka miwili.

**"Hii imesababisha TTCL ipate hasara ya Sh. bilioni 1.11 katika mkataba wa kupitisha mawasiliano pekee. Pia, kama TTCL itachukua hatua ya kuongeza bei ili kupunguza hasara, kuna uwezekano wa kupoteza mapato kutokana na ushindani mkali uliopo katika soko," alisema.**

SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)

KUMBUKUMBU

Bodi ya Wakurugenzi Menejimenti pamoja na Wafanyakazi wote wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) inawatakiwa Watanzania wote Maadhimisho mema ya kumbukizi ya kifo cha Muasisi na Rais wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, SHEIKH ABEID AMANI KARUME



SHEIKH ABEDI AMANI KARUME

TANESCO Tunayaangaza Maisha yako

Mkurugenzi Mtendaji
Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)
Plot No. 114, Block G, Dar es Salaam Road, P.O.Box 453 Dodoma.
Simu:- +255 262323457 | Barua pepe:- info@tanesco.co.tz | Tovuti:- www.tanesco.co.tz

tanesco_official_page umemeforum.blogspot.com tanescoyetultd tanescoyetu



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi (mwenye Miwani), akitoa elimu kwa kinamama wafanyabiashara wa viazi lishe (hawapo pichani), katika soko maarufu la viazi lishe katika Kitongoji cha Kideka, Kijiji cha Nkunikana, kuhusu jinsi ya kunawa mikono , ili kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19, akiwa katika ziara ya kikazi wilayani Ikungi jana. Kulia ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Edward Mpogolo na (kushoto) ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Justice Kijazi. **PICHA: JOHN MAPEPELE**

# Makonda atangaza kukamata wazururaji

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametangaza kuanza kukamata wazururaji na moja ya kazi watakazofanya ni kufagia maabusi kama adhabu.

Makonda aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa mkoa huo una kazi nyingi ambazo wanalipa watu gharama kubwa hivyo wameona wazururaji wazifanye.

Wakati Makonda akiyasema hayo, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kupitia Mkurugenzi wake, Anna Henga, alisema sheria hiyo ni mbaya kwa sababu utekelezaji wake unaweza kumkamata mtu ambaye siyo sahihi.

Akizungumza jana, Makonda alisema, "Tutawakamata ili ukiamka asubuhi kwenda kuzurura ujua Makonda atakunyakua ufanye kazi, zipo kazi zaidi ya saba ambazo tumeziainisha moja wapo tutakuepeleka maabusi ukatusaidie kusafisha.

"Hatukufungi utafanya kazi siku nzima unarudi nyumbani, kama utakuwa na tabia ya kuzurura kila siku basi utakuwa mfanyakazi bora."

Makonda alisema wakati wakipambana na virusi vya corona huku wakielimisha watu kunawa mikono wanataka na jiji hilo liwe safi.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa wakiamka asubuhi na kuanza kuzurura mtaani bila ya kufanya kazi yoyote.

Aidha, alisisitiza wananchi wafanye badala ya kujifungia ndani kwa kuhofia kupata corona.

"Wangapi wameacha kutongoza kwa sababu ya ukimwi, kwa nini tunatafuta mbinu za kutafuta kinga ili kujilinda, tushindwe kujilinda suala la kunawa mikono tu, corona kinaua, kifua kikuu, kinaua.

"Kama mambo mengine yanahusu mahusiano, tumetafuta kinga ya tukikosa unamtumia hata mtu wa Uba akakuletee zana, niwaeleze kwa sasa zana ni vitakasa mikono ili kuepuka corona."

Hata hivyo, alisema waandishi wa habari hawajaacha kutoa habari kwa sababu wanajua ndiyo chanzo cha kipato chao na kuwataka wengine nao wafanye hivyo.

"Kikubwa unapotoka kwenda kwenye shughuli zenu, hakikisheni mnazingatia na kufuatilia taratibu na tahadhari zote zinazotolewa na Wizara ya Afya (Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) dhidi ya corona,"

Alisisitiza kuwa, uwezo wa kujilinda ni wa gharama nafuu ambao unamtaka mtu kuhakikisha ananawa mikono kwa maji yanayotiririka kwa kutumia sabuni za maji au vitakasa mikono na kuepuka mikusanyiko.

Kuhusu ziara anazozifanya mkoani humo huku kukiwa na katazo la mikusanyiko, Makonda alisema kila anakokwenda katika mkoa wa Dar es Salaam ni ofisi yake.

"Ninapokuwapo hapa nipo ofisini (Mlimani City), shughuli yangu kubwa ni kuhakikisha mambo ya maendeleo yanafanyika huku watu wakizingatia namna bora ya kujilinda dhidi ya corona.

Makonda aliwataka wanaojadili ziara zake kwenye mtandao ya kijamii waachwe kwa sababu wanaweza kumjadili, lakini kumbe wanafuata masharti yanayotolewa.

"Unakuta mtu anapenda kusema tu, kwa sababu ndiyo hulka ya binadamu, waacheni waseme, lakini waandishi hakikishieni kwamba biashara zinafanyika na sisi hatufungi mpaka Rais (John Magufuli) atupe maelekezo mengine, alituelekeza watu wafanye kazi," alisema.

Makonda aliwajibu wale wanaosema ataugua corona kwa kuwaeleza kuwa, ikitokea hivyo basi ni kwa mapenzi ya Mungu kwa sababu hawezi kuwa muoga na kujifungia ndani.

"Siwezi kuwa muoga nikajifungia ndani nishindwe kuhudumia watu milioni sita katika mkoa wangu kwa kuogopa corona.

"Nitaendelea kufanya kazi na afya yangu ipo mikononi mwa Mungu, anajua lini nitaugua au nitakufa kwa ugonjwa gani, siwezi kuwa muoga wa corona, mimi ni mwanaume natoka ili kuingia mapambanoni."

Akitoa ufafanuzi zaidi, Henga alisema: "Mtu anakwenda kazini au anafanya mazoezi barabarani utawatambuaje kama ni mzururaji au wapo kwenye shughuli za kila siku.

"Tuliwahi kupeleka sheria hii Mahakama Kuu kuipinga ingawa haikufanikiwa kusikilizwa, sheria hii ni ya kumdhalilisha mtu."

Kaimu Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Camilius Wambura, alisema alichokisema Makonda ni sehemu ya kazi zao za doria na misako za kila siku ambazo Jeshi la Polisi huzifanya.

"Siyo jambo jipya, upo utaratibu wa kukamata, tafsiri ya kauli ya Makonda kwetu ni kwamba ametusisitizia kuongeza misako zaidi ili wasiokuwa na shughuli wakamatwe.

"Wasiokuwa na shughuli ni chanzo cha uhalifu, hatuwakamati kwa sababu ya corona bali pia kulifanya jiji letu kuwa salama, tutawakamata," alisema.

# Wafa maji wakivusha watu Mto Msimbazi

**Na Maulid Mmbaga**

VIJANA wawili wakazi wa Gongolamboto waliokuwa wakifanyakazi ya kuvusha watu mto Msimbazi, wamefariki dunia baada ya kusombwa na mafuriko.

Akizungumza na Nipashe, baba mdogo wa marehemu, Mbegu Abdala, alithibitisha kutokea kwa vifo hivyo na kuwataja waliofariki kuwa ni Chuma (21) na Omary Salimu (19), ambao walisombwa maji Aprili 3.

Alisema chanzo cha watu hao kusombwa ni kutokana na kuvusha wananchi katika mto huo kufuatia mvua kunyesha na baadaye maji kuwazidi nguvu na kuwazoa.

"Hii sehemu watu wanapovuka kulikuwa na daraja, lakini lilisombwa na maji siku chache zilizopita, hivyo vijana baadhi hufanya shughuli ya kuvusha wananchi wasiotaka kukanyaga maji, na wanajipatia kipato cha kuendesha maisha yao, Chuma na Omary, walikuwa wanavuka kwenda ng'ambo ya pili kubeba watu hapo ndipo maji yalipowazidia na kuwasomba," alisema.

Alisema baada ya kusombwa waliwatafuta bila mafanikio na mwili wa Chuma ulipatikana baada ya siku moja na Omary ulipatikana jana na mama mmoja aliyekua anakata kuni na kuona mguu wa marehemu ukiwa umejitokeza juu pembezoni mwa mto huo.

Alisema aliwaita watu na kumtoa wakagundua kuwa ni yeye.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo Said Shayo, mkazi wa Ulongoni, Gongolamboto alisema, alikuwa sehemu ya tukio na alishuhudia vijana hao wakiwa wanasombwa na maji.

"Tulikuwa tumesimama karibu na mto na tuliwaona rafiki zetu wakiwa wana tapatapa kwenye maji, tulijaribu kutaka kuwaokoa, lakini tulishindwa kwa kuwa maji yalikuwa mengi," alisema Shayo.

Kamanda wa mkoa wa kipolisi wa Ilala, Zubri Chembela, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema taarifa hizo hazijawafikia kwa kuwa halikuripotiwa polisi.

**Alisema baada ya kusombwa waliwatafuta bila mafanikio na mwili wa Chuma ulipatikana baada ya siku moja na Omary ulipatikana jana na mama mmoja aliyekua anakata kuni na kuona mguu wa marehemu ukiwa umejitokeza juu pembezoni mwa mto huo.**

# HABARI KITAIFA

## Meya Ubungo atangaza kung'atuka udiwani

**Na Elizabeth Zaya**

MEYA wa Manispaa ya Ubungo jijini Dar es salaa, Boniface Jacob, amesema hatogombea tena nafasi ya udiwani katika uchaguzi mkuu ujao wa mwaka huu, na kuweka wazi nia yake ya kugombea ubunge endapo chama chake kitaridhia.

Katika ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter, Jacob alitangaza kutokugombea nafasi ya udiwani na alipoulizwa kama ana mpango wa kugombea ubunge, alijibu atakuwa tayari kufanya hivyo kama chama chake kitaridhia.

Katika ukurasa wake huo, Jacob alisema kwa kipindi cha miaka 10 alichotumikia katika nafasi yake hiyo ya udiwani imetosha.

"Nimetangaza kung'atuka katika udiwani Kata ya Ubungo muda wa madiwani utakapoisha, sitogombea tena udiwani uchaguzi ujao,"aliandika ujumbe huo Jacob katika ukurasa wake huo.

Aliongeza: "Miaka 10 ya utumishi wangu ni kwa sababu Wana-Ubungo mlinikopesha imani, tumekuwa wote wakati wa shida na raha, mabonde na milima."

Jacob ametangaza msimamo wake huo wa kutokugombea nafasi ya udiwani huku kukiwa na tetesi zinazodai kwamba mpango wake ni kusogea katika hatua nyingine ya kugombea ubunge.

Hivi karibuni, wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo(Chadema), walikwenda nyumbani kwa Meya huyo na kumuomba agombee nafasi ya ubunge katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Wananchi waliokwenda nyumbani kwa Meya huyo kumuomba agombe nafasi hiyo ya ubunge ni wa wale wanaoishi Ubungo ambao pia walidhihirisha nia yao hiyo kwa kusaini katika karatasi waliyokuwa wamejiorodhesha.

Akizungumza na Nipashe, Jacob alisema yuko tayari kutumikia nafasi nyingine ya juu kisiasa endapo atapewa ridhaa na chama chake.

"Kwa kweli kwa kipindi hiki ambacho nimetumia katika nafasi ya udiwani kimenitosha, nimefanya mambo mengi ambayo naamini hata wananchi wameridhika, sasa nimekomaa, niko tayari kusonga mbele kidogo ili nipambane na changamoto nyingine kubwa zaidi," alisema Jacob.

Aliongeza: "Mimi ni kama kiraka, niko tayari kugombea nafasi ya Ubunge katika jimbo lolote ambalo viongozi wangu wataridhia."



Fundi chuma, Kevin Mwanyika (kulia), akimwelekeza mteja wake jinsi ya kutumia kifaa alichokitengeneza cha kunawia mikono huku ukiruhusu sabuni na maji kutoka bila ya kutumia mkono, kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona, katika ofisi yake iliyopo katika eneo la Mtwivila Kihesa mjini Iringa mwishoni mwa wiki. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Takururu Dodoma ilivyookoa mil. 297/-

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Dodoma, imeokoa kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 297 na magari matatu ya umma katika ufuatiliaji wa mradi wa maji wa Mlongia, wilayani Kondoa.

Aidha Sh. 143, 515,177 ziliokolewa kutoka kwa viongozi na wanachama 67, wa vyama sita vya akiba na mikopo (Saccos) waliokuwa wanadaiwa kwa muda mrefu.

Magari matatu yaliyookolewa ni aina ya Toyota Hiace yalichukuliwa kutoka kwa viongozi wa Saccos, moja walikuwa wanatumia kwa faida binafsi, ikiwamo ufuatiliaji wa madeni na mali za ushirika.

Mkuu wa Taasisi hiyo mkoani Dodoma, Sostenes Kibwengo, alisema kiasi kilichobaki ambazo ni Sh. 153, 600 297 kimeokolewa kwa kufuatilia na kurejesha mapato ya serikali yaliyokusanywa kwa Mradi huo wenye thamani ya Sh. 579, 323, 000 ambao ulianza mwaka 2013 na kukamilika 2014, lakini haukuwa unatoa maji hadi Takukuru ilipoingilia kati kwa Mkandarasi Leostar Engineerring Co . LTD na kumrejesha tena site ili kufanya marekebisho.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kibwengo alisema katika taarifa yake ya robo mwaka katika ufuatiliaji, wamebaini Sh. 120, 247, 164 zaidi ya thamani ya mradi huo ili arekebishe mradi utoe maji na tayari ameanza kurejesha fedha hizo.

Kibwengo alisema wanaendelea kufuatilia utokaji wa maji hayo na kujihakikishia Mkandarasi anarejesha kiasi cha fedha kilichobaki.

Alisema kiasi kilichobaki ni Sh. 153, 600, 297 kufuatia kurejesha mapato ya serikali yaliyokusanywa kwa njia ya kielektroniki, lakini hayakuwasilishwa sehemu husika.

Alisema pia wamefuatilia miradi 26 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. milion 6. 6 katika sekta ya elimu maji, ujenzi, mifugo, kilimo na umwagiliaji, mapato na utawala ambapo jumla ya Sh. milion 94. 7 zimeokolewa baada ya kuwa zimechepushwa katika miradi hiyo na hivyo kuongeza ufanisi wa utekelezaji wake.

Alisema vilevile, ufuatiliaji katika miradi hiyo wamebaini kuwa miradi minne yenye thamani ya jumla ya Sh. 261,042, 561 ina viashiria vya rushwa.

Ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo una faida kubwa kwani ni pamoja na kuokoa rasilimali zinazochapishwa.

Alifafanua kuwa wamefanya uchambuzi wa mifumo ya utendaji na utoaji huduma katika maeneo ya vyama vya ushirika, fedha, michezo na rasilimali.

Alisema lengo la kuchambua ni pamoja na kubaini mianya ya rushwa ikiwemo kufanya vikao sita vya kiutendaji ili kuweka vitu sawa.

Katika hatua nyingine, wamefanikiwa kufungua klabu 70 za kupinga rushwa ambazo wanaamini zitasaidia kutoa elimu kwa jamii juu ya kujikinga na rushwa na huo ni mkakati wa skauti.

# Wawili wafa, sita wajeruhiwa ajalini

**Na Mwandishi Wetu**

WATU wawili wamefariki dunia na wengine sita wamejeruhiwa katika ajali iliyotokea juzi kwenye barabara ya Arusha- Namanga.

Kati ya waliyofariki katika ajali hiyo, ni Inspekta wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, Enock Wange (41), na Julius Saitoti.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Koka Moita, alisema ajali hiyo, ilitokea juzi majira ya jioni katika eneo la Landakarai Kijiji cha Ranch Kata ya Olbomba Tarafa ya Longido.

Aliwataja waliyojeruhiwa ni Azaeli Mbise (37), ambaye ni dereva wa gari, Lolubare Kilesi (44-50) ,Gasto Mushi (32), daktari wa Hospitali ya Longido, Saluni Lengireri (50), Kondo Kibwana na (60), Justine Lobikeki (24).

Moita alisema chanzo cha ajali hiyo ni gari namba T.742DGP Toyota PSV Noah, mali ya Ndete Lengai kupasuka gurudumu la nyuma upande wa kulia na kuacha njia.

Hata hivyo, alisema gari hilo, lilikuwa kwenye mwendokasi na lilimshinda dereva kulimudu.

Kamanda Moita alisema hali za majeruhi ni mbaya kwa kuwa wamejeruhiwa sehemu mbalimbali za mwili na wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru) na ya Wilaya ya Longido.

Aidha, alisema miili ya waliokufa imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mount Meru.


**KUPOTOLEWA NA LESENI YA KUCHIMBA MADINI**

**JUMAA MUSSA SIMBA**

Anatangaza kupotolewa na leseni ya kuchimba madini, scale ya kupimia madini, nyundo mbili ya kusotia madini na **TIN** namba ya **TRA**. Atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi kwa namba hii **TAN/MAR/RB/243709/2020.**

115691902



MUCOBA BANK PLC
P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.
E-Mail: mucoba@mucobatz.com

**TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA DHARURA WA WANAHISA WA BENKI YA MUCOBA**

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba, kutakuwa na mkutano mkuu wa Wanahisa utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 11 mwezi wa April 2020 katika ukumbi wa **MAM –uliopo Mafinga Mjini** kuanzia saa tatu kamili asubuhi. Kutokana na mazingira ya Ugonjwa wa CORONA, kibali kimepatikana cha kufanya mkutano huu kwa kuzingatia masharti na vigezo vya Wizara ya Afya.

Ajenda ya Mkutano itakua kupewa mrejesho kuhusu uwekezaji katika Benki ya MUCOBA.

**Notisi hii imetolewa leo tarehe 07/04/ 2020**

**Mambo ya kuzingatia**

1. Mwanahisa anayetarajia kuhudhuria Mkutano huu atatakiwa kufanya hivyo kwa gharama zake mwenyewe na
2. Iwapo Mwanahisa anayeruhusiwa kuhudhuria Mkutano na kupiga kura, atashindwa kwa sababu zozote zile kuhudhuria Mkutano, ataruhusiwa kuchagua Mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata na kuzingatia taratibu na sheria za Kampuni.
3. Nakala za Makabrasha ya Mkutano zitapatikana siku ya Mkutano tarehe 11, April 2020.

**PHILIP RAYMOND PHANUEL**
**KATIBU BODI YA WAKURUGENZI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuendelee kuyakumbuka mema ya Sheikh Karume

**MMOJA** wa waasisi wa Tanzania, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, leo ametimiza miaka 48 tangu alipofariki dunia mwaka 1972.

Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Karume ndio walioziunganisha Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964 na kuundwa kwa taifa la sasa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa utayari na utashi wake huo wa kuona umuhimu wa kuunganisha nchi hizo mbili, kunamfanya awe kiongozi wa kukumbukwa kutokana na ujasiri wake, uzalendo wake na mapenzi yake kwa uafrika na Utanzania.

Itakumbukwa pia jinsi Sheikh Karume alivyoongoza harakati za Wazanzibari za kudau uhuru wao na usawa, ambazo zilianza mwaka 1957 kwa kuanzisha Chama cha Afro Shirazi (ASP).

Jitihada hizo ndizo zilizowezesha kufanyika kwa Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 26, mwaka 1964, ambayo ndiyo yaliyoondoa ubaguzi dhidi ya waafrika na kuleta usawa kwa watu wote.

Karume alishirikiana na waasisi wengine kujitoa mhanga kufanya mapinduzi hayo kutokana na kutorishishwa na uhuru bandia ambao ulitolewa kwa Zanzibar mwaka 1963, lakini ukaonekana kuwa bandia kwa kuwa waliopewa uhuru huo walikuwa vibaraka wa Sultan.

Mbali na kuongoza Mapinduzi hayo ambayo yalirejesha heshima na utu wa mwafrika, kadhalika Mapinduzi hayo yalibadili maisha ya weusi ambao walikuwa wakikosa huduma za msingi za jamii.

Karume katika uongozi wake wa kuanzia mwaka 1964 hadi mwaka 1972, aliitumia nguvu zake na akili zake zote katika kujenga Zanzibar na kuipaisha kiuchumi na maendeleo ya kijamii.

Kwa mfano, alihakikisha wananchi wanapata ajira na kuanza kutoa huduma za jamii bure ikiwamo elimu, afya, maji na hata makazi.

Ujenzi wa nyumba eneo la Michenzaji na kuwagawia wananchi kuishi bila malipo ni ushahidi mwingine kuhusiana na alivyojitolea kuhakikisha Wazanzibari wananufaika na Mapinduzi.

Wakati leo Wazanzibari na Watanzania tunafanya kumbukumbu ya Karume, hatunabudi kuenzi mambo mema aliyoyafanya kwa Taifa letu, ambayo yaliweza kutufanya tuwe taifa moja lenye amani, utulivu, mshikamano na umoja wa kitaifa.

Tunasema hivyo kwa kuwa Karume na Mwalimu Nyerere hawakusimamia kwenye maslahi yao binafsi, bali kwa nchi zao na kutambuliza mbele maslahi ya taifa, na ndiyo maana walijitoa kwa kila namna kuhakikisha watu wao wanaondokana na kupuuzwa, kudharauriwa, manyanyaso na ubaguzi.

Lakini pia tunapozungumzia Muungamo wa Tanganyika na Zanzibar, lazima Mzee Karume hawezi kuwekwa kando kutokana na msimamo wake wa kutoogopa Zanzibar kupoteza maslahi yake.

Hili ni moja ya mambo ambayo yameweza kuufanya muungano huu kudumu kwa miaka mingi na kuendelea kuwa imara, tofauti na mataifa mengine, ambayo yaliungana na baada ya muda mfupi muungano wao kusambaratika.


Jambo la kupongeza ni kuwa viongozi wakuu wote wa pande zote za muungano waliofuata baada ya waasisi hao wameendelea kuuenzi na kuulinda muungano wetu, hivyo kulifanya taifa letu kuendelea kuwa imara na linaloheshimika duniani.

Kwa upande wa maendeleo, tunashauri viongozi waliopo sasa na wajao wa Zanzibar waendelee kumuenzi Karume kwa kuendeleza jitihada alizozifanya kusukuma maendeleo na ustawi wa Wazanzibari.

Kazi nzuri aliyoifanya Rais wa sasa, Dk. Ali Mohamed Shein, hainabudi kupongezwa, kwa kuwa kwa takribani miaka tisa na nusu ya viongozi wake, ametekeleza miradi mingi ya maendeleo ya wananchi, ikiwamo hutoa huduma bure ya elimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Komu mbona mapema hivi unakimbilia wapi?

**MBUNGE** wa Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Antony Komu, ametangaza kukihama chama hicho na kujiunga na NCCR-Mageuzi.

Pamoja na kutangaza kuachana na chama hicho, mwanasiasa huyo anasema ataondoka Chadema mara atakapomaliza kipindi chake cha ubunge na kwamba atagombea tena kupitia NCCR Mageuzi.

Komu amechukua hatua hiyo huku akidai kwamba ndani ya Chadema kumekuwa hakuna uhuru wa kutoa maoni na kuitwa msaliti hata pale anaposhauri mambo yenye tija ndani ya chama.

Hata hivyo, pamoja na kutangaza kuhama, anaiomba Chadema itumie busara kumwacha amalizie majukumu yake ya ubunge kwa muda uliobaki, kwa vile bado anahitaji kuwatumikia wananchi wake.

Baada ya kauli hiyo, Chadema kupitia kwa Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje, John Mrema, kinasema kitakaa vikao na kutoa taarifa rasmi kwa umma juu ya jambo hilo.

Kwamba kauli za mbunge huyo zinaonyesha haamini chama kinasimamia nini na analazimika kubaki ndani ya chama kwa kuwa anasubiri posho zake za bunge na kiinua mgongo.

Nikirudi kwenye jambo ambalo ninataka kulizungumzia, ni kwamba sioni kama kulikuwa na haja ya kuharakisha kutangaza kuhama chama wakati bado anahitaji kuwatumikia wananchi.

Mbunge anatangaza kuhama, halafu anaomba busara itumike kumwacha aendelee kubaki ndani ya chama hadi amalize ubunge wake ndipo aondoke! Haraka ya nini wakati bado upo upo Chadema?

Kwa kawaida mtu anakuwa mbunge kupitia chama kilichompa ridhaa ya kuwania nafasi hiyo, sasa huyo ametangaza kujiondoa lakini kwa utaratibu ambao anataka aendelee kukumbatia ubunge hadi bunge litakapovunjwa.

Binafsi sioni ni kwa nini amefanya haraka kutangaza kuhama chama wakati bado anataka kuendelea kuwa mbunge na anatambua kuwa akihama atakuwa amepoteza sifa za kuendelea kushika nafasi hiyo.

Hii inatokana na ukweli kwamba nafasi hiyo mwanasiasa anaipata kupitia chama cha siasa, hivyo anapokihama na kwenda kujinga na kingine hawezi kuondoka nayo bali anakuwa siyo mbunge tena.

Kama Chadema watakaa na kuamua kumuondoa kwenye chama, atakuwa ameshindwa kuwatumikia wananchi kwa miezi iliyobakia na pia hata posho zake za mwisho nazo atakuwa amezikosa.

Ninadhani kwamba washauri wake waliomwambia atangaze mapema kuhama chama wamefanya vibaya, kwani sasa anasubiri kile alichokiita busara ya Chadema kuendelea kuwa ndani ya chama hicho.

Maana yake ni kwamba chama hicho kikiamua kumfuta uanachama, atakuwa amekwama kutimiza malengo yake ambayo amesema ndiyo yamembakiza kwa muda ndani ya Chadema.

Lakini pia ikumbukwe kwamba suala la mwanachama kuhama chama ni haki ya kidemokrasia, ambayo awe mchanga hata mkomavu, ana haki ya kufanya hivyo pale inapobidi.

Inawezekana wapo baadhi ya wanasiasa wanaohama vyama kwa sababu ya ubinafsi kwa kujiona kuwa wao ndiyo wenye haki ya kuongoza, au kuteuliwa kugombea nafasi fulani za uwakilishi.

Katika hilo, wengine wanahama vyama kwa sababu ya kukimbia migogoro, wapo wanaoenda kutafuta nyadhifa, maslahi na hata kufikia kuviponda vyama wanavyotoka.

Wanasiasa wa aina hiyo wasipochaguliwa au kuteuliwa, huamua kuhama vyama vyao na kujiunga na vingine, lakini pia jambo la kuzingatia ni kwamba suala la kuhama chama ni haki ya kidemokrasia.

Hata hivyo, dhana ya kuhama chama inaweza kuwa inachangiwa na kuvutiwa na sera, ikijumuisha tunu, malengo, falsafa, itikadi zake, hasa kule wanakokwenda, ila kikubwa zaidi ni suala la haki ya kidemokrasia.

Inawezekana wapo baadhi ya wanasiasa wanaohama vyama kwa sababu ya ubinafsi kwa kujiona kuwa wao ndiyo wenye haki ya kuongoza, au kuteuliwa kugombea nafasi fulani za uwakilishi.

Wengine wanahama vyama kwa sababu ya kukimbia migogoro, wapo wanaoenda kutafuta nyadhifa, maslahi na hata kufikia kuviponda vyama wanavyotoka.

Wanasiasa wa aina hiyo wasipochaguliwa au kuteuliwa, huamua kuhama vyama vyao na kujiunga na vingine, lakini pia jambo la kuzingatia ni kwamba suala la kuhama chama ni haki ya kidemokrasia.

## HABARI KITAIFA

### Tarura itatukumbuka lini Wanakerenge?

*MHARIRI,*

*SISI wakazi wa Kijiji cha Kerenge Kibaoni mkoani Tanga tuna mengi yanayotuumiza lakini kinachotukera wakati huu wa mvua ni ubovu wa barabara inayotoka Kerenge hadi Korogwe ambako ndiko yaliko makao makuu ya wilaya na hospitali ya Magunga.*

*Tunapata shida licha ya kwamba ni wazalishaji wakubwa wa mahindi, maharage, mpunga na matunda hasa machungwa , machenza na mananasi kutokana na ubovu wa barabara hatuwezi kuyafikisha sokoni.*

*Vijiji vingi vinategemea barabara hii wapo wakazi wa Mianzini, Kwa Mndolwa, Kwa Meta hadi Korogwe mjini ni shida na kila mwaka tumekuwa tukiomba barabara ichongwe na iwekewe lami.*

*Tunaiomba tena serikali na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) kukumbuka wakazi wa vijiji hivi katika mwaka wa fedha wa 2021 ili nasi tujivunie mafanikio ya kazi zetu hasa kilimo.*

***Ni sisi wakazi wa Kerenge.***
***P.O.BOX 169***
***Korogwe***

### Muhali ukomeshwe kulinda wasichana

*MHARIRI*

*SISI tunasoma na kwa miaka mingi tumekuwa tukisikia kuwa mabinti wakiwamo wanafunzi walipewa ujauzito na hatma zao kuvurugwa, lakini kesi hazifiki polisi wala mahakamani, kisa familia ya mwanaume na ya binti zilitengeneza na kumaliza mambo.*

*Kutengeneza huko ni kutafuta suluhu baina ya ndugu wa binti aliyebakwa na kupata mimba au mtoto aliyelawitiwa kinachoendelea watuhumiwa kulipwa fedha au kupewa zawaid ili wasichukue hatua.*

*Wengine pia hukubaliana kuwa kama wakifika mahakamani washitakiwa na washitaki wasijitokeze na hata wakafika kortini wasitoe ushirikiano hivyo kesi hufutwa kwa kukosa ushahidi.*

*Wakati huu wa corona ambao watoto wetu wako likizo tuwe makini hayo yasitokee ili tusiwaangamize watoto wa mimba zisizo na sababu. Lakini pia tupige vita na kutokomeza mienendo kama hiyo kisheria.*

*Ili kuondokana na tatizo hilo la kufichiana siri kuna haja ya kutunga sheria ya kudhibiti muhali ili watoto wetu wasome na kumaliza elimu ya msingi na sekondari.*


***Daniela na Pascholina***
***Arusha***

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Uharibifu huu wa ardhi barabarani unatisha

**Na Gwamaka Alipipi**




'TUNZA mazingira yakutunze' si msemo mgeni masikioni mwako, yawezekana umewahi kuusikia sehemu ukitajwa.

Iko hivi, unaposafiri kutoka Dar es Salaam kuelekea mikoani, hususani mikoa ya kusini au kaskazini kwa wale wanaotumia barabara za mikoa hiyo, watakubaliana na mimi kuwa kumekuweko na mabadiliko tele ya muonekano kando kando ya hiyo barabara.

Awali, barabara za mikoa hiyo ilikuwa imezingirwa na misitu midogo kwa mikubwa na maeneo machache yalikuwa ni makazi ya watu. Lakini leo hii, ni maeneo machache sana ambayo utaona ile misitu iliyokuwa ya asili, mingi imefyekwa kwa kigezo cha uendelezaji maeneo na sehemu nyingine kunaonekana kabisa kwa umbali wa upeo wa macho.

Huu ni mfano mmoja tu kati ya mifano mingi ambayo nimeiona katika mikoa mbali mbali ambayo ilikuwa na maeneo mengi ambayo kwa kipindi cha nyuma yalikuwa bado hayajaendelezwa.

Imekuwa ni kawaida kwa serikali kusisitiza kuhusu uendelezaji mashamba, tujiulize maswali machache, kwanza hii dhana ya kuendeleza mashamba ni mpya au ni ya muda mrefu? Dhana hii inatokana na nini hasa? Mwongozo wa kuendeleza mashamba ukoje? Nani anatakiwa kusimamia dhana hii? Ni nini matokeo yake kwetu na kwa vizazi vijavyo?

Nikianza na dhana ya umiliki wa mashamba utaona mashamba mengi ya maeneo ya vijijini yana umiliki wa aina nyingi, Hapa tutaangalia umiliki wa aina tatu tu.

Umiliki wa kwanza ni ule wa wanakijiji mmoja mmoja ambapo hulima kufuatana na misimu, aina ya mazao na pia masoko. Mashamba haya kimsingi umiliki wake ni ule wa kiasili wa kurithi na wakati mwingine kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, basi watu wanahamia mahali wanaanza kupalima.

Umiliki wa pili ni ule wa watu wanaojulikana kama wageni ambao sio wakazi wa kijiji kile nao hununua mashamba madogo madogo. Hawa makazi yao wengi ni mijini, huenda kununua sehemu katika vijiji kwa kuuziwa na wanavijiji wenyewe na kuwapo na idhini ya uongozi wa kijiji.

Umiliki huu una matatizo matatu, la kwanza ni ununuzi usio na malengo ambao kutokana na wimbi la watu kutaka tu kumiliki ardhi. Wengine wananunua hizi sehemu ili pindi wanapostaafu pawe ni kama sehemu ya kianzio cha uwekezaji.

Umiliki wa tatu ni ule wa uwekezaji, umiliki huu maeneo yake ni makubwa, na pengine makubwa sana. Hufuata ngazi mbalimbali hadi mwekezaji kupamiliki.

Wanaomiliki wana malengo pengine yaliyo wazi na wanakijiji hujua tangu mapema malengo yenyewe. Umiliki huu mara nyingi hufuata sheria zilizopo na hii ni pamoja na kufuata hatua za kisheria kumiliki eneo,

kupata hati na wakati mwingine kupata kibali cha kituo cha Taifa cha Uwekezaji. Maeneo haya mara nyingi huanza kazi kwa upembuzi yakinifu na pia kupata vibali toka Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (Nemc) ili kuona athari za kimazingira za mradi husika na hatua zitakazochukuliwa na mwekezaji kupunguza athari hizo.

Pia wamo wale ambao wanaanza kama wawekezaji, lakini uwekezaji unakwama aidha kwa sababu mbali mbali. Lakini pia wamo wale ambao kwa malengo mabaya wanachukua mashamba labda ili kupata mikopo mikubwa kisha kuyatelekeza.

Kila umiliki una changamoto zake na namna ya kuzishughulikia. Lakini changamoto ambayo naiona ni kubwa, ni ile ya kutunza maeneo yetu ili yaweze kuwa mazuri ya kutosha kurithiwa na vizazi vijavyo. Utunzaji wa Mazingira.

Umiliki wa mwanakijiji mmoja mmoja athari hizi hazionekani maana aidha wanafundishwa au wanajua namna ya kuweka mazingira kuwa endelevu kwa kupanda miti na kuzuia mmomonyoko wa udongo. Pia wanajua mahitaji yao ya miti kwa ajili ya matunda na shughuli nyingine za kimaisha.

Kumekuwapo na kampeni kubwa ya kusafisha mashamba pori. Kampeni hii inalenga kuweka mashamba katika hali ya usafi. Lakini utekelezaji wa kampeni hii unaonekana kuwa na changamoto nyingi, kubwa ni ile ya kuharibu mazingira ambapo usimamizi wake haujaangalia athari za kimazingira. Miti inakatwa ovyo, misitu inateketea, na uoto wa asili unaangamia.

Kampeni hii inasimamiwa bila kuwapo miongozo bayana ya maana halisi ya kuendeleza mashamba. na wale wanaoitekeleza, hususani wale ambao wengi wao ni wageni, wanatumia nguvu kubwa kusafisha, wakiacha nyuma yao ardhi nyeupe kabisa isiyokuwa na miti ambayo huleta mvua, uoto ambao utazuia mmomonyoko na vivuli na chakula ambavyo vitatunza viumbe hai rafiki wa mazingira.

Matokeo yake ni kama yanavyoonekana katika pembezoni mwa barabara za mikoa niliyoitaja hapo juu na nyinginezo ambapo misitu imekatwa, mashamba yamesafishwa kwa kisingizio cha uendelezaji mashamba huku yakiacha ardhi tupu yenye rutuba ikiharibika.

Ni vema mamlaka husika zikatoa maelekezo maalum kwa viongozi wa vijiji na wasimamizi wa undelezaji huu juu ya namna bora ya kuendeleza mashamba bila kuathiri mazingira.

Maelekezo haya yalenge katika kutunza miti ya asili, kupanda miti mipya, kupanda miche na mimea ambayo itazuia mmomonyoko wa udongo na pia kuhakikisha viumbe hai rafiki wa mazingira vinatunzwa. Visingizio kuwa mashamba pori yana athari kwa vijiji husika inaweza kuwa kweli lakini kisiwe ndicho chanzo cha kuanzisha majangwa yasiyotarajiwa.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Askofu ashauri wenzake kujali corona kuliko sadaka

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

RAIS wa Chama cha Wachungaji, Maaskofu, Manabii na Mitume (TPA) ambaye pia ni Askofu Mkuu wa Kanisa la Spiritual Pentecoste Church of Tanzania (SPCT), Musa Mlawi, amewataka viongozi wa madhehebu ya dini kuacha tamaa ya kupata sadaka nyingi wakati huu wa janga la corona.

Aidha, amesema kuwa badala ya viongozi wa dini kuwaza kupata sadaka nyingi wakati huu, wanatakiwa kutafuta namna nzuri ya kuwasaidia waamini kuepukana na maambukizi ya corona katika makanisa.

Askofu huyo aliyasema hayo jiji hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya nafasi ya makanisa katika kukabiliana na maambukizi ya corona.

"Tunatakiwa kuacha tamaa ya kupata sadaka nyingi, bali tuweke utaratibu wa usalama wa waamini wetu pamoja na sisi viongozi wa dini," alisema Mlawi.

Aliiomba serikali kuwapunguzia kodi wafanyabiashara katika kipindi hiki kwani janga hili limeathiri kwa kiasi kikubwa uchumi wa dunia.

Vilevile, alisema katika kuhakikisha kuwa corona inatokomezwa, wameandaa maombi ya kuliombea taifa yatakayofanyika Aprili 16 na 17, mwaka huu.

"Maombezi haya yatafanyika jijini Dodoma na wengine watafanya katika makanisa yao, siyo mkusanyiko kama ambavyo imezoeleka ili kuondokana na uwezekanao wa maambukizi mapya ya corona kwa Watanzania," alisema Askofu Mlawi.

Pia, alisema serikali inatakiwa kuwachukulia hatua kali wote ambao wanapuuza juhudi zinazofanywa za kukabiliana na corona, na kuwataka waumini wao kuwapuuza watu hao.

Alisema katika maombezi hayo pia wataombea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanya Oktoba 2020.

Akizungumzo juu ya uchaguzi mkuu mwaka huu alisema viongozi wa dini hawatakuwa tayari kuungana na chama chochote kinacho onyesha dalili za uvunjifu wa amani.

"Navitaka vyama vya siasa kuhakikisha kuwa vinamtanguliza Mungu katika maandalizi ya uteuzi wa wagombea katika majimbo pamoja na kata," alisema.



Mchuuzi wa mikate akiwa ameisheheni kwenye pikipiki yake, akitafuta wateja katika eneo la Kitunda jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Inspekta anayetuhumiwa kwa rushwa ajitetea

**Na Hellen Mwango**

INSPEKTA wa Polisi, Fatuma Mbwana, amedai mahakamani katika kesi ya kujihusisha na rushwa inayowakabili askari wenzake wapelelezi wanne wa kituo cha Kawe kwamba, alipokea barua ya kuchunguza nyaraka zinazobishaniwa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Kadhalika, alidai kuwa, baada ya kuyafanyia uchunguzi maelezo ya onyo ya Diana Naivana, yalifanana na sampuli ya maandishi ya askari Joyce Kitta.

Shahidi huyo wa kwanza ambaye pia ni mchunguzi kutoka Maabara ya Uchunguzi wa Kisayansi ya Jeshi la Polisi Makao Makuu, alitoa ushahidi wake mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu, dhidi ya kesi ya kushawishi rushwa ya Sh. milioni 200.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Maghela Ndimbo.

Akiongozwa na Ndimbo, shahidi alidai kuwa Mei 16, 2019 akiwa ofisini kwake, alipokea barua kutoka Takukuru Makao Makuu, jijini Dar es Salaam ikiambatanishwa na nyaraka zilizokuwa zinabishaniwa na ikimwelekeza kuvifanyia uchunguzi.

Alidai kuwa nyaraka hizo ni maelezo ya onyo ya Desemba 17, 2018 ya Naivana na Sampuli ya sahihi zake na sampuli za maandishi ya Kitta.

"Nilifuata maelekezo, nilizifanyia uchunguzi zile nyaraka na baada ya uchunguzi, nilibaini kuwa sampuli ya maandishi ya Kitta inafanana na maelezo ya onyo yanayodaiwa kuwa ya Naivana na kwamba yaliandikwa na mtu mmoja, pia nilibaini sampuli za saini za Naivana hazifanani na zile zilizopo katika maelezo hayo ya onyo," alidai Inspekta Mbwana.

Alidai kuwa baada ya uchunguzi huo aliandaa ripoti na kuiwasilisha Takukuru akieleza uchunguzi wa nyaraka hizo.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni wapelelezi Emmanuel Njegele, Shaban Sillah na Ulimwengu Rashidi.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wote wanakabiliwa na mashtaka manane ikiwamo kujihusisha na vitendo vya rushwa kwamba Desemba 17, 2018 maeneo ya Rainbow Social Club, Kinondoni, wakiwa maofisa wa upelelezi, waliomba rushwa ya Sh. milioni 200 kutoka kwa Naivasha kama kishawishi cha kutokuchukuliwa hatua za kisheria kwa kosa la kukutwa na nyara za serikali.

Kesi hiyo itaendelea kusikilizwa Aprili 15, mwaka huu.

# Wagonjwa corona nchini wafikia 24

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imethibitisha kuwapo kwa kesi mpya nne za maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19) zilizopatika katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Zanzibar.

Kuwapo kwa ongezeko la kesi hizo nne mpya, kumeifanya idadi ya wagonjwa wanaougua virusi hivyo vya homa ya mapafu kufika 24 tangu kuanza kugudulika mgonjwa wa kwanza Machi 17, mwaka huu.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, katika taarifa yake iliyotoa kwa vyombo vya habari jana, alieleza kuwa kati ya wagonjwa hao wane, wawili wanatoka Zanzibar na taarifa zao zimesharipotiwa na Waziri wa Afya wa Zanzibar juzi.

Alisema wagonjwa wapya wawili wa Tanzania Bara ni mwanaume mmoja (41) Mtanzania ambaye ni mfanyabiashara na mkazi wa Mwanza aliingia nchini kutoka Dubai Machi 24, mwaka huu, kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na kuelekea Mwanza Machi 29, mwaka huu na baada ya kuchukuliwa vipimo alikutwa na maambukizi.

Alimtaja mgonjwa mwingine ni mwanamume (35) raia wa Tanzania, mkazi wa Dar es Salaam, ambaye ni mfanyabiashara.

"Wagonjwa wote wapo chini ya uangalizi wa watoa huduma za afya katika vituo maalum vya tiba Dar es Salaam, Zanzibar na Mwanza. Wizara ya Afya inaendelea kuwafuatilia watu wa karibu waliowahi kukutana na watu hao ili kudhibiti maambukizi mapya nchini," alisema Waziri Ummy.

Aidha, alisema Serikali inatoa msisitizo kwa wananchi kuzingatia maelekezo ya wataalamu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona hususan kwa kunawa mikono kwa sababu na maji tiririka.

"Tunawasisitiza wananchi pia kuzingatia maelekezo ya mengine yanayohusu kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima na kukaa umbali usiopungua mita moja kati ya mtu na mtu," alisisitiza Ummy.

Kati ya wagonjwa hao 24 waliogundulika nchini, mmoja alifariki dunia wiki iliyopita na watatu wameshadhibitishwa kupona, hivyo kufanya idadi ya wagonjwa wanaoendelea na matibabu kuwa 20.

HABARI KITAIFA

# Bakwata yashauri waumini corona

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata) mkoani Shinyanga, limewataka waumini wake kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya namna ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Katibu wa Bakwata mkoa wa Shinyanga, Kassimu Malemba, aliyasema hayo mjini Kahama baada ya kufanyika kwa uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Masheikhe wilaya na kupatikana wajumbe saba na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Baraza hilo, Haji Nassor.

Malemba aliwataka waumini wake kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya namna ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona ambao umekuwa tishio duniani.

"Mufti wa Tanzania alitoa maelekezo kwa viongozi wote pia wataalamu wa afya walitupatia elimu dhidi ya kujikinga tumekuwa tukifuata maelekezo hayo na waumini wote na kuwapa angalizo ya kila wakati kunawa mikono, kutoshikana mikono hata majumbani, kuweka ndoo yenye majisafi na sabuni, na wageni wanaokuja wakaribishwe kwa kunawa mikono kwanza," alisema Malembo.

Aidha, Malemba aliwataka viongozi waliochaguliwa waendelee na kusimamia maelekezo yanayotolewa.

Haji Nassor alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Bakwata kwa kupata kura 58, huku kura nne zilimkataa na kura moja kuharibika.

Pia walichaguliwa masheikhe saba wa baraza la wilaya na wajumbe 10, ambapo wajumbe 63 walihudhuria na kupiga kura.

Baada ya kuchaguliwa, Nassor alisema uchaguzi umekwenda vizuri, na kuwashukuru wajumbe waliompigia kura, na kumpongeza Rais John Magufuli na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kuendelea kutoa taarifa kila siku kuhusiana na ugonjwa wa corona.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alisema mwitikio wa kunawa mikono kwa wananchi ni wa wastani, ingawa walikwishatoa maelekezo kwa viongozi wa dini misikitini na kanisani kuhamasisha waumini wao kunawa mikono kwa kuweka vyombo rafiki vya kuweka maji na sabuni ili kujikinga na corona.

**"Mufti wa Tanzania alitoa maelekezo kwa viongozi wote pia wataalamu wa afya walitupatia elimu dhidi ya kujikinga tumekuwa tukifuata maelekezo hayo na waumini wote na kuwapa angalizo ya kila wakati kunawa mikono, kutoshikana mikono hata majumbani, kuweka ndoo yenye majisafi na sabuni, na wageni wanaokuja wakaribishwe kwa kunawa mikono kwanza," alisema Malembo.**

# Polisi sasa wausaka mtandao wa ujangili

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

JESHI la Polisi kwa kushirikiana na askari wa Kikosi cha Idara ya Wanyamapori wilayani Tunduru, Mkoa wa Ruvuma wanausaka mtandao wa majangili wanaoua wanyamapori kwa kutumia mapanga.

Hayo yalibainishwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, na kwamba hatua hiyo imefuatia kukamatwa kwa mtu mmoja akiwa na kilo 10 za nyama ya nyati.

Kamanda Maigwa alisema mtu huyo aliyetambulika kwa jina la Hamisi Nasoro Chamtumavi (24), mkazi wa Kijiji cha Kidodoma alinaswa usiku wa kuamkia Aprili 4, mwaka huu akiwa na vipande 14 vya nyama hiyo, baada ya Polisi kupata taarifa kutoka kwa wasamaria wema.

Alisema katika maelezo ya awali yaliyotolewa na mtuhumiwa huyo, Polisi walibaini kuwapo kwa kundi hilo, na kwamba baadhi yao ni kutoka wilaya ya Kirwa mkoani Lindi.

Kwa mujibu wa maelezo kutoka kwa mtuhumiwa huyo ambaye ni mwenyeji wa kikosi hicho, majangili hao huwinda wanyama hao usiku wa manane wakiwa katika mapori ya hifadhi.

Alisema wakiwa katika misitu hiyo wapo watu ambao hujifunga Tochi kubwa zenye mwanga mkali ambazo huzitumia kuwamulika wanyama ambao hubakia palepale wakiwa wanashangaa mwanga huo.

Alisema baada ya tukio hilo watu wengine ambao huwa wamebeba mapanga makali yaliyo nolewa sana kuwazunguka kwa nyuma na kuanza kuwashambulia kwa kuwakatakata mishipa ya miguu yao ya nyuma na kuwafanya washindwe kukimbia na baadae huendelea kuwakatakata na kuwamaliza.

Akizungumzia tukio hilo, Kaimu Ofisa Wanyama pori wa Wilaya ya Tunduru, LImbega Ally, alithibitisha kuwapo kwa matukio hayo, na kwamba idara yake imejipanga kwa ajili ya mapambano dhidi ya mitandao ya majangili.



Fundi akiendelea na kazi kwenye ghorofa ya sita katika ujenzi unaoendelea wa jengo la kitega uchumi la Jiji la Dodoma, jana, huku akiwa hajachukua tahadhari ya kuvaa mikanda kwa ajili ya kujikinga na ajali, kitendo ambacho ni hatari. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kalemani afafanua mradi wa umeme Rufiji

**Na Idda Mushi, RUFIJI**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewaondoa hofu Watanzania kuwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji wa Julius Nyerere, haujawahi kusimama na hautasimama kabla ya kukamilika.

Amesema wanaohisi hivyo wanapotosha, na kuwa mvua zinazonyesha katika maeneo mbalimbali nchini pia hazijaathiri shughuli zozote za mradi huo uliokwishakamilisha kwa asilimia 20.

Waziri Kalemani alisema hayo baada ya kutembelea kwa mara ya 11 mradi huo na kujionea shughuli mbalimbali zinazoendelea na kueleza kuridhishwa na kasi ya ujenzi, hivyo kumuagiza msimamizi wa ujenzi huo Shirika la Umeme Tanzania ( Tanesco) na mkandarasi anayejenga mradi huo kuhakikisha barabara zote za ndani na nje ya mradi zilizo ndani ya mkataba zinakarabatiwa na kupitika wakati wote.

Akabainisha msisitizo mkubwa kuhakikisha unafanywa kwa makalavati na madaraja ili mizigo iweze kupita bila vikwazo na kwamba eneo la Fuga la kushusha mizigo kwa njia ya treni limekuwa msaada mkubwa kwa kubeba vifaa na mizigo ya mradi huo.

Akatoa wito kwa Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (Tazara),kuendelea kushirikiana na Tanesco pamoja na TECU kusimamia vizuri njia hiyo.

Aidha, aliutaka Wakala wa Barabara nchini (Tanroads), kuanza mara moja ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya kutoka Stesheni ya Fuga hadi eneo la mradi ya kilometa 35.8 ili kusaidia upelekaji wa vifaa vizito eneo la mradi.

Waziri Kalemani aliyetembelea maeneo matano katika mradi huo yakiwamo eneo la njia ya kufua umeme, eneo la kuhifadhi maji yatakayokwenda kwenye mtambo wa kuzalisha umeme, eneo la kusaga kokoto za mradi na mtambo wa kufua umeme utakaokuwa na mashine tisa kwa ajili ya shughuli hiyo, alimtaka mkandarasi kuhakikisha kazi hizo zinakamilika ndani ya muda uliopangwa na kwa wakati.

Alipongeza hatua inayoendelea ya kuajiri wazawa kufanya kazi zinazoweza kufanywa na Watanzania, ambapo kwa sasa kuna Watanzania 3,822 sawa na asilimia 64.8 wanaofanya kazi katika mradi huo unaotarajiwa kukamilika Juni 14, mwaka 2022.

Mratibu wa Mradi huo, Mhandisi Steven Manda, alisema tangu kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo Desemba 2018, kazi zimeendelea kufanywa kulingana na mpango kazi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Tanesco, Dk Tito Mwinuka, aliwaondoa hofu Watanzania kwamba wataalamu wa Kitanzania wanaosimamia kazi za mradi huo wana kiwango cha juu kuwazidi wageni, na wanaamini wataweza kusimamia miradi mingine mikubwa inayotekelezwa nchini.

## Mahakama 33 kukamilishwa ujenzi Desemba

WIZARA ya Katiba na Sheria, imesema majengo ya mahakama za wilaya 33 yaliyopangwa kuanza kujengwa mwezi Juni, mwaka huu yatakamilika Desemba, 2020 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Kwa sasa mahakama ipo katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za awali za ujenzi wa majengo hayo.

Wizara hiyo ilitoa majibu hayo bungeni jana katika swali la Mbunge wa Mbogwe (CCM), Augustino Masele (pichani), ambaye alisema wananchi wa wilaya ya Mbogwe wanakabiliwa na kero ya kupata huduma za kimahakama kwa kuzifuata wilaya za jirani.

"Je, serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama ya Wilaya Mbogwe?"

Wizara hiyo ilisema, uhaba wa majengo ni moja ya kero zinazoikabili Mahakama ya Tanzania.

"Mahitaji ya majengo ya kuendeshea shughuli za mahakama hapa nchini ni makubwa, kwa msingi huo, imejiwekea utaratibu wa kujenga majengo haya kwa awamu kulingana na mpango wa ujenzi na upatikanaji wa fedha," ilisema.

Ilieleza kuwa ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya Mbogwe ni miongoni mwa majengo ya Mahakama za Wilaya 33 yaliyopangwa kuanza kujengwa mwezi Juni na kukamilika Desemba, 2020 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Ilisema mchakato wa ujenzi huo upo hatua za mwisho na utaanza kwa muda kama ilivyo katika mpango wa mahakama.

"Tayari Mshauri Elekezi amefanya mapitio ya michoro na ujenzi unatarajiwa kuanza kama ilivyopangwa,"Ilisema.






# Wataalamu afya zaidi ya 8,000 waajiriwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**



SERIKALI imewaajiri wataalamu wa kada mbalimbali za sekta ya afya nchini 8,994 ndani ya miaka mitatu.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ilipokuwa ikitoa majibu katika swali la Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi.

Shangazi katika swali lake aliuliza sekta ya afya nchini inakabiliwa na uhaba wa watumishi na kuhoji mpango wa haraka wa kuziba pengo hilo.

Majibu yaliyotolewa na Ofisi hiyo, yalisema kuanzia Mei, 2017 hadi Julai, 2019 jumla ya watumishi 8,994 wameajiriwa na kupangwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Pia ilisema serikali imeendelea kuajiri wataalamu wa kada mbalimbali na imetoa kibali cha kuajiri madaktari 610 ambao watapangwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwamo Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Viti maalumu (Chadema), Rose Kamili (pichani), alihoji lini serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya watoto, wanawake, wanaume na nyumba za watumishi wa Zahanati ya Bassotu.

Katika majibu yake ofisi hiyo ilisema kutokana na mwongozo unaosimamamia utoaji wa huduma za afya, zahanati hazina wodi ya watoto, wanawake na wanaume.

Hata hivyo, ilisema kutokana na umbali uliopo kati ya zahanati hiyo na hospitali wa kilometa 55, serikali itafanya tathmini ili kuboresha miundombinu iliyopo na kuifanya zahanati hiyo kuwa na hadhi ya kituo cha afya.

# Serikali haina mpango kuzuia wakulima kuuza

SERIKALI imesema haina mpango wowote wa kuwazuia wakulima kushirikiana na sekta binafsi kuuza mazao yao nje ya nchi.

Majibu hayo yalitolewa bungeni jana na Wizara ya Kilimo katika swali la Mbunge wa Viti Maalumu (Chadema), Anatropia Theonest (pichani).

Mbunge huyo alihoji kwanini serikali inawazuia wakulima wanaoshirikiana na sekta binafsi, kuuza mazao yao ya biashara hasa kahawa, mahindi na korosho nje ya nchi kwa lengo la kujipatia faida.

"Je, ni kwa nini serikali isiongeze ruzuku ya Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) ili inunue mazao hayo pindi bei zinaposhuka," alihoji.

Katika majibu yaliyotolewa na wizara hiyo, ilisema serikali inaendelea kutoa vibali kwa wakulima na wafanyabiashara mbalimbali wanaosafirisha mazao ya kilimo hususan mahindi nje ya nchi au kuingiza ndani ya nchi.



"Vibali vitolewavyo na Wizara ya Kilimo ni vya kuingiza mazao ya kilimo nchini au kusafirisha mazao ya kilimo nje ya nchi yaani 'Import and Export Permits' pamoja na cheti cha Usafi wa Mazao yanayosafirishwa yaani 'Phytosanitary Certificate'," ilisema.

Hata hivyo, ilisema serikali haina mpango wa aina yoyote wa kuwazuia wakulima kushirikiana na sekta binafsi kuuza mazao yao nje ya nchi na inaendelea kuhimiza wakulima waendelee kujiunga katika vikundi ili kuwa na nguvu ya pamoja katika kuuza mazao yao.

Ilibainisha kuwa wanatakiwa kuongezea thamani mazao yao ili kujiongezea kipato zaidi.

Ilisema majukumu ya NFRA ni kununua na kuweka akiba ya chakula cha taifa, kudhibiti mfumuko wa bei wa vyakula vya nafaka kwa kuingiza nafaka sokoni ya bei nafuu pamoja na kutoa chakula cha msaada kwa maelekezo ya mfuko wa maafa wa taifa pindi taifa linapopatwa na majanga ya maafa.

"Kwa kuzingatia majukumu hayo, Wakala umekuwa kimbilio la wakulima kwa kuwa umekuwa ukinunua nafaka kwa bei nzuri katika masoko inayozingatia gharama za uzalishaji za mkulima," ilisema.

Vile vile, ilisema serikali hutenga ruzuku kwaajili ya ununuzi wa nafaka kila mwaka.

"Kwa kuzingatia majukumu ya Wakala, ununuzi huu hauhusishi mazao yasiyo ya nafaka. Pia, Wakala hutumia vyanzo vingine vya mapato kununua nafaka zikiwamo mauzo ya nafaka na mikopo kutoka taasisi za fedha, mikopo ambayo hurejeshwa kwa kutumia fedha za mauzo ya nafaka," ilifafanua.

## Gambo aonya wanasiasa wanaojipitisha sokoni

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amewaonya wanasiasa wanaojipenyeza kwenye Soko la Samunge lililopo eneo la NMC katika Halmashauri ya jiji lililoungua Machi 28, mwaka huu na kuwataka kukaa mbali na wafanyabiashara.

Akizugumza mwishoni mwa wiki kwenye hadhara alipotembelea soko hilo, Gambo alisema serikali itahakikisha kila mfanyabiashara aliyekuwapo kwenye soko hilo anapata eneo la kufanyabiashara bila kusumbuliwa.

"Lakini nawaonya wale wote wanaojipenyeza hapa kwa kudhani ndio sehemu ya kupiga siasa, nawataka wakae mbali vinginevyo hatua kali za kisheria nitawachukulia,"alisema.

Alisema sasa sio muda muafaka wa kupiga siasa, bali ni utekelezaji wa kuhakikisha miundombinu ya wafanyabiashara hao inarudishwa katika hali yake ili maisha ya watu yaendelee.

Aliwatoa hofu wafanyabiashara hao na kuahidi serikali kuwapo eneo hilo kwa siku nzima ili kila aliyeunguliwa anapata eneo lake na aanze ujenzi mara moja ikiwamo kufanyabiashara kwa ajili ya kujitafutia kipato cha familia zao.

Kaimu Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Arusha, Joseph Massawe, aliyeambatana na Gambo, alitaka serikali kuhakikisha inamaliza kuweka miundombinu kwa haraka, ili wafanyabiashara hao waanze kazi mara moja.

Kamanda wa Kikosi cha Zimamoto, Yusuph Semtana, alisema miundombinu hiyo ya barabara itaanzia kusini na kaskazini na upande wa Mashariki na Magharibi kutakuwa na barabara ambayo itasaidia kupita magari yao kwa ajili ya kuzima moto bila shida kama ilivyokua awali.

"Moto huo uliteketeza bidhaa na mabanda sababu hakukuwa na barabara za kupita kila upande, lakini sasa wataweka miundombinu hiyo vizuri," alisema.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Koka Moita, aliwatoa hofu wafanyabiashara hao na kuwaambia jeshi hilo litashughulika na yeyote atakayebainika kuleta uvunjifu wa amani katika eneo hilo.

Soko la Samunge liliungua kwa moto Machi 28, mwaka huu na kusababisha kifo cha mfanyabiashara mmoja James Temba (57), mkazi wa Moshono, wilayani Arusha, kutokana na mshtuko baada ya kuona vibanda vyake vinateketea kwa moto, huku bidhaa na vibanda zaidi ya 3000 kuungua.

**"Moto huo uliteketeza bidhaa na mabanda sababu hakukuwa na barabara za kupita kila upande, lakini sasa wataweka miundombinu hiyo vizuri," alisema.**

# Soko laongeza vituo vya kunawa mikono

**Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA**

SOKO kuu la mkoani Manyara, limeanza kupunguza msongamano katika vituo vya kunawa mikono kwa kuongeza vituo vingine, kwaajili ya kuwakinga wafanyabiashara na wateja wanaofika sokoni hapo na maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Akizungumza na Nipashe jana, katika soko hilo mkoani Manyara, mfanyabiashara wa soko hilo, Julieth Philipo, alisema wameongeza vituo vya kunawa mikono ili kuondoa msongamano.

"Kwa sasa hali ya msongamano haitakiwi kabisa, sababu ni hatari kwa afya za watu kutokana na tishio la ugonjwa corona, hivyo vyema tukazingatia hili na kuchukua tahadhari mapema," alisema Julieth.

Alisema pamoja na kuongeza vituo hivyo pia wanakumbushana kuzingatia unawaji wa mikono hata kwenye familia zao ili kujiweka salama.

Naye mfanyabiashara mwingine, Gasper Marishamu, alisema uongozi wa soko hilo umefikiria jambo jema kwa kuongeza vituo vya kunawa mikono, kwa kuwa hali ilivyokua awali ilihatarisha usalama wao kutokana na msongamano.

"Napongeza juhudi za viongozi kuongeza vituo hivi, hali hii inalenga kuwakinga dhidi ya ugonjwa wa corona kuliko ilivyokuwa awali tulikua tunasongamana na kugombea kunawa katika kituo kimoja," alisema.

Mwenyekiti wa soko hilo, Mwazamu Ramadhani, alisema pia anaendelea na mikakati ya kampeni ya kuhamasisha watu kunawa mikono kwa hiari badala ya kusubiri kulazimishwa.




Wakazi wa Kijiji cha Orbomba wilayani Longido, mkoani Arusha, wakiangalia gari aina ya Toyota Noah, lenye namba ya usajili T742DGF, lililoanguka katika barabara ya Namanga-Arusha, juzi jioni, baada ya kuchomoka gurudumu la nyuma na kusababisha vifo vya watu wanne akiwemo Inspekta wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, Enock Wange. **PICHA: ZANURA MOLLEL**

# Shirika latoa msaada wa chakula vituo vya watoto

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

SHIRIKA la Convoy of Hope International Tanzania, limetoa msaada wa chakula katika vituo vya watoto yatima mkoani Arusha, ili kuvinusuru na janga la njaa, kutokana na katazo la wasamaria wema na wafadhili kunyimwa kutembelea vituo hivyo, kutoa misaada kama ilivyokuwa kabla ya ugonjwa wa Covid-19.

Shirika hilo limetoa msaada wa vyakula kwa vituo 20 vya watoto yatima vyenye watoto 530.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Godfrey Mjema, alisema kuwa chakula walichotoa ni akiba iliyokuwa ya watoto waliokuwa shuleni ambao kwa sasa wamefunga shule kwa ajili ya tishio la ugonjwa huo.

Mjema alisema msaada huo ni kuisaidia serikali kwa kuwa haiwezi kufanya kila kitu na kuhakikisha afya za watoto hao haziyumbi katika kipidi hiki cha tishio la ugonjwa huo.

Alisema walipokea maombi ya msaada kutoka kwa wawakilishi wa walezi wa watoto yatima ambao baadhi yao wanalea watoto wanaoishi na virus vya Ukimwi.

Kwa upande wake, Josephat Mmanyi, ambaye ni Mwenyekiti wa mtandao wa wamiliki na walezi wa watoto yatima jijini Arusha, alisema ugonjwa wa Covid-19, umeleta shida kwa watoto yatima kwa kuwa wafadhili wa ndani na nje ya nchi hawawezi kuingia katika vituo hivyo kuendelea kutoa msaada.

Mmanyi aliomba wadau wengine wenye mapenzi mema kujitokeza kusaidia watoto yatima kwa kuwa wote wako kwenye vituo baada ya wale waliokuwa vyuoni, shule za msingi, sekondari kurudishwa nyumbani ama kwenye makazi yao.

Alisema akiba waliyokuwa nayo imeisha na sasa wanapitia katika wakati mgumu na kuwataka watu wenye mapenzi mema na mashirika kujitokeza kuwasaidia.

Mmanyi alishukuru kwa msaada huo ambao alisema utasaidia vituo vilivyokuwa katika hali mbaya zaidi.





## Wajasiriamali Mwanga wapewa siri kufanikiwa

**Na Godfrey Mushi, MWANGA**

SERIKALI imesisitiza ili wajasiriamali waweze kushindana vyema katika soko huria, hawanabudi kuwa wabunifu na kutafakari huduma wanazotoa, na namna ya kuziboresha na kuzitofautisha na nyingine.

Mkakati huo umo katika taarifa ya halmashauri hiyo iliyowekwa katika tovuti yake na kuthibitishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Zefrin Lubuva.

Mkakati huo unaelekeza kuwapo kwa mabadiliko na ubunifu kwa wajasiriamali hao, hasa wakitambua kuwa dunia inabadilika kila siku.

"Leo tuna soko huria na mambo mengi ambayo awali hayakuwapo. Katika huduma za kuwezesha wajasiriamali tumejipanga kuhamasisha /kuhimiza jamii kuwa na ari ya kujituma kutumia fursa mbalimbali zilizopo katika maeneo yao ili kujiletea maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

"Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, itatoa mafunzo ya ujasiriamali kwa watu binafsi na vikundi vinavyojihusisha na shughuli za ujasiriamali, kutoa huduma ya usajili wa vikundi vya ujasiriamali vya vijana na wanawake na kuhamasisha jamii kushiriki kwenye shughuli za maendeleo."

Aidha, mkakati huo unalenga pia kutoa huduma ya mikopo kwa akina mama na vijana, kushauri na kutoa elimu juu ya miradi inayoendeshwa na fedha za mikopo zilizotolewa kwa vijana na wanawake.

Wakati Wilaya ya Mwanga ikija na mkakati huo, wajasiriamali wengi nchini wanakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa elimu ya kawaida na ile ya biashara, hali ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa kushindwa kukua kwa biashara zao, hivyo kuchangia umaskini kwa wanajamii.

Mtaalamu wa masuala ya ujasiriamali, Abdon Israel, alipotafutwa kuzungumzia mkakati huo iwapo utafanikiwa, alisema: "Haya yote yasingejulikana kama kusingekuwa na tafiti mbalimbali ambazo zimekwisha fanyika.

"Tafiti husaidia sana katika kuibua vitu vilivyojificha, vyote vizuri ama vibaya, kwa lengo la kuvipatia ufumbuzi wa kisera na kisheria kwa manufaa ya Watanzania wote."

**"Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, itatoa mafunzo ya ujasiriamali kwa watu binafsi na vikundi vinavyojihusisha na shughuli za ujasiriamali, kutoa huduma ya usajili wa vikundi vya ujasiriamali vya vijana na wanawake na kuhamasisha jamii kushiriki kwenye shughuli za maendeleo."**

# Manispaa yasikia kilio cha wafanyabiashara

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Moshi, imesikia kilio cha muda mrefu cha wafanyabiashara wa maduka katika kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani na yanayofanya safari zake ndani ya mkoa wa Kilimanjaro, baada ya kuongeza muda wa mkataba wa umiliki.

Kutokana na mabadiliko hayo, sasa mkataba utakuwa ni wa kutoka mwaka mmoja hadi mitatu.

Jana, Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, alisema kuongezwa kwa muda wa mkataba wa umiliki wa maduka hayo ni neema kwa wafanyabiashara hao.

"Tumepitisha jambo hili kwamba kuanzia sasa wafanyabiashara hao wa maduka watasaini mkataba wa miaka mitatu, badala ya mwaka mmoja kama ilivyokuwa awali. Nadhani hiyo kwao ni neema ambayo walikuwa wakiisubiri kwa muda mrefu," alisema Mboya.

Aidha, Meya huyo alisisitiza katika suala la upangaji katika maduka hayo, wao walitangaza zabuni na wafanyabiashara walioomba zaidi ya asilimia 92 walishinda zabuni hiyo kulingana na bei ya soko.

Kwa mujibu wa Meya huyo, Baraza la Madiwani wa Manispaa hiyo, pia liliridhia bei mpya ya kodi ya pango kulingana na bei ya soko, ikizingatia mapendekezo ya wafanyabiashara.

Desemba mwaka jana, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ilitangaza maombi ya zabuni kwa njia ya ushindani ya kupangisha vyumba vya biashara vilivyopo jengo la stendi kuu ya mabasi.

Katika tangazo hilo lililosainiwa na Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Michael Mwandezi, Desemba 3, 2019, lilieleza kuwa muda wa mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ilikuwa ni Desemba 17, 2019, saa 4:00 asubuhi.

Katika tangazo hilo, halmashauri hiyo ilisisitiza haipokei maombi yaliyochelewa au ya ki-elektroniki.



Mkazi wa Kijiji cha Rundugai, wilayani ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Dotinata Francis akichota maji kwa ajili ya kunywa na kupikia katika chemchem ya Musa Toroka, juzi. Kijiji hicho kinakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maji ya bomba. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wanaoendeleza mila za ukatili wamchefua DC

**Na Mary Mosha, ROMBO**

BAADHI ya koo zinazoendelea kuongeza makali ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake katika suala la umiliki wa ardhi na usimamizi wa mali, 'zimemchefua' Mkuu wa Wilaya Rombo, Agness Hokororo.

Akieleza jana namna anavyochukizwa na hali hiyo, Hokororo alisema, baadhi ya koo wilayani humo bado zinaumiza wanawake na hasa wajane kutokana na kuzalisha migogoro inayotokana na mfumo dume.

"Kutokana na hali hiyo, nawaagiza viongozi wa koo katika Wilaya ya Rombo, ni vyema wakaachana na mfumo dume hasa katika ugawaji wa ardhi, kwa sababu ipo kasumba inayotesa baadhi ya familia ambazo hazikujaliwa mtoto wa kiume au wametangulia mbele za haki, basi ukoo unachukua hilo eneo hata kama kuna watoto wa kike.

"Wakati mwingine unakuta kama mwanamke ameolewa na kuzaa watoto wa kike tu, hunyanyaswa na kuonewa, hata kama baba mwenye familia alijaliwa hekima na akaamua kugawa eneo lake kwa watoto wa kike. Sasa anapofariki baadhi ya ndugu kwenye ukoo wanawanyang'anya maeneo hayo, jambo hilo halikubaliki kisheria na ni uonevu. Sitakubaliana na jambo hilo."

Mkuu huyo wa Wilaya, ameonya iwapo baadhi ya viongozi au ndugu wanaoendelea kukumbatia uonevu huo hawatabadilika au kubadili mtazamo huo, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Aidha, Hokororo alizitaka familia zenye migogoro ya aina hiyo kuachana na mfumo huo, kwa kuwa unaumiza wanyonge.


Alisema: "Kibaya zaidi unakuta hao wanaofanya hayo, hawawapi nafasi wanawake wajane wakati wa usikilizwaji wa mashauri ya kifamilia au wanapotoa uamuzi hasa katika kumiliki ardhi. Punguzeni mfumo dume ili mtusaidie kumaliza migogoro ya ardhi kwenye jamii yetu."

Alisema baadhi ya koo wilayani humo, zimekuwa zikizalisha migogoro ya ardhi kutokana na mfumo dume pamoja na kuwanyima haki wajane.

Wakati huo huo, Hokororo aliyataka mabaraza ya ardhi katika ngazi za vijiji hadi wilaya kutekeleza wajibu wao katika kusuluhisha migogoro ya ardhi ili kupunguza mashauri hayo mahakamani.

Ofisa Ardhi Mteule wa Wilaya hiyo, Arbogast Mhumba, alisema licha ya kuwapo kwa mfumo dume unaoendelea kusababisha ongezeko la migogoro ya ardhi katika

Nipashe
# TESA
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Jumanne Aprili 7, 2020



Ukurasa 18

**Dk. John Snow: Daktari aliyemaliza kipindupindu**




Ukurasa 19

Corona ipo, si wakati wa kuzembea wala kupuuza



Ukurasa 17

## Wagonjwa 253 694 wapona corona duniani



# Mko wapi wanawake waongoza ndege Tanzania?

Ukurasa 16

ELIMU YA KIPOLISI

# Polisi: Malezi bora suluhu ya uhalifu

TANGU kuumbwa dunia, familia imeonekana kuwa ni nguzo muhimu ya jamii, kuanzia maendeleo, ustawi na ukuaji wa taasisi nyingine za jamii na taifa kwa ujumla, yote hutegemea sana uimara ambao hutokana na uwepo wa familia yenye malezi bora.

Kwa tafsiri ya rahisi ya familia inaweza kuwa ni baba, mama na mtoto au watoto ambapo mtoto huwategemea baba na mama ambao ni wazazi katika maisha yake ya kila siku kuhusiana na malezi na makuzi yake kuanzia utoto.

Kutetereka kwa malezi katika ngazi ya familia mara nyingi huleta upungufu katika maadili na uadilifu ambayo huwa tabia na kuhamia katika taasisi nyingine ndani ya jamii na kupelekea kuharibika kwa jamii nzima. Makuzi ya mwanadamu hukutana na mazingira mbalimbali katika maisha yake ambayo humwezesha kujifunza mambo mengi ndani ya jamii.

Mafunzo hayo yanaweza kuwa ya kujifunza au kuiga namna watu wengine ndani ya jamii wanavyofanya au kwa kupatiwa mafunzo mema na yasiyokuwa mema. Ni dhahiri kuwa, suala la malezi ya familia linatakiwa kuangaliwa kuanzia ngazi ya familia ambacho ndicho kitalu cha kwanza cha makuzi ili taifa lisijekuwa na watu wasiokuwa wema.

Inafahamika wazi kuwa, kulingana na shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii, siku hizi wazazi na walezi wengi hutumia muda wao mwingi nje ya familia kwa ajili ya kutafuta mali na maisha kwa ajili ya kujiongezea kipato.

Mfano wafanyakazi hutumia muda mwingi kwa waajiri wao na wakati mwingine hutelekeza familia zao kwa lengo la kumridhisha mwajiri, jambo ambalo hupelekea kushindwa kutoa malezi bora kwa kiwango kinachotakiwa kwa watoto na kusababisha watoto kuangukia katika malezi ya makundi ya watu wasiofaa ndani ya jamii.

Wakati mwingine wazazi na walezi wanajisahau na kufikiri kuwa uhusiano walionao na wafanyakazi wenzao ni muhimu sana kuliko uhusiano na watoto wao, ndugu zao, jambo ambalo hupelelekea kutokuwa na uangalizi wa watoto wao, matokeo yake kutokuwa na malezi bora katika familia.

Tafsiri yake ni kwamba wana sahau uwekezaji wa malezi bora kwa familia ndio msingi wa jamii bora, tukiwekeza katika familia zetu kwa kuimarisha uhusiano na uangalizi tutaweza kukabiliana kuchipuka kero ndani ya jamii ikiwamo suala la uhalifu.

Kwa kutambua hilo, Machi 3, mwaka huu, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, anazungumza na wananchi wa mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro na kuwataka wazazi na walezi kuendelea kuimarisha malezi ya familia kwa kuwajenga watoto wao katika maadili yanayofaa jambo ambalo litasaidia kuwaepusha kwenye vitendo vya uhalifu na kuwa kero ndani ya jamii.

"Ni aibu kuwa na mtoto mwizi na ni aibu pia kuwa na mtoto anayefanya vitendo vya ukatili" anasema IGP Sirro.

Kutenda uhalifu kwa tafsiri na mtazamo wa kidini ni kutenda dhambi jambo ambalo viongozi wa dini zote huwakemea waumini wao kutotenda dhambi na kuwataka kufanya matendo mema. Huenda mbali zaidi kwa kuwafundisha waumini wao kuwa kujiepusha kutenda dhambi humfanya mtu kupata thawabu na baraka kutoka kwa Mungu.

Pia, anasema kutenda dhambi kwa tafsiri ya mtazamo wa kiusalama, ni kutenda uhalifu jambo ambalo vyombo vya usalama likiwamo Jeshi la Polisi ambalo mara kwa mara limekuwa likikemea vitendo hivyo ndani jamii na kuwakamata na kuwafikisha mahakamani wale wanao kiuka sheria.

Hivyo, malezi bora ya watoto yanatakiwa kuzingatiwa na kupewa kipaumbele cha pekee kwa kuwa ndio mwanzo wa jamii na taifa kwa ujumla. Wazazi na walezi wakizingatia na kuwekeza hazina ya malezi bora katika familia kwa kuimarisha uangalizi watoto tutapunguza dhambi nyingi na kero ya uhalifu ndani ya jamii.

***Ofisi ya Uhusiano, Makao Makuu ya Polisi, Dodoma.***



Kamishna wa Oparesheni na Mfunzo, Liberatus Sabas (kulia), alipokutana na Kikosi Maalum cha Kupambana na Uhalifu mkoani Mtwara, katika kuimarisha ulinzi na usalama mpakani mwa Tanzania na Msumbuji. Uhalifu ni matokeo ya kukosekana malezi bora kwenye familia. **PICHA NA JESHI LA POLISI**

JIELIMISHE

# Jinsi ya kula mlo bora licha ya kipato kidogo




Senene pamoja nzige ni chakula rahisi kwa wakazi wa vijijini hasa sehemu zinapopatikana kwa wingi . Protini zake ni za kutosha kukupa mlo kamili. **PICHA: MTANDAO.**

KATIKA taifa ambalo kuna baadhi ya watu wana ardhi, rasilimali na fedha kuna wengine hawana kitu, hivyo njaa itaendelea kuwapo.

Na vipindi vya njaa vitaendelea kutokea iwapo vita, milipuko ya magonjwa, uchafuzi wa mazingira uliokithiri, ukosefu wa utunzaji bora wa ardhi, na sera zinazowalazimisha watu kuhama vitaendelea kuibuka. Vyanzo hivyo vya njaa ni lazima vishughulikiwe ili kuhakikisha kila mtu anapata chakula cha kutosha.

Lakini familia au jamii moja inaweza kula vizuri hata kama wana rasilimali kidogo. Na kwa kula vizuri, wanaweza kupata nguvu za kuzalisha mali na kusimama imara kupigania haki zao za kibinadamu na kuboresha maisha yao.

**MBINU**

Mbinu za kupata mlo wa kutosha na wenye lishe ni nyingi lakini za msingi ni kununua vyakula vya kawaida visivyo ghali kama vile maharagwe, na nafaka. Vyakula hivi vina virutubishi zaidi na gharama yake ni nafuu kuliko vyakula ambavyo vimetengenezewa viwandani kama vile mikate myeupe, biskuti, na supu za kwenye makopo.

Kama unaishi vijijini, chuma au winda vyakula vya asili kama vile uyoga unaoliwa, mboga za majani za porini na matunda, wanyama wadogo au wadudu kama senene na kumbikumbi. Vyakula hivi mara nyingi huwa na virutubishi vingi na fuga kuku kwa ajili ya mayai na nyama. Baadhi ya watu hujenga mabwawa madogo ya kufugia samaki kwa ajili ya kula.

Panda chakula chako mwenyewe kwenye vyombo au bustanini.

Nunua chakula kila mara kwa wingi. Kununua chakula kidogo kidogo kwa rejareja huwa ghali zaidi kuliko kununua chakula kwa wingi kwa bei ya jumla, chakula ambacho unaweza kutumia kwa muda mrefu zaidi.

Kama huwezi kumudu chakula kingi kwa wakati mmoja, unaweza kushirikiana na jirani yako au mwanafamilia, na baadaye kugawana gharama.

Kumbuka watoto wachanga na wadogo wanahitaji maziwa ya mama, siyo maziwa au vyakula vya viwandani. Maziwa ya mama ndiyo lishe bora zaidi kwao na hayana gharama.

Maziwa ya kawaida ya wanyama, au vyakula ambavyo vimepikwa vizuri na kupondwa pondwa vina gharama nafuu zaidi na pia huleta afya zaidi kwa watoto kuliko vyakula vya watoto wachanga vilivyofungashwa viwandani.

Usitupe mchuzi wa maharagwe, nyama au mbogamboga ambao hutokea wakati wa kupika. Mchuzi huu umesheheni virutubishi na unaweza kuzuia anemia.

Kunywa au tumia mchuzi huo kupika nafaka au vyakula vingine. Au pika na maji kidogo na kufunika chombo ili virutubishi vibaki ndani.

Tumia fedha uliyonayo kwa ajili ya chakula. Pombe, tumbaku, na pombe au soda hugharimu fedha nyingi na havina tija kilishe.

**Mtandao**

ELIMU

**NA MWALIMU REUBENI LUMBAGALA**

# Mtoto anaposukumwa kwenda shule, inazaa gharama kila kona



Ni vyema zaidi polisi watumike kuwafundisha wanafunzi masomo kama usalama barabarani lakini si kuwalazimisha wazazi kuwapeleka watoto shule. **PICHA: MTANDAO**

KARIBU msomaji wa makala haya katika muendelezo wa mada hii muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya elimu nchini.

Kwenye matoleo yaliyotangulia tulichapisha uchambuzi kuhusu umuhimu wa elimu kwa karne ya 21 tuliyomo ambayo zama hizi zimejaa kasi kubwa ya maendeleo katika nyanja zote hasa sayansi na teknolojia.

Hivyo kusababisha mahitaji makubwa ya rasilimali watu wenye maarifa, ujuzi na stadi za kutosha ili kuendana na kasi ya maendeleo.

Tuliona namna ambavyo baadhi ya wazazi na walezi walivyo kikwazo kikubwa cha mafanikio ya elimu kwa watoto wao na taifa kwa ujumla kwa kuwazuia wanafunzi waliochaguliwa kwenye shule mbalimbali kujiunga na elimu ya sekondari, tatizo ambalo lipo katika maeneo mengi nchini.

Katika kupambana na tatizo hili, serikali imeamua kutumia viongozi na vyombo vya ulinzi na usalama kukabiliana na wazazi na walezi wanaorudisha nyuma juhudi kubwa zinazofanywa na wadau mbalimbali wakiwamo sekta ya umma, binafsi na washirika wengine wa maendeleo katika kuhakikisha sekta ya elimu inapiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Elimu na kusoma kwa ujumla ni suala la kimaendeleo ambalo kila mtu anapaswa kutoa ushirikiano chanya kufanikisha mafanikio ya elimu.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea, hivyo Watanzania tunapaswa kushirikiana kwa pamoja kuipa elimu kipaumbele cha kwanza, kwani hata nchi zilizoendelea zilitilia mkazo wa kipekee elimu, hali iliyopelekea kufikia mafanikio na maendeleo makubwa waliyonayo sasa.

Ndicho chanzo cha kuwa na uwezo wa kutoa mikopo na misaada kwa nchi zinzoendelea kama Tanzania.

Tukiangalia madhara ya mtoto kusoma kwa shinikizo la polisi, yapo mengi lakini mosi ni wanafunzi kukosa hamasa ya kusoma kwa bidii.

Wanafunzi wanaozuiliwa na wazazi na walezi kusoma ni wale ambao wamesoma kwa bidii na hatimaye kufaulu mitihani yao ya taifa. Wengine walikiuka maagizo ya wazazi wao waliowaagiza kujifelisha kwenye mitihani ili wasiendelee na elimu ya sekondari.

Hawa wanapofaulu, wazazi huwa vikwazo na kuwazuia wasijiunge na elimu ya sekondari.

Polisi wanapoingilia kati na hatimaye mtoto huyo kuendelea na masomo, morali ya mtoto kusoma inakuwa imeshuka kwa kiwango kikubwa.

Pili, wazazi na walezi kuwa wagumu kuwapatia watoto wao mahitaji ya msingi ya shule.

> Mtoto ni mtoto akikosa uangalizi na ufuatiliaji wa karibu kutoka kwa wazazi wake au walezi ni rahisi kufeli masomo.

Upo mgomo baridi kwa baadhi ya wazazi na walezi kutumia kisingizio cha umaskini kuwakataza watoto wao kusoma shule ili hali kwa sehemu kubwa gharama za elimu zinagharamiwa na serikali kupitia kodi za wananchi.

Kutokana na wazazi kushurutishwa na serikali kuwapeleka watoto wao shule, wengine wamekuwa hawatoi mahitaji muhimu ya shule kwa watoto wao.

Mathalani, sare, madaftari, mkoba wa shule, viatu, chakula na hata kuwalipia gharama za kukaa bweni.

Yote haya husababisha kushindwa kupata mahitaji haya kumesababisha watoto wao kukwama kusoma vizuri na kuishia kuanguka kwenye mtihani wa taifa kidato cha nne.

Tatu, wazazi kutofuatilia maendeleo ya kitaaluma ya watoto wao. Wazazi wana mchango mkubwa kufanikisha maendeleo ya kitaaluma ya watoto wao kutokana na nafasi kubwa waliyonayo kama wazazi kwa watoto.

Wazazi na walezi ambao hawataki watoto wao wasome, hawatoi ushirikiano katika masuala ambayo yanaongeza thamani kitaaluma kwa watoto wao.

Kwa mfano, kushindwa kukagua kile ambacho mwanaye anajifunza shuleni, kutohudhuria vikao vya wazazi vya kujadili maendeleo ya taaluma ya mwanaye, kutompa hamasa mwanaye juu ya kusoma kwa bidii nk.

Mtoto ni mtoto akikosa uangalizi na ufuatiliaji wa karibu kutoka kwa wazazi wake au walezi ni rahisi kufeli masomo.

Nne, kushindwa kutekelezwa kikamilifu mkakati wa kutokomeza utoro.

Wazazi wana sehemu kubwa ya kupambana na tatizo la utoro ambalo ni kikwazo cha kufikia mafanikio ya kitaaluma kwa baadhi ya shule, wilaya na hata mikoa nchini.

Kama nilivyoeleza awali kuwa wazazi wanaoshurutishwa na serikali kupitia polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, huwa wagumu kutoa ushirikiano katika mikakati ya maendeleo ya elimu. Uwe utoro wa rejareja au utoro sugu unaathiri mafanikio ya kitaaluma ya mwanafunzi.

Kwahiyo, wazazi waliopeleka watoto shule kwa msukumo na shinikizo la polisi, wanashindwa kufuatilia mahudhurio ya mtoto shuleni, wakati mwingine kumkataza mtoto kuhudhuria shule kikamilifu na kuwapa majukumu mengine kama kulima, kuchunga mifugo na kuuza bidhaa mbalimbali mitaani au sokoni.

Jambo jingine ni kulisababishia taifa gharama za rasilimali kuanzia fedha na muda kufuatilia watoto ambao hawajaripoti shule.

Kodi za wananchi zinapaswa kutumika katika masuala makubwa ya kimaendeleo, lakini sasa rasilimali za nchi zinatumika kufanya msako kuwadhibiti wazazi wanaozuia watoto wao wasisome shule.

Wazazi tubadilike ili fedha hizo zitumike katika shughuli nyingine za maendeleo ya elimu kama ujenzi wa madarasa, mabweni, vyoo, ununuzi wa vitabu na utengenezaji wa madawati. Wazazi na walezi tuwawekee mazingira bora watoto wasome ili wafanikiwe maishani.

Mzazi, tafakari chukua hatua.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali Dodoma.***


***Maoni: 0765- 409249.***

SAYANSI

NA BEATRICE PHILEMON

# Mko wapi wanawake waongoza ndege Tanzania?

• Waliopo 23 pekee, kikwazo kusoma sayansi...




Ndege katika uwanja wa JNIA, mawasiliano ya kupaa na kutua kwa ndege hizo hufanywa na traffic controller. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

HISTORIA inaonyesha kuwa kazi za kuendesha mitambo, ubunifu na zile zinazoonekana kuwa zinatumia zaidi utaalamu na teknolojia zilifanywa na hata sasa ni jukumu la wanaume.

Utaratibu huo wa maisha uliwaweka wanaume kwenye kazi za viwandani, kutumia mitambo, kuwa wataalamu wa kuendesha na kutumia vifaa vya teknolojia, mfano X-ray hospitalini, wengine kuendesha meli baharini yote hayo yakihitaji uwezo mkubwa kielimu, ujuzi wa sayansi na kuwa na uwezo mkubwa kiuchumi mambo yaliyowaacha wanawake nyuma na kwa miongo mingi kuwa wategemezi wa wanaume.

Lakini, chanzo cha mambo hayo pamoja na unyanyasaji wa kijinsia, wanawake wengi wamekosa fursa za kujiendeleza kwa sababu ya kuachwa nyuma kielimu. Hawakupewa nafasi ya kusoma na kusomeshwa kama walivyo wanaume.

Hata pale waliposoma waliishi kujifunza masuala ya sanaa (arts) ambayo nayo hayana msukumo mkubwa kwenye anga za sayansi na teknolojia, ndiyo maana wanawake wanahimizwa kujitokeza na kusoma masomo ya sayansi ikiwamo fani ya uongozaji ndege (air traffic control) ili kuongeza nafasi za wanawake kwenye masuala ya utaalamu wa vyombo vya anga.

Kwa hiyo, kuwa mwanaanga si kazi ya wanaume pekee, hata wanawake wanaweza lakini ni kupitia masomo ya sayansi hasa hesabu na fizikia ili kuifinikisha Tanzania kupata watalaamu wengi wa kike wa kuuongoza ndege na kutumikia sekta ya anga.

> Traffic controller' anajishughulisha na masuala ya usalama wa ndege na abiria, anamwelekeza rubani cha kufanya wakati wa kutua, anashauri pia namna ya kupunguza pengine msongamano au kuchelewa angani.

Ni ushauri unaotolewa na Mwanajumaa Kombo, mwanamke wa kwanza Mtanzania kuongoza ndege 'air traffic controller'.

Air traffic control (ATC) ni kitu gani? Ni huduma au jukumu la kuongoza ndege lakini linalofanyika na wataalamu walioko ardhini, ndege ikiwa angani. Air traffic controller anawasiliana na kuiongoza ndege uwanjani, anatoa ushauri mbalimbali katika hatua zote unapohitajika na anapotakiwa kufanya hivyo.

"Traffic controller' anajishughulisha na masuala ya usalama wa ndege na abiria, anamwelekeza rubani cha kufanya wakati wa kutua, anashauri pia namna ya kupunguza pengine msongamano au kuchelewa angani. Pia anaangalia sehemu za kutua kwa ndege uwanjani, au nje ya uwanja, hata wakati wa kupaa anatoa ushauri na kuendelea kufuatilia mwenendo wa safari za ndege zikiwa angani.

Mwanajumaa anawahimiza wanawake kujitokeza kwenye kazi hizo kwani ni vizuri wanawake kujikita katika eneo hilo kwa sababu Tanzania bado ina pengo kubwa la waongoza ndege wanawake ukilinganisha na nchi nyingine duniani.

"Nawashauri watoto wa kike wafanye uthubutu wa vitu lakini wasishindwe kuthubutu kuwa marubani na waongoza ndege pia. Wanapofanya au kupanga kuwa sehemu ya fani hii watakuwa wengi zaidi kama zilivyo nchi nyingine," anasema na kuongeza kuwa ukienda mataifa mengine kina mama wapo wengi na waongoza ndege na sifa moja ni kwamba wako makini na hufanyakazi kwa ubora.



Mwanajumaa (kushoto) akiwa kazini kwenye chumba cha mawasiliano cha kuongoza ndege cha Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam. **PICHA: BEATRICE PHILLEMON**

### HISTORIA

Mwanajumaa ambaye hivi sasa ni Meneja wa Usafiri wa Anga ` Civil Aviation Manager' wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) amezaliwa katika Kijiji cha Gombero, wilaya ya Mkinga mkoa wa Tanga, anasema mpaka sasa Tanzania ina kilio cha uhaba mkubwa wa watu wa kuongoza ndege.

Anasema hali ni mbaya zaidi kwa kinamama na anawakaribisha mabinti na wasichana wa ngazi mbalimbali shuleni kuanzia shule za msingi na sekondari pamoja na vyuoni kujitokeza kusoma fani ya air traffic control.

Tanzania inauhitaji wa waongoza ndege 230 na kwamba walipo ni 137 ambao kati yao wa kike ni 23, bado kuna uhaba mkubwa wa waongoza ndege kwenye viwanja vyote vya ndege vilivyopo nchini na idadi ya wanawake ni ndogo.

Mwanajumaa ambaye ni mwongoza ndege wa kwanza Tanzania, anasema wataalamu hao ni wachache ikilinganishwa na nchi nyingine kwa hiyo kuna haja ya kuweka msisitizo na mikakati kwa kinamama na watoto wa kike ili wajitokeze kusomea fani hii.

Anasema ingawa ushiriki wa wanawake katika masomo ya sayansi, hisabati, uhandisi na tekinolojia bado ni mdogo, wasichana wasikate tamaa wafanye uthubutu wa vitu wanavyofanya au kupanga ili kuvifanikisha.

"Wanawake wafanye uthubutu kwa sababu nchi za wenzetu kama Uingereza, Singapore, Marekani Afrika Kusini, Kenya na Uganda kina mama wapo wengi na wanaongoza ndege hodari na makini," anasema mtaalamu huyo.

### KUHIMIZA

Anawakumbusha kusoma fani ya sayani na kuwakaribisha kuja kutembelea ofisini kwake ili waone jinsi wanavyoendesha ndege ambayo ndiyo kazi yao akiamini kuwa itawasaidia wanawake kupenda kusoma fani hiyo.

Anasema ingawa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania imekuwa ikiajiri watu, bado wanawake wanahitajika katika fani hiyo kwa sababu mpaka sasa wapo wachache, wanaofanya kazi katika fani hiyo ambao watoto au kinamama wanaweza kujifunza kutoka kwao.

Anasema mwanamke au mtoto yeyote atakayepata nafasi ya kusoma fani hiyo ni fursa ya kufanya mazoezi katika viwanja vya ndege ili kuwa mahiri katika uongozaji wa ndege.

Mwanajumaa anasema alipata leseni ya kimataifa ya kuongoza ndege mwaka 1988 na leseni hiyo inatolewa na Tanzania Civil Aviation Authority ( TCAA's ).

### NDOTO YAKE

Akielezea ndoto yake ya kuwa mwongoza ndege anasema alikuwa na maono ya kufanya kazi katika sekta ya anga ikiwamo kwenye viwanja vya ndege tangu akiwa mtoto na dada yake ndiye aliyemshawishi mpaka akapenda kufanya kazi katika eneo hili.

"Miaka ya zamani dada yangu alikuwa anafanyakazi ya kuhudumia wasafari kwenye uwanja wa ndege, japo alikuwa haruki hivyo hakuwa air hostess bali 'ground hostess' kwa hiyo jinsi alivyokuwa anavaa nguo zake anapendeza, mimi nilikuwa napenda na alinivutia sana, baadaye nilimwambia dada na mimi nataka kufanya kazi ofisini kwenu na baadaye aliniambia kuwa kuna kozi nyingi unaweza kusoma na hatimaye ukatimiza ndoto zako," anasema Mwanajumaa.

Anakumbuka kuwa alianza safari yake ya kusoma fani ya kuongoza ndege mwaka 1986 katika Chuo cha Usafiri wa Anga nchini na kuhitimu mwaka 1988.

Anasema kabla ya kufanya kazi katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), mwaka 1984 alijiunga na jeshi na mwaka 1985 alikuwa akifanya kazi katika kiwanda cha karatasi cha Mgololo na alipofika mwaka 1986 alianza kusoma kozi ya kuongoza ndege.

### SAUTI YA WAHANDISI

Kwa upande wake mwenyekiti na mwanzilishi wa Taasisi ya Wahandisi wa Wanawake ya "Women and Electronics in Tanzania (WOET), Emma Kabali, anasema kuwa mpaka sasa ushiriki wa wanawake katika masomo ya sayansi, teknolojia, hisabati na uhandisi ni mdogo na hii inatokana na mazingira kandamizi ambayo yanaanzia kwa mtoto wa kike tangu akiwa mdogo kwa kuaminishwa kuwa kuna kazi za kiume mwanamama hawezi kuzifanya na kuna kazi au shughuli za kike.

"Kusema wanawake wanaweza haitoshi, bali yatupasa kuonyesha kuwa kweli wanaweza na hii ni kuingia ndani zaidi kwa kuwaonyesha wanawake mashujaa hawa ambao wapo katika idara mbalimbali ambazo awali ziliaminika kuwa ni idara zinazowahusu wanaume pekee yao." Anasema.

Kibali anaeleza kuwa, mwaka uliopita WOET ilikaribisha wanafunzi wa kike katika shindano la insha na wengi walitaja moja ya sababu zinazowakatisha tamaa kutilia mkazo masomo ya sayansi, tekinolojia, uhandisi na hisabati kuwa ni kutokuwa na watu wa mifano katika maeneo hayo.

> Ukweli ni kwamba watu hawa wapo lakini bado hakuna jitihada za kutosha zilizofanyika kuwatambua, kuwatambulisha na kuainisha mchango wao.

"Ukweli ni kwamba watu hawa wapo lakini bado hakuna jitihada za kutosha zilizofanyika kuwatambua, kuwatambulisha na kuainisha mchango wao ikiwa ni kuudhihirishia umma kuwa tunao mashujaa wanawake kwenye maeneo haya na wanafanyakazi zilizotukuka," anasisitiza.

Anasema kutokana na changamoto hiyo hivi sasa WOET imeanzisha program maalumu ya kuwaibua mashujaa hawa waliofikishwa na wasiosikika na kuwaleta mbele kwa jamii ili jamii iondokane na dhana ambazo zimekuwa kikwazo katika jitihada hizi za usawa wa kijinsia.

### KUSHIRIKI UCHAGUZI

Mwenyekiti anasema, mbali na hilo mwaka huu ni wa uchaguzi, hivyo wanatoa wito kwa wanawake kujitokeza kwa wingi kuomba ridhaa ya kugombea katika maeneo yao mbalimbali kwani kwa ushiriki wao kwa wingi katika uongozi, kutasaidia kwa namna moja ama nyingine kusukuma ajenda zitakazomwinua mwanamke mahali pa kazi na kwingineko.

Anasema WOET ilianzishwa mwaka 2016 na mpaka sasa imesaidia wanafunzi watatu kutoka Chuo cha St. Joseph College of Engineering and Technology (SJUCET) na Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam (DIT) ambao wametoka kwenye familia masikini kupata ada ya shule na kuwaunganisha kupata kazi .

"Mpaka sasa mwanafunzi mmoja wa kike ameajiriwa katika kampuni ya Dangote Cement Factory Mkoa wa Mtwara na mwingine yuko katika Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) kama "Air Navigation Engineer." Anasema na kuongeza kuwa hayo ni mafanikio makubwa kwa wanawake wanasayansi wa taifa hili.

---

RIPOTI

# Wagonjwa 253 694 wapona corona duniani



Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, ni miongoni mwa viongozi maarufu duniani wanaougua corona. Kiongozi huyo amelazwa hospitalini akipatiwa matibabu . **PICHA: MTANDAO**

WATU 253,694 waliokuwa wamegunduliwa kuwa na virusi vya corona wamepona baada ya kupatiwa matibabu.

Wagonjwa hao kutoka mataifa mbalimbali takribani 253, 694 waliripotiwa kupona virusi vya corona baada ya kupatiwa matibabu katika mataifa tofauti duniani.

China ni taifa linaloongozwa kwa kuwa na idadi kubwa ya watu waliopona virusi vya corona baada ya kupatiwa matibabu. Inaelezwa kuwa wagonjwa 76, 964 ndiyo waliopona nchini China tangu kuanza kwa janga hilo mwishoni mwa mwaka 2019.

Taarifa zilizotolewa na Worldometers zimefahamisha kuwa taarifa hizo kuhusu watu waliotangazwa kupona virusi vya corona hazina utata ni sahihi.

Katika tovuti rasmi ambayo inaonyesha kwa takwimu kuhusu Covid-19, inabainisha kuwa China ndiyo inaongoza mstari wa mbele kwa kuwa na watu wengi waliopona virusi hivyo hatari.

Uhispania inashika nafasi ya pili ikiwa na watu 38,080, Ujerumani ikiwa na watu 26,400, Italia watu 20,996 na Ufaransa ikiwa na watu 15438.

### AFRIKA

Kwa upande wa Afrika inaelezwa kuwa virusi vya corona vimewashambulia watu 8,000 na kwamba takribani 334 wamefariki wakati wengine 702 wamepona.

Hata hivyo takwimu nyingine zilieza kuwa Afrika ina watu zaidi 6,700 waliothibitishwa kuwa wana corona huku mataifa mengi yakiweka na kutangaza hatua mbalimbali za kudhibiti ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa taarifa za takwimu zinazotolewa na Africa Center for Disease Control on COVID 19, bara zima limetangaza kuathiriwa na ugonjwa huo.

Takwimu hizo zinatolewa na Africa CDC katika Chuo KIkuu cha John Hopkins cha Marekani. **Africanews**

JE, WAJUA?

# Dk. Snow: Daktari aliyemaliza ugonjwa wa kipindupindu



Vimelea wa kipindupindu 'vibrio cholerae' wanavyoonekana kwenye hadubini. **PICHA: MTANDAO**

LEO dunia inasumbuliwa na corona na kila mmoja anazungumzia ugonjwa huo, lakini ikumbukwe kuwa maradhi mengi yalisumbua kikiwamo kipindupindu ambacho watu walikufa kwa muda mfupi na kwa kasi ya ajabu.

Dokta John Snow, aliyezaliwa mwaka 1813 nchini Uingereza, akiwa mtoto wa kwanza wa familia yao, iliyoishi kwenye makazi ya watu maskini waliojenga pembeni ya mto, ni mtaalaamu aliyechunguza na kubainisha sababu za watu kupata kipindupindu.

Hata sasa, jamii maskini zikiendelea kuteseka na ugonjwa huu, msomi huyu ameshamaliza kazi ya kuibua chanzo na jinsi ya kujitibu. Wakati huu wa corona ni vyema kuikumbuka historia yake.


Kwa kuwa daktari huyu makazi yao yalikuwa karibu na mto Ouse, huko Uingereza, alishuhudia mafuriko ya mara kwa mara na kuathiri sehemu ya jamii yao iliyoshambuliwa na kipindupindu.

Kwa muda mfupi wa maisha yake, alifanya mambo makubwa katika fani za magonjwa ya kuambukiza hasa maradhi ya kipindupindu na kujijengea jina kwenye sayansi ya tiba.

Daktari huyu alikuwa wa kwanza kuchunguza kwa kina mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu. Wakati ugonjwa huo ulipotokea mwaka 1854 kwenye mji wa London, mitaa ya Soho huko Westminster jijini London.

Alitafiti kuhusu uhusiano wa ugonjwa huu,vifo pamoja na vyanzo vya maji. Alichora ramani ya kitongoji cha Soho na kuonyesha ni wapi wagonjwa walipotoka na ni wapi vifo vilitokea na sehemu watu walipochota maji.

> Watatu kati ya watano walikuwa ni watoto wa shule iliyo karibu na pampu hiyo. Ilionekana wazi kuwa waliougua kipindupindu ni wale waliokuwa wanatumia maji kutoka kwenye pampu ya mtaa huo.



Dk. John Snow

Alipochora ramani inayojumuisha makazi ya wagonjwa, na ni wapi walipata maji, aliona kuwa waathirika wengi wa kipindupindu walitoka kwenye nyumba ambazo zilikuwa zinachota maji kutoka kwenye pampu iliyokuwa imewekwa kwenye barabara ya Broad Street (Sasa inaitwa Broadwick Street) au mtaa wa Broadwick.

Maji ya pampu hiyo yalitoka katika vyanzo viwili vya maji ya mto Thames na kisima kilichokuwa karibu na pampu hiyo ambavyo vilichafuliwa na kinyesi.

Alisema kuwa bila shaka majitaka hayo yalikuwa yanachafua maji ya kisima hicho na wananchi waliotumia maji yake walikuwa wanakunywa maji yaliyochanganyikana na kinyesi.

Baada ya kutoa taarifa hizi za utafiti alioufanya, pampu ya maji ya kisima hicho iliondolewa kufuatia mlipuko wa kipindupindu ulioanza mwishoni mwa Agosti mwaka 1854.

Alipotoa maelezo haya, kuwa pampu hii ya maji ya kisima cha Mtaa wa Soho, ilihusiana na mlipuko wa ugonjwa huu wa kipindupindu ilibidi iondolewe ili wananchi wasinywe maji taka yenye wadudu wa maradhi hayo.

Hatua ya Snow kugundua kuwa kisima hiki cha maji ndicho kilichosababisha mlipuko wa kipindupindu kilikuwa ni kitendo cha kihistoria katika kujua chanzo na jinsi ya kuzuia magonjwa hayo.

Snow alionyesha kwamba kampuni zilIzosambaza maji kutoka vyanzo vya mto Thames ambavyo vilikuwa vimeingiliana na maji taka vilikuwa na wagonjwa wengi wa kipindupindu kuliko maeneo ambayo yalipatiwa maji kutoka sehemu ambazo maji hayakuingiliana na majitaka.

Katika miaka hiyo ya karne ya 19 wataalamu hawakuwa wanajua kuwa chanzo cha magonjwa kinaweza kikawa bakteria, fangasi au virusi.

Wakati huu ilidhaniwa kuwa maradhi yanaletwa na hewa mbaya. Ilisadikiwa kuwa magonjwa kama kipindupindu na tauni yalisababishwa na hewa au upepo mbaya.

Daktari Snow hakuamini kuwa kipindupindu kingeweza kikaletwa na hewa chafu. Mwaka wa 1849 aliandika jarida juu ya jinsi ugonjwa huo unavyoambukiza akisisitiza kuwa haiwezekani upepo mbaya bali unaenezwa na maji yenye kinyesi. Mwaka 1855, alichapisha tena habari za kipindupindu; akaeleza kinavyoenezwa na kuambukizwa, akihusisha takwimu na uzoefu wake wa jinsi mlipuko wa kipindupindu huko Soho wa mwaka wa 1854 ulivyoenea.

Aliandika kuwa alipokwenda Soho kuchunguza chanzo cha vifo vya kipindupindu alikuta karibu vyote vilitokea kwenye nyumba zilizokuwa karibu na pampu ya maji iliyokuwa mtaa wa Broad.

Kulikuwa na vifo 10 vilivyokuwa karibu na pampu nyingine. Nyumba tano kati ya 10 wenyeji walisema walikuwa wanapata maji kutoka kwenye pampu iliyo mtaa wa Broad kwani walipendelea maji yake kuliko ya pampu nyingine.

Watatu kati ya watano walikuwa ni watoto wa shule iliyo karibu na pampu hiyo. Ilionekana wazi kuwa waliougua kipindupindu ni wale waliokuwa wanatumia maji kutoka kwenye pampu ya mtaa huo.

Uchunguzi zaidi uligundua kuwa kisima cha pampu hiyo kilichimbwa futi tatu kutoka palipokuwa na shimo la taka na mfereji wa maji taka uliokuwa unavuja.

Utafiti huu wa Dk. Snow ulikuwa wa kihistoria katika mambo ya afya ya jamii kwani ulikuwa ni wa kwanza na wa kipekee na ulikuwa ndiyo mwanzo wa fani ya sayansi ya 'epidemiolojia' au elimu ya maradhi yanayowashambulia binadamu na jinsi ya kuyatibu.

Mtaalamu huyo kwa kuchunguza kwake kisayansi mlipuko wa kipindupindu huko Soho, anakumbukwa kama baba wa sayansi ya epidemiolojia. Epodemiolojia ni sayansi ya kuchunguza vipengele vinavyohusika na afya na magonjwa yanayowashambulia wanadamu ili kupata misingi ya kubuni mbinu na mikakati ya kukabiliana na kujikinga na magonjwa huku watu wakihakikisha wanaendelea kuwa na afya bora.

Mwingereza huyo aliishi maisha ya kulinda afya yake bila kula nyama, alipendelea kula vyakula vya mboga za majani, maharage na kunde, akinywa maji yaliyochemshwa bila kugusa pombe.

Alipofikia umri wa miaka 45 alipata kiharusi na kufariki, Juni mwaka 1858. ***Mtandao***

ELIMU

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Corona ipo, si wakati wa kuzembea wala kupuuza




Kugombania daladala hasa Dar es Salaam kunawaweka abiria kwenye hatari ya kuambukizwa corona. Ni vyema kupanga foleni na kupanda kwa utaratibu. **PICHA: MTANDAO**

SISI ambao bado tunaishi, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, maana ni yeye peke yake mwenye uwezo wa kutujalia kuendelea kuishi wakati huu ya tishio la kuenea virusi COVID-19.

Kiuhalisia, COVID-19 ilianzia nchini China na hatimaye kusambaa dunia nzima kwa kasi kubwa. Kulingana na taarifa zinazotolewa mara kwa mara na viongozi wetu na serikali wengi tumeelewa hali ilivyo kuhusiana na janga la corona duniani na nchini kwetu.

Hata hivyo kupitia maombi yetu ya kila siku kwa Mwenyezi Mungu aliye mponyaji wa kweli, naamini tutaweza kuishinda corona mpaka jamii duniani ishangae kulikoni Tanzania?

Nichukue fursa hii kuipongeza serikali yetu kwa kuchukua hatua za makusudi kuzuia corona isisambae sana. Kwanza, kwa kuweka utaratibu kuwa kila mgeni au raia anayetoka nje ya nchi awekwe karantini kwa muda wa siku 14 asichanganyike na jamii.

Baada ya siku hizo kumalizika, akaonekana hana virusi vya corona utaratibu wa kawaida utafuatwa. Iwapo atagundulika kuwa na virusi atapelekwa kwa matibabu kwenye sehemu zilizoandaliwa. Pili, kutoa elimu kwa umma kuhusu janga la corona kwa kututaka tunawe mikono kutumia maji yanayotiririka na sabuni kwa muda wa takribani sekunde 20. Aidha, kutakasa viganja vya mikono yetu kwa kutumia vitakasa mikono au 'sanitizer.' Lakini pamoja na kututaka tutumie sanitizer kuweka mikono yetu katika hali ya usafi na salama; baadhi ya wafanyabiashara wakaona hiyo ni fursa nzuri kuweza kupata fedha zaidi kwa kipindi kifupi hivyo sanitizer zikapanda bei .

Serikali imeliona na imeamua sanitizer ziuzwe kupitia Bohari ya Dawa (Medical Supplies Department-MSD) hususani katika jiji la Dar-Es-Salaam.

Tunashukuru sana kwa uamuzi huo na tuombe kuwa sanitizers zipatikane muda wote na bila kikwazo chochote.

Vilevile, serikali iliamua kusitisha shughuli zenye kusababisha misongamano kama michezo ya aina yote, kufunga shule na vyuo, kututaka wananchi wasitembee bila sababu za msingi, kuacha utamaduni wa kukumbatiana na kushikana mikono wakati wa kusalimiana.

Lakini ikaamua shughuli za ibada ziendelee kufanyika kwa misingi ya kumwabudu na kumwomba Mwenyezi Mungu atusaidie na kutunusuru na janga la corona. Lakini tunaagizwa kufanya hivyo kwa tahadhari. Waamini wa dini na madhehebu mbalimbali wanatahadharishwa kuachana na tabia ya kufanya ibada kimazoea na pia kutakiwa kunawa mikono kabla na baada ya kutoka kwenye ibada.

> Sehemu za kunawa mikono pia zilionekana kuwa chache ingawa waliohojiwa wengi walikiri kufahamu corona ni nini lakini mwamko wa kujikinga ulikuwa bado wa chini.

Aidha, tunatakiwa kuyafanya hayo yote, ikiwamo shughuli za kutafuta riziki zetu za kila siku kwa tahadhari kubwa sana. Vilevile Serikali pia imeunda timu tatu za kitaifa lakini pia mamlaka za mikoani na wilayani pia zimechukua hatua ya aina hiyo kuhakikisha corona haisambai bali inadhibitiwa ipasavyo.

Vilevile, nivishukuru vyombo vyote vya habari kwa jitihada na juhudi zilizofanyika na zinazoendelea kufanyia kuhamasisha na kuelimisha umma wa Tanzania namna ya kujikinga na kuepuka kuambukizwa virusi aina ya corona.

Hakika wanahabari na watangazaji wote pamoja na timu zenu za ufundi na viongozi wote mnafanya kazi nzuri ya kupongezwa na kuwatakia kila lililojema na Mwenyezi Mungu awasaidie na kuwajalia afya njema muda wote wa mapambano.

Kutokana na juhudi za serikali na za kwenu, hakuna atakayejitetea kwa kudai kuwa yamemkuta kwa kutofahamu au kukosa kupata taarifa sahihi.

Kazi kubwa inafanyika sana kwenye maeneo ya Majiji, Manispaa, Miji na viunga vyake. Vijijini wanapata taarifa ndiyo lakini siyo kwa kiwango kama cha maeneo hayo. Ni vizuri tukaongeza nguvu huko vijijini kwa kusudio la kuinua uelewa wao wajue corona ni nini na wafanye nini kujikinga wasiambukizwe virusi-corona.

**TUBADILIKE**

Kwenye mikusanyiko mikubwa sokoni hakuna mwamko, hii inadhihirisha kuwa pamoja na jitihada zinazofanyika bado hali ya sintofahamu imo ndani ya baadhi yetu. Nimeona hali ilivyokuwa kwenye soko kuu la Dodoma, baadhi walionyesha kutojali kunawa mikoko yao.

Sehemu za kunawa mikono pia zilionekana kuwa chache ingawa waliohojiwa wengi walikiri kufahamu corona ni nini lakini mwamko wa kujikinga ulikuwa bado wa chini.

Hali ilionekana hivyo kwenye soko kuu la samaki eneo la Feri Dar-Es-Salaam. Hivyo hivyo katika soko la ndizi eneo la Mabibo, Manispaa ya Ubungo pia kwenye stendi ya daladala iliyoko Makumbusho (ingawa hapo wengi walionekana kuchukua hatua ikiwemo daladala kutobeba abiria waliosimama).

**KUGOMBEA MABASI**

Pamoja na kunawa mikono, kutumia sanitizer kizungumkuti kingine kinaoekana kwenye kupanda daladala ambako watu wanasukumana kupanda basi wengine kupitia kwenye madirisha. Kwa nini hatupangi mistari na kuweza kuingia kwenye magari kwa ustaarabu?

Kwenye mabasi ya mwendo kasi huko hali siyo shwari, lakini sasa wameanza kubadilika kidogo maana kila wakati msongamano ulikuwa mkubwa na mabasi machache.

Ipo haja kuchukua hatua za haraka kuongeza ma-mabasi, ikiwa ni pamoja na kuruhusu daladala zipeleke abiria Posta na Kariakoo kutoka Kimara na Mbezi.

Kusema kweli tusizembee hali siyo shwari maana corona inaenea kwa spidi kubwa dunia nzima. Ikitokea hali ikawa mbaya tukafungiwa ndani bila kutoka nje ndipo tutakapoonja machungu maana wengi wetu kula yetu inatokana na kutoka nje kubangaiza hapa na pale.

Wenzetu mataifa yaliyoendelea wanaouwezo kiuchumi kuzuia watu wasitoke na wakawapa riziki ya kila siku angalau kwa muda fulani. Sisi uwezo huo ni mdogo na tayari tumeishaathirika na mafuriko pamoja na miundombinu mingi kuharibika.

Fedha nyingi zinaelekezwa huko, tukiongeza janga la corona hali inakuwa mbaya zaidi. Kadhalika, tuachane na mtazamo wa "serikali ifanye" mara kwa mara wengi tunasema hivyo lakini bila kuchukua hatua stahiki.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

## Walimu wanatajwa kama wazazi wa pili wa wanafunzi kwa vile wanakaa nao muda mrefu shuleni. Je, wanatakiwa kuwa na tabia gani ili kuwajenga vyema wanafunzi wao? Wadau wanajadili.



### WILLBARD LUCAS (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

WALIMU wana mchango mkubwa sana katika malezi wetu, kwani watoto hutumia muda mwingi zaidi kukaa na walimu kuliko wazazi wao.

Kwa mantiki hiyo, walimu ni watu muhimu sana katika jamii yetu, kwani huwajenga watoto katika maadili mema tangu wakiwa wadogo.

Hivyo basi walimu wanatakiwa wawe mfano wa kuigwa kwa tabia zao na mwenendo wao mzima wa maisha, kwani wakiwa na maadili mabovu wataharibu jamii nzima ya taifa la kesho.

Lakini pia suala la kusimamia maadili au nidhamu ili kuwajenga vizuri wanafunzi sio la walimu pekee yao, bali ni jukumu la jamii nzima, hivyo wakati walimu wakifanya sehemu yao, hata sisi wazazi pia tunatakiwa kushiriki kila mmoja kwa nafasi yake katika malezi bora kwa watoto.

Ninasema hivyo, kwa sababu baadhi ya wazazi wanadhani suala la nidhamu shuleni ni jukumu la walimu, hiyo sio kweli kabisa, sote tunahusika katika malezi bora.

Ni makosa kuwaachia walimu jukumu hilo. Wazazi na walimu wana jukumu la malezi bora kwa wanafunzi, kwani mwanafunzi anapotoka nyumbani kwenda shule anakutana na mzazi wa pili ambaye ni mwalimu, hivyo ushirikiano wa mwalimu na mzazi ni wa muhimu kwa maendeleo mazuri ya mwanafunzi, vinginevyo walimu wanaweza kulaumiwa bure na kumbe wanatimiza wajibu wao vizuri lakini kwa upande wa wazazi wakawa wazembe.

Jambo la msingi ni kwamba jukumu la malezi mema ya kuandaa taifa la kesho ni letu sote.



### MONICA CHOGWE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

NJIA mojawapo inayoweza kusaidia walimu kuwajenga vyema wanafunzi ni maadili mema ya walimu na pia ushirikiano kati yao na wazazi.

Kwa sababu wazazi ni sehemu chanya ya kusababisha wanafunzi kujifunza ili kuimarisha elimu ya mtoto shuleni, njia hii inaweza kusaidia kuondoa anguko la wanafunzi wengi kwenye mitihani, kwa sababu ushirikiano wa walimu na wazazi katika kusimamia maendeleo ya wanafunzi na tabia njema ni jambo la msingi sana.

Wapo baadhi ya wazazi, ambao ni wagumu kufuatilia watoto wao shuleni wakiamini jukumu hilo ni la walimu.

Lakini ikumbukwe kuwa walimu wana majukumu makubwa, hivyo wanahitaji ushirikiano, kwani hawana uwezo wa kufuatilia mwanafunzi mmojammoja.

Hapa inamaanisha kwamba, ili mwanafunzi awe kwenye mstari mzuri, kuna watu wawili wanatakiwa kuhusika, ambao ni walimu na wazazi, lakini kila upande ukidhani sio jukumu lake, mwanafunzi hawezi kufika kokote.

Kila upande utimize wajibu kikamilifu. Ushirikiano mdogo wa wazazi na walimu ni sababu inayochangia wanafunzi kushindwa kufanya vizuri katika masomo na hata kushuka kinidhamu.

Hivyo ili kuinua kiwango cha elimu, wazazi na walezi wanatakiwa kufuatilia maendeleo ya watoto wa wanapokuwa shuleni kwa lengo la kuwakuza kielimu. Kazi hiyo sio ya walimu tu kwa sababu ufaulu mzuri wa wanafunzi unachangiwa na tabia njema na ushirikiano wa sehemu hizi mbili.



### RHOBI SAMWELLY (MKURUGENZI WA HOPE FOR GIRLS AND WOMEN) TANZANIA

KWANZA kabisa, kitaaluma mimi ni mwalimu ingawa sifundishi. Nianze kwa kuelezea kuwa ualimu ni taaluma na ni miongoni mwa taaluma zote zilizopo duniani na pia ualimu ni kazi ya kuheshimika, ingawa baadhi ya watu wamekuwa wakiidharau.

Lakini ni ukweli usiopingika kuwa, walimu wanatengeneza maisha ya baadaye ya wanafunzi. Jambo la msingi linalotarajiwa kutoka kwa walimu ni lile ambalo linawafanya waitwe kwa jina hilo, ingawa kuna changamoto nyingi zinazowakabili, lakini wanatimiza wajibu wao inavyotakiwa hata kama wapo wachache wasiotimiza wajibu wao, hao hawawezi kusababisha walimu wote wakaonekana wabaya.

Walimu waliofundishwa wakaelewa taaluma hii huwa wana tabia njema na wamekuwa wakibuni mbinu mbalimbali za ufundishaji na pia kuwasaidia wanafunzi kuwa na nidhamu ingawa nidhamu yaweza isiwe tatizo kwa wanafunzi bali kukosekana kwa mpango na utaratibu mzuri wa kazi, ambao wakati mwingine huchangia matatizo ya kinidhamu kwa wanafunzi na kusababisha wasijengwe vyema.

Binafsi kama mwalimu ninaamini kwamba walimu wana majukumu makubwa ya kuhakikisha mwanafunzi anaimarishwa kielimu na kinidhamu ili kuwa kiongozi wa baadaye.

Kwa kifupi ni kwamba walimu wanatakiwa kuwa na mfano bora ambao wanafunzi wanatauiga badala ya kuwa chanzo cha matatizo.



### GODSON MHEMA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

NIDHAMU ni jambo la msingi katika maisha ya binadamu. Nidhamu humpa mtu uwezo wa kuongoza mawazo yake na matendo yake katika mkondo sahihi.

Vile vile, uwezo huu humfanya mtu kutawala maisha yake vyema. Ni vyema kutambua kuwa bila nidhamu, mtu hawezi kupata furaha katika maisha yake na pia hakuna jambo lolote analoweza kufanya sawa iwapo hatajifunza kuwa na nidhamu katika maisha yake.

Unapokuja kwenye uongozi ni kwamba huwezi kuwaongoza wengine vizuri kama wewe mwenyewe huna nidhamu, kwani nidhamu ndio unayoweza kumfanya mtu kutawala maisha yake na kuwa na mahusiano mema na wengine.

Nimeanza kuelezea umuhimu wa nidhamu nikiwa na maana kwamba mwalimu anatakiwa kuwa na nidhamu ili kuweza kuwasaidia wanafunzi wake. Yaani wamuige kwa matendo mema, kwa sababu kama hatakuwa na nidhamu hawezi kuwasaidia kwa lolote. Hawawezi kupata cha maana kutoka kwake.

Mwalimu mwenye nidhamu atakuwa tayari kumrekebishe mwanafunzi ambaye itabainika kuwa ni mkorofi au ana tabia chafu na anaweza kudhibiti nidhamu shuleni, kwani utovu wa nidhamu huathiri mfumo mzima wa kufundisha na kujifunza. Mwalimu au walimu kwa ujumla wanatakiwa kuwaongoza wanafunzi kuwa na tabia njema na kuwawekea mipaka ya kipi wafanye na kipi wasifanye.



### WITNESS MASAKA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

SWALI lako kwamba walimu wawe na tabia gani ili kuwajenga vyema wanafunzi, jibu langu ni kwamba wanatakiwa kuwa mfano bora kuanzia kwenye tabia, mwenendo, matendo na vingine vyote vya kiutu, ambavyo vitamfanya wanafunzi wapate kitu kizuri cha kujifunza kutoka kwao.

Walimu ni wazazi wa pili kwa wanafunzi, na sidhani kama kuna wazazi wanaotaka watoto wao wawe na tabia mbovu. Wanafunzi wanapokuwa shuleni wanakuwa chini ya uangalizi wa walimu ili kuhakikisha wanazingatia maadili kana kwamba wapo nyumbani kwao.

Utovu wa nidhamu na maadili mabovu kwa baadhi ya walimu yanaweza kusababisha wanafunzi kuwa na tabia chafu. Kwa lugha nyingine niseme kuwa walimu ni kioo cha wanafunzi. Walimu wana kazi nyeti ya kujenga maadili mema kwa wanafunzi. Kuna malalamiko ambayo yanawalenga baadhi ya walimu kwamba hawana maadili mema, sidhani kama katika vyuo vya ualimu wanafundishwa kinyume. Mwalimu anapokwenda kinyume na maadili ya kazi yake ni tabia yake mwenyewe.

Kwa sababu mwalimu aliyefundishwa akaimarika, atakapokuwa kazini hawezi kwenda kinyume na maadili ya kazi yake, hawezi kuthubutu kujihusisha na mambo yasiyotakiwa. Walimu wawajengee uwezo wanafunzi kuhusu stadi za maisha zinazoweza kuwasaidia kuepuka vishawishi vikiwamo vya kujihusisha na mambo yasiyofaa, badala yake wakazanie elimu.





# Mbalizi wahofia kupoteza mazao

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAKULIMA wa mahindi katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, wameingiwa na hofu ya kupoteza mazao yao kutokana na kuibuka kwa wimbi la wizi wa mazao yao yakiwa shambani ambao unafanywa na watu wasiojulikana.

Inadaiwa kuwa wezi hao huwa wanavuna mahindi nyakati za usiku na kutokomea nayo, hali ambayo inawasababishia wakulima hasara na kutokana na kutumia gharama kubwa kwenye uzalishaji.

Mmoja wa wakulima hao, Juma Mwazyela alisema mahindi bado hayajakauka lakini wezi hao wanawalazimisha kuyavuna hivyo hivyo hali ambayo itasababisha mavuno kutokuwa bora kama ambavyo huwa wanafanya miaka yote.

"Nimetoka shambani jioni kupanda maharage na mahindi, yalikuwa vizuri kabisa lakini nawahi asubuhi nakuta nusu ya shamba limevunwa na mahindi wameondoka nayo... sasa tunapata wasiwasi kuwa huu ni mwaka wa hasara," alisema Mwazyela.

Alisema mbali na wezi hao kuvunja mahindi, lakini huwa hawathamini maharage yaliyomo kwa kuyakanyaga kanyaga na kuyafanya yaanze kunyauka.

Naye Sophia Saimon, alisema watalazimika kuanza kulala mashambani kulinda kwa maelezo kuwa mwaka huu mahindi yana soko zuri na ndiomaana wezi wameanza kuiba.

Alisema mavuno hayajaanza kutokana na mahindi bado hajakauka vizuri lakini ukienda sokoni yanauzwa sio chini ya Sh. 10,000 kwa debe wakati miaka mingine kipindi cha mavuno huwa yanauzwa mpaka Sh. 4,000.

# Ahadi ya Mwl. Nyerere Kyela yatekelezwa baada miaka 38

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

SERIKALI imetekeleza ahadi ya kuwajengea wananchi wa Kata ya Ikimba wilayani Kyela ambayo iliahidiwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Alitoa ahadi hiyo wakati wa ziara yake wilayani humo mwaka 1982, ikiwa miaka mitatu kabla ya kung'atuka madarakani.

Utekelezaji wa ahadi hiyo umeanza kwa Serikali kutoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya kuanza mradi huo, ambapo wakazi wa kata hiyo wanadai walikuwa wameshakata tamaa wakiamini kuwa haitakuja kutekelezwa.

Wakizungumza na Nipashe walipokuwa wanaendelea na ujenzi wa Kituo hicho, wananchi hao walimshukuru Rais John Magufuli kwa kuidhinisha fedha hizo, na kwamba na wao wataendelea kuchangia nguvu zao.

Hitson Mwanyilu, alisema wakati Mwalimu Nyerere anatoa ahadi hiyo yeye alikuwa kutafuta maisha Zambia, na aliposikia taarifa hizo alifurahi na kuamini kuwa sasa wangepata ahueni ya kutotembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.

Alisema baada ya hapo haikuwahi kutekelezwa na waliendelea kusafiri umbali mrefu kupata huduma za afya Kyela mjini hali ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikihatarisha maisha yao.

"Tunamshukuru sana Rais Magufuli, maana tunamuona anapita kwenye njia zile zile za baba wa Taifa letu, anatembea kwenye kumbukumbu zile zile mpaka ametukumbuka na sisi wananchi wa Ikimba na sisi tunaahidi kuwa tutafanya kazi kwa ushirikiano," alisema Mwanyilu.

Naye Rachael Ipeta, alisema kwa kipindi kirefu wanawake wa Kata hiyo walikuwa wanapata shida hasa wanapokuwa wajawazito kwa kusafiri mpaka Kyela Mjini ilipo Hospitali ya Wilaya kwenda kupata huduma za afya.

Alisema kwa sasa Kituo cha Afya Ikimba kikikamilika watakuwa wanapata huduma jirani na hivyo hata gharama za usafiri hazitakuwa kubwa kama ilivyokuwa awali ambapo wakati mwingine walikuwa wanaamua kwenda kuweka kambi hospitalini.

Alisema baadhi ya wanawake walikuwa wanajifungulia njiani ama nyumbani kutokana na kuchelewa kwenda hospitalini ama kushindwa kumudu gharama za usafiri wa kwenda hospitali.

"Wataalamu wanashauri kuwa sio vizuri kumpakia mama mjamzito kwenye pikipiki wakati wa kwenda kujifungua... sasa sisi kutoka hapa kwenda Kyela ni mbali sana, hivyo tunamshukuru rais wetu kwa kutukumbuka," alisema Rachael.

Alisema kituo hicho kitawasaidia hata kurahisisha huduma endapo itatokea mgonjwa wa usiku kwa maelezo kuwa watakuwa wanatembea hata kwa mguu.

Kaimu Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Khamis Ango, alisema wananchi hao wameanza ujenzi wa Kituo hicho kwa kuanzia na jengo la wagonjwa wa nje (OPD), ambalo alisema alidai litakamilika mwishoni mwa mwezi huu.

Alisema ujenzi wa kituo hicho unatumia utaratibu wa akaunti ya dharura (Force account) ambao unahamasisha matumizi ya mafundi wa mitaani badala ya kutumia makandarasi.

Ango alisema ofisi yake itahakikisha inasimamia ujenzi wa Kituo hicho ili kijengwe kwa viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa sheria na kituo kidumu kwa muda mrefu.

Diwani wa Ikimba, Katule Kingamkono, aliwataka wananchi wa Kata hiyo kujitokeza kwa wingi kila siku kushiriki kwenye ujenzi huo ili kituo kikamilike haraka na waanze kupata huduma.

Aliiomba Serikali kuwapelekea watumishi vitendea kazi katika kituo hicho kikishakamilika ili huduma zianze kutolewa mapema kwa maelezo kuwa haitakuwa na maana kituo kikamilike halafu kiwe kinachelewa kufunguliwa.



Baadhi ya watoto wakitafuta chupa za maji, kwenye jalala lililopo nje ya bustani ya Jiji la Mbeya, mwishoni mwa wiki, kwa ajili ya kuziuza. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kamati kudhibiti moto mashambani

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAKAZI wa vijiji vya Kata ya Igoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamekubaliana kuunda kamati maalumu za kudhibiti matumizi ya moto wakati wa kuandaa mashamba ili kulinda misitu na uharibifu wa mazingira.

Wananchi hao wanadai kuwa matumizi ya moto huo wakati wa kuandaa mashamba umekuwa ukiwashinda na kuteketeza misitu ya asili na ya kupandwa na hivyo kuharibu mazingira.

Walifikia uamuzi wa kuunda kamati hizo mwishoni mwa wiki wakati wa kupokea msaada wa mbao 1,000 na mifuko 100 ya saruji kutoka kwa viongozi wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) kupitia shamba la misitu la Kiwira kwa ajili ya kukamilisha kituo cha afya cha kata hiyo.

Mmoja wa wakazi hao, Pascal Mahenge, alisema misitu ya eneo hilo ambayo inamilikiwa na serikali na watu binafsi ina msaada mkubwa kwao na hivyo lazima waunde kamati za kuilinda.

Alisema makubaliano yao ni kwamba mtu yeyote atakayetaka kuchoma moto kwenye shamba lake wakati wa kuandaa, ni lazima awasiliane na kamati hiyo ili ikajiridhishe kama moto huo hauwezi kuleta madhara kwenye misitu.

"Wenzetu kule Mbulu wameweza kukomesha matumizi ya moto kwenye mashamba, hivyo hata sisi tunaamini itawezekana tu, mbali na mbao tulizopewa pamoja na saruji lakini tunaamini hali ya hewa nzuri tuliyonayo ni kwa sababu ya uwepo wa hii misitu kwa hiyo tunawahakikishia kuwa tutashirikiana kuilinda," alisema Mahenge.

Alisema msaada waliopewa ni mkubwa na utasaidia kuharakisha mradi wa ujenzi wa kituo cha afya, na kwamba wangetaka kuchangishana, wangechukua muda mrefu kukamilisha.

Diwani wa Kata hiyo, Fred Mwankenja, aliwataka wenyeviti wa vijiji na watendaji kusimamia utaratibu huo wa kusimamia misitu kwa maelezo kuwa wananchi wanatakiwa kuelimishwa vizuri ili wasije waendelea kukiuka taratibu.

Alisema viongozi wa vijiji ndio wanaotakiwa kuwa mstari wa mbele kulinda misitu hiyo na kwamba wananchi wanatakiwa kuongozwa kwa makubaliano ya kijiji.

"Hatutaishia tu kudhibiti matukio ya moto lakini pia hata kuwadhibiti wanaoingia kuiba miti kwenye misitu hii, hatutavumilia kuona tatizo lolote linatokea kwenye maeneo haya wakati tupo," alisema Mwankenja.

Akikabidhi msaada huo wa mbao na saruji, Meneja wa Shamba la miti la Kiwira, Lucas Sabida, alisema waliamua kuwasaidia wananchi wa Kata hiyo kutokana na ushirikiano wao kwenye ulinzi na utunzaji wa msitu huo.

Alisema msitu huo uko salama na hauvamiwi na wezi kwa sababu ya ulinzi ya wananchi hao na kwamba ndio maana waliamua kuchangia ujenzi baada ya kuona wananchi wanachangishana kutaka kuezeka jengo la wagonjwa wa nje (OPD).

"Lakini pia sisi ni sehemu ya jamii ya Kata hii, tukipata matatizo tunaweza tukatibiwa hapa, sasa tumechangia na naamini mchango wetu utasaidia kukabiliana na upungufu uliopo," alisema Sabida.

Aliwataka wanaotaka kupanda miti kwenda kununua miche iliyoandaliwa na TFS kitaalamu kwa maelezo kuwa baadhi ya miti huwa haistawi vizuri kutokana na maandalizi.





# Miradi ya kimkakati Dodoma sasa kuzinduliwa mwezi huu

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MIRADI ya kimkakati ya Jiji la Dodoma ya stendi kuu ya mabasi, Soko kuu la Ndugai na kituo cha mapumziko cha Chinangali Park, iliyogharibu zaidi ya Sh. bilioni 89, inatarajia kuzinduliwa Aprili 26, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Kunambi alisema miradi hiyo yote imeshakamilika kwa asilimia 100, hivyo aliwataka wakazi wa Dodoma na maeneo mengine nchini kuzitumia fursa zinazotokana na miradi hiyo mikubwa ya kimkakati.

Akizungumzia mradi wa stendi kuu ya mabasi ya mikoani, Kunambi alisema, itakuwa na uwezo wa kuchukua watu 1,200 kwa wakati mmoja wanaosubiria usafiri.

"Stendi hii itakuwa ni ya kimataifa Afrika mashariki, itakuwa stendi ya kwanza ambayo ina eneo la watu maalum (VIP) na imejengwa kisasa sana na kwa hili sisi wana-Dodoma tunamshukuru sana Rais John Magufuli," alisema Kunambi.

**"Stendi hii itakuwa ni ya kimataifa Afrika mashariki, itakuwa stendi ya kwanza ambayo ina eneo la watu maalum (VIP) na imejengwa kisasa sana na kwa hili sisi wana-Dodoma tunamshukuru sana Rais John Magufuli," alisema Kunambi.**

Akizungumzia ujenzi wa Soko Kuu la Ndugai, Kunambi alisema kuwa litahudumia kata zote 41, za jiji la Dodoma.

Kuhusu kituo cha kupumzikia cha Chinangali Park, alisema kuwa kitakuwa na michezo mbalimbali ikiwamo kuogelea, tenes, vyakula na vinywaji.

Kunambi pia aliwataka wakazi wa Dodoma pamoja na maeneo mengine kuchukua fomu kwa ajili ya kupata maeneo ya kuwekeza biashara mbalimbali katika maeneo hayo yote ili wawe sehemu ya kujenga uchumi wa mkoa.

Aliongeza kuwa jiji linatarajia kukamilisha ujenzi wa kituo cha malori, ambacho kitakuwa na uwezo wa kuegesha malori 300, kwa wakati mmoja.




Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi (katikati), akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jijini humo jana, kuhusu kuanza kwa miradi mikubwa mwezi huu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Simbachawene awachachamalia waharibu mazingira

**Na Mwandishi Wetu, MPWAPWA**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema yupo tayari kukosa kura za watu wanaoharibu mazingira kwenye Jimbo la Kibakwe.

Simbachawene alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki, katika ziara iliyofanywa na Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dodoma, kuangalia uharibifu wa miundombinu uliotokea Wilaya ya Mpwapwa.

Alisema hayupo tayari kupigiwa kura na watu wanaoharibu vyanzo vya maji na mazingira.

"Hizo kura mimi sizihitaji, najua wanaoathirika ni wengi, watanipa kura tufike hatua tuamue... Kiboyani tumezungumza, lakini mawasiliano ya watu kule miti haibaki ,uharibifu ni kila siku, itafika wakati Mpwapwa haitabaki," alisema.

Alisema imefika hatua sasa ili kuiokoa Mpwapwa ni lazima serikali iingilie kati, kinachofanyika kwa sasa nyumba zitaondoka na barabara za lami zinazojengwa zitasombwa na maji kutokana na mkondo mkubwa wa maji. Alisema uharibifu wa miundombinu umetokana na kiasi kikubwa cha mvua kunyesha eneo la Mpwapwa, ambapo maji kutoka milima yanashuka kwa kasi kubwa hali iliyochangiwa na uharibifu wa mazingira.

"Watu wamevamia kwenye milima na kufanya shughuli za kibinadamu tunapambana... naomba nimpongeze Mkuu wa Wilaya, anajitahidi, ni wajibu wa chama na serikali kutoa elimu na kuwaondoa kwenye milima kwani uharibifu ni mkubwa sana, hii Mpwapwa itafika siku itaondoka yote," alisisitiza.

Naye, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Godwin Mkanwa, alisema kauli ya Simbachawene inapaswa kuungwa mkono na kila kiongozi na kupitia vikao mbalimbali waweke suala la uharibifu wa mazingira kuwa ajenda ya kudumu.

"Tuungane na Simbachawene anapozikataa kura za waharibifu wa mazingira... mimi niliwahi kuzikataa hadharani, lakini zilinigharimu hawakunipigia kura, lakini bora wasipige kura bora kuliko kugharimu kiasi hiki," alisema.

Alisema viongozi wachukue hatua madhubuti na wafanye uamuzi mgumu. "Mwenyekiti wa CCM Wilaya, chukueni hatua kwenye vikao vyenu, pitisheni mambo...Mwenyekiti Halmashauri chukueni hatua na mara nyingine sisi matawi yetu tutafuta, mimi ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa, tunafuta matawi yaliyopo kwenye vyanzo vya maji, tunafuta matawi yaliyopo kwenye uharibifu wa mazingira tunafuta," alisisitiza.

# Kanisa Anglikana lachukua hatua corona

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

KATIKA kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa wa corona, Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Centrel Tanganyika, imeongeza idadi za ibada na kufupisha muda ili kuepukana na mrundikano wa waumini wanapokusanyika kwa mara moja.

Uamuzi wa kuongeza idadi ya ibada hizo, utasaidia kuepukana na maambukizi ya ugonjwa wa corona, serikali inaposisitiza katazo la mikusanyiko.

Uamuzi huo ulitangazwa na Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Dickson Chilongani, alipokuwa akihubiri kwenye ibada ya misa ya matawi juzi katika Kanisa Kuu jijini Dodoma.

Alisema ili kutekeleza maagizo yanayotolewa na serikali, kwa upande wa kanisa wameamua kuongeza idadi za ibada ambazo ili waumini wachache waingie, na kwamba hata watakapokuwa ndani, wataachiana nafasi ya kutosha bila kugusana.


Alisema Rais John Magufuli ameruhusu kufanyika kwa ibada kwenye makanisa na misikiti, hivyo lazima watumie fursa ya kuabudu kwa kufuata maelekezo kutoka kwa viongozi.

"Kanisa hapo mwanzo tulikuwa na ibada tatu, lakini kuanzia Jumapili ya Pasaka tutakuwa na ibada nne, tena za muda mfupi ili kuepukana na maambukizi ya corona," alisema.

Askofu Chilongani alisema kuwa kanisa linapoongeza idadi ya ibada, Wakristo watapungua, hivyo kutoa nafasi ya ukaaji wenye nafasi.

Kwa upande wake, Katibu wa kanisa hilo, Chrisper Mlule, alisema kuwa wakati viongozi wa serikali wameruhusu kuabudu, ni vizuri kutekeleza maagizo katika kujikinga na maambukizi ya corona.

Alisema kuwa kutokana na serikali kuwapa uhuru wa kuabudu, hawanabudi kutekeleza maagizo ikiwamo kutoa elimu katika maeneo ya kazi na familia.





# Masharti magumu utoaji leseni biashara vileo yaja

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Zanzibar imesema Mswada wa Sheria ya mwenendo wa matumizi ya vileo lengo lake ni kudhibiti utitiri wa kuanzishwa kwa vilabu vya pombe katika maeneo ya makazi ya watu na kusababisha kuporomoka kwa maadili, mila na silka za Wazanzibari.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Haji Omar Kheir, wakati akiwasilisha Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vileo wa mwaka 1928, ambao ulitungwa katika kipindi cha ukoloni.

Kheir alisema biashara ya vileo imekuwa huru kupita kiasi na kuonekana ni jambo la kawaida huku ikifanyika katika maeneo ya makazi ya kawaida ya wananchi.

Alisema jambo hilo halikubaliki na limezusha malalamiko makubwa kutoka kwa jamii kutokana na kuathirika kwa mila na utamaduni huku vijana wengi wakiiga na kujiingiza katika ulevi.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kuleta mswada huu mbele yanu kwaajili ya kufanya marekebisho makubwa kwa sheria iliyopo sasa ambayo imeifanya biashara ya vileo kuwa huru na kufanywa na mtu yeyote anayependa, bila ya kuwapo kwa masharti yanayoendana na mila na silka za utamaduni wetu," alisema.

Alisema lengo la kuleta mswada huo ni pamoja na kuweka masharti bora ya kudhibiti holela ya biashara hiyo ikiwamo kufanyika mbali na makazi ya wananchi.

Pia, aliyataja masharti mengine ya msingi yanayokusudiwa kuwekwa katika mswada mpya wa sheria ya vileo ni kudhibiti utoaji wa leseni na vibali vya biashara hiyo.

"Tunataka kuweka masharti magumu ya utoaji wa leseni na vibali vya biashara ya pombe ikiwamo kuona biashara yenyewe inafanyika sehemu gani," alisema. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalumu za (SMZ), Zulfa Mmaka, alisema kamati inaunga mkono marekebisho ya mswada huo pamoja na kuweka masharti magumu ya kuwapo kwa vibali vya kufanya biashara ya vileo.

Mmaka alisema kwa muda mrefu yapo malalamiko kutoka kwa wananchi katika maeneo mbalimbali kuhusu kuanzishwa kwa vilabu vya pombe katika makazi ya wananchi.

Alisema wananchi wengi wakitoa malalamiko hayo huambiwa wayafikishe katika bodi ya vileo ambayo alidai imeshindwa kufanya kazi na kuchambua malalamiko ya wananchi ya msingi.

"Sisi Wawakilishi tulikuwa tukiusubiri kwa muda mrefu Mswada wa sheria ya kudhibiti vileo ambao matarajio yetu ndiyo muarobaini wa kulipatia ufumbuzi tatizo la kuibuka kwa nyumba za vileo kila sehemu," alisema.

Alisema maduka yanayouza biashara ya vileo yanatakiwa kutengwa na yasichanganyike katika makazi ya wananchi ili kulinda maadili ya wananchi wakiwamo vijana.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman (kushoto), akimkabidhi Sheha wa Shehia ya Muyuni A, Maulidi Hassan Zidi, vifaa kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa corona, zikiwamo ndoo ya kusafisha mikono, sabuni na vitakasa mikono (sanitizer), katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wawili kutoka Tanga wathibitika na virusi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Afya Zanzibar, imethibitisha kupatikana kwa watu wawili wakitokea mkoa wa Tanga wakiwa wameambukizwa na ugonjwa wa corona.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Waziri wa Afya Hamad Rashid Mohamed, watu hao waliingia nchini wakitokea Tanga na kupitia katika bandari ya Mkokotoni, mkoa wa Kaskazini Unguja.

Taarifa hiyo ilifafanua zaidi na kuonyesha kwamba mgonjwa wa kwanza ni mwanamume mwenye umri wa miaka (33), ambaye ni Mwalimu wa shule moja ya Tanga ambaye aliingia nchini Machi 18, kupitia bandari ya Mkokotoni.

Mgonjwa wa pili ni mwanamume mwenye umri wa miaka (27), mfanyakazi wa hoteli moja Zanzibar ambaye aliondoka nchini Februari kwa likizo na kurudi Zanzibar Machi 13 na kugunduliwa na ugonjwa huo.

"Wizara ya Afya ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa taarifa ya kuongezeka kwa wagonjwa wawili wa ugonjwa wa corona na kufanya idadi kufikia wagonjwa saba kwa sasa," alisema.

Wagonjwa hao wamefikishwa katika kituo cha kupokea wagonjwa walioambukizwa na ugonjwa huo kilichopo Kidimni, Wilaya ya Kati, Unguja.

Baadhi ya wananchi wameitaka serikali kufunga baadhi ya bandari zinazotumiwa na wananchi kupokea wageni kutoka mikoa ya Tanzania Bara.

Bandari ya Mkokotoni hutumiwa na wananchi wengi wanaoingia kutoka Tanga ikiwamo maeneo ya Pangani, Kipumbwi pamoja na Kigombe.

"Tunaiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchukua hatua za kufunga kwa muda baadhi ya bandari zinazoingiza watu kutoka mikoa ya Tanzania Bara ikiwamo Tanga," alisema Juma Khamis.

# Vijana Z'bar waaswa kuisaidia serikali dhidi corona

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

VIJANA nchini wametakiwa kuiunga mkono na kuisaidia serikali katika vita dhidi ya maradhi ya corona ili kupata jamii yenye afya.

Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Mfenesini kichama, Haji Abdallah Daima, alisema hayo katika hafla ya makabidhiano ya vifaa vya kunawia na vitakasa mikono vilivyotolewa na Baraza la Vijana Shehia ya Chuini, Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja.

Alisema katika vita dhidi ya maradhi hayo, kunahitajika nguvu za pamoja na kuwapongeza vijana hao kwa kufanikisha upatikanaji wa vifaa hivyo ambavyo vitasaidia kuongeza kinga dhidi ya virusi hivyo.

Aliwataka wananchi wa shehia zinazopakana na bahari kuacha usiri na kutoa taarifa za wageni wanaoingia katika shehia zao ili kuzuia uwezekano wa kusambaa kwa virusi vya ugonjwa huo.

"Kama kuna jambo tunatakiwa kuwa makini nalo kwa sasa ni kuepuka muhali wa kutoa taarifa za wageni wanaoingia katika shehia zetu ambao walikuwapo nje ya nchi jirani kwa kutumia bandari bubu kwa usalama wetu na wao," alisema Daima.

Akitoa maelezo kuhusu vifaa hivyo, Katibu wa Baraza la Vijana shehia ya Chuini, Hafidh Haji Othman, alisema vifaa hivyo vimetolewa kwa masheha, ofisi za CCM wadi, misikiti, makanisa na vyuo vya kur-ani vilivyomo katika jimbo la Mfenesini, wilayani humo.

Alisema pamoja na kutoa vifaa hivyo Baraza hilo limejipanga kushirikiana na wataalamu wa afya kutoa elimu ya kinga dhidi ya maradhi hayo kwa makundi mbali mbali ndani na nje ya shehia yao.

"Tunajua maradhi haya ni tishio na yameshaenea katika maeneo mengi ulimwenguni, hivyo sisi kama vijana tumejizatiti kutoa elimu ya tahadhari ili yasiendelee kutapakaa katika jamii yetu," alieleza Hafidh.

Kwa upande wake, mlezi wa Baraza hilo ambaye pia ni Sheha wa shehia ya Chuini, Mohammed Shehe Kheir, aliwataka viongozi waliokabidhiwa vifaa hivyo kuvitumia kama ilivyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kuzingatia usafi wa mazingira yanayowazunguka.

Alisema ingawa Zanzibar ina idadi ndogo ya wagonjwa waliothibitishwa kuwa wameambukizwa virusi hivyo, kuna haja ya kuendelea kuchukua tahadhari ili kuzuia kuongezeka kwa idadi hiyo.

# Serikali, TPSF kukabili pamoja changamoto za biashara mtandao

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) wameandaa mfumo wa kieletroniki wa kupeana malalamiko, maoni na kupata mrejesho ili kuinua daraja wa uwekezaji nchini na kuzidi kuboresha mazingira ya kufanya biashara.

Hayo talibainishwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, hivi karibuni wakati akiwasilisha bajeti ya ofisi yake kwa mwaka 2020/2021, na kusema mfumo huo utaanza mwaka huo wa fedha.

Aliusifu mfumo huo na kusema utapunguza urasimu na kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wawekezaji na kulieleza kwamba juhudi ya Watanzania kujiletea maendeleo ya kisasa inazaa matunda.

"Mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara vimeendelea kuimarika, na ushahidi huu unathibitishwa na taarifa ya hivi karibuni ya Benki ya Dunia juu ya wepesi wa kufanya Biashara ya mwaka 2020. Tanzania imepanda kwa nafasi tatu kutoka nafasi ya 144 hadi nafasi ya 141,''alieleza.

Alifafanua kuwa mfumo huo wa kieletroniki utaongeza ufanisi zaidi katika ukuzaji, uwekezaji na ufanyaji biashara nchini.

Aliahidi kwamba serikali ikishirikiana na TPSF itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara ili kupata nafasi za juu ya dunia katika eneo hili.

Waziri Mkuu alizitaka taasisi zote za serikali kuweka mazingira mazuri na rafiki kwa uwekezaji, kuimarisha uratibu wa ukaribu na kufungua fursa zaidi za uwekezaji na ufanyaji biashara.

"Serikali itaendelea kuhamasisha mikoa yote nchini kuandaa makongamano ya uwekezaji na kuzindua miongozo ya uwekezaji ya mikoa inayobainisha fursa za uwekezaji ili kufikia nafasi ya juu ya utendaji ifikapo mwaka 2025," amesema Majaliwa.

Kwa mujibu wa Majaliwa, serikali itahakikisha maeneo ya uwekezaji yanatengwa na kuendelezwa kwa kuwekewa miundombinu ya msingi.

"Juhudi kubwa imefanywa na serikali za mikoa kwa kuzindua miongozo ya fursa za kiuwekezaji ambapo jumla ya hekta 854,821 zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo ya halmashauri zote nchini,'' alisema.

Mikoa ambayo imezindua miongozo ya uwekezaji ni Ruvuma, Songwe, Pwani, Lindi, Mtwara, Kagera, Geita, Kilimanjaro, Simiyu, Manyara, Dodoma, Mwanza, Kigoma, na Morogoro.

Hadi Februari 2020 jumla ya miradi 146 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1,514.57 imesajiliwa na inategemewa kutoa ajira za moja kwa moja 26,384.

**"Serikali itaendelea kuhamasisha mikoa yote nchini kuandaa makongamano ya uwekezaji na kuzindua miongozo ya uwekezaji ya mikoa inayobainisha fursa za uwekezaji ili kufikia nafasi ya juu ya utendaji ifikapo mwaka 2025," amesema Majaliwa.**

# DC apiga 'stop' uuzaji vyakula sokoni usiku

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, amepiga marufuku masoko ya vyakula nyakati za usiku na bidhaa zinazopangwa chini, akisema utaratibu huo ni hatari kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona.

Amesema wateja wa vyakula hivyo wako hatarini kupata kirahisi maambukizo ya virusi hivyo kwa kuwa wanakula bila kunawa mikono yao kwa vitakasa mikono.

Macha alitangaza marufuku hiyo juzi alipozungumza na waandishi wa habari mjini hapa, akipiga marufuku pia michezo ya bao na drafti kwenye maeneo ya masoko wilayani hapa.

Alisema ameamua kupiga marufuku masoko ya vyakula nyakati za usiku na bidhaa zinazopangwa chini baada ya kubaini kuwa nyakati za asubuhi, wafanyabiashara wanauza bidhaa za kawaida lakini usiku wanaongeza vyakula.

"Mfano soko la Namanga, wateja wamekuwa wakinunua vyakula vilivyoandaliwa kabisa kama vile nyama, ndizi zinakuwa zimemenywa, mboga za majani na msongamano wa watu unakuwa mkubwa nyakati za usiku, sasa ni marufuku," aliagiza.

Alisema masoko yanayoendeshwa mchana na magulio yataendelea kama kawaida lakini wilaya hiyo kwa sasa hairuhusu mrundikano wa watu kwenye masoko wakicheza drafti, karata au bao kwa kisingizio kuwa wanasubiri mizigo.

Alisema wafanyabiashara wanapaswa kuzingatia agizo lililotolewa la kufunga masoko ila inapotimu saa 12 jioni, akiwataka watendaji wa kata, viongozi wa masoko, maofisa maendeleo ya jamii na maofisa afya kusimamia utekelezaji wa agizo hilo.

Macha alisema maeneo mengi kumekuwa na ndoo, lakini uwekaji wake na sabuni hauko katika utaratibu mzuri, akifafanua kuwa vifaa vinatakiwa viwe kwenye hali ya usafi na kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu.



Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi (wa tatu kulia), akipokea sehemu ya mbegu za mahindi tani nne zenye thamani ya Sh. milioni 20 kutoka kwa Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Mwambapa, mkoani humo mwishoni mwa wiki. Msaada huo umetolewa na benki hiyo kupitia ombi maalum la Mbunge wa Kuteuliwa wa mkoa huo, Salma Kikwete (wa pili kushoto), ili kuwasaidia wananchi ambao mashamba yao yaliathiriwa na mafuriko mapema mwaka huu. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Lindi Mjini, Shaibu Ndemanga na (kulia) ni Meneja wa benki hiyo CRDB Kanda ya Kusini, Jenipher Tondi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ikungi yawamwagia vijana mil. 50/-

**Na Mwandishi wetu**

HALMASHAURI ya Ikungi, mkoani Singida, imetoa mikopo ya Sh. milioni 50 kwa vikundi vya vijana ambavyo kwa sasa vinatengeneza mifuko mbadala na kuisambaza mkoani humo.

Mkuu wa mkoa wa Singida, Dk. Rehma Nchimbi, alifanya ziara na kuzindua kiwanda cha kutengeneza mifuko mbadala kilichoanzishwa na kikundi cha New Bright Future cha vijana 10 katika kijiji cha Siuyu wilayani Ikungi.

Pia, alitembelea mradi wa kutengeneza matofali ya saruji wa kikundi cha Jitume Vijana chenye vijana 10 kwenye Kijiji Ikungi, lengo likiwa ni kuwawezesha kuajiajiri na kuajiri wengine.

Vikundi vyote vimepewa jumla ya Sh. milioni 25 kila kimoja, ikiwa ni mkopo usiokuwa na riba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema halmashauri imeshatoa Sh. milioni 127 kwa wanufaika 78 wa makundi ya vijana, kina mama na wanye ulemavu.

Aidha, alisema halmashauri hiyo inatarajia kutoa hadi milioni 150 kwenye mwaka huu wa fedha endapo makusanyo yatakuwa kama yalivyokadiriwa

Dk. Nchimbi alieleza kuridhishwa na ubunifu wa kusaidia makundi hayo uliofanywa na halmashauri hiyo ambayo itaongeza ajira na kuwafanya vijana kujituma zaidi.

Pia, alisema viwanda hivyo ambavyo vitaendelea na uzalishaji vitaondoa vijana kukaa bila kazi, na hasa wakati huu wa kujiepusha na maambukizi ya corona.

Aliutaka uongozi wa halmashauri hiyo kuhakikisha unatatua changamoto kwa vikundi hivyo ikiwamo masoko ya bidhaa wanazozalisha na kupatia elimu zaidi, ili kuwawezesha kurejesha fedha ya Serikali kama inavyotakiwa.

"Nazielekeza halmashauri zote mkoani hapa, kuiga kinachofanywa na Ikungi katika kutoa mikopo kwa makundi haya kwa kuanzisha miradi endelevu huku akipiga marufuku utoaji wa mikopo ya fedha," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa pia alitembelea soko la viazi katika kitongoji cha Kideka, kijiji cha Nkunikana, na kuwapongeza wafanyabiashara hao huku akiwasisitiza kujikinga na corona.

Dk. Nchimbi aliwataka wakulima wa viazi lishe kuendelea kulima kwa bidii ili wananchi wapate lishe bora kutokana na viazi hivyo.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa mkoa, ugonjwa Covid-19 uwe ni chachu ya kufanya kazi kwa bidii za uzalishaji, kwa kwamba viwanda hivyo viwe darasa maalum ya kutolea mafunzo hayo bila malipo kwa vijana wengine ili kuwapa maarifa kwa vijana wengi zaidi

Aidha, alitoa Sh. milioni moja huku Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ikitoa Sh. milioni 5 na kufanya jumla ya Sh. milioni 6 zilizoombwa na kikundi cha The New Bright Future kwa ajili ya kununua malighafi.

Awali, Katibu wa kikundi cha The New Bright Future, Petro Mwacha, alishukuru Serikali kwa kuwapa mkopo huo na kusisitiza kuwa mradi huu umelenga kuunga mkono juhudi za rais

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogolo, alisema Serikali imejipanga vizuri kujikinga na corona kwenye maeneo mbalimbali.

## HABARI KIMATAIFA

### Corona yawakata mishahara Rais Kagame na maofisa wake

**KIGALI,** Rwanda

KATIKA mapambano dhidi ya ugonjwa wa virusi vya corona, Serikali ya Rwanda, imeamua kuwa mawaziri wote, Wakuu wa taasisi za umma na maofisa wakuu wengine watatoa mishahara yao ya mwezi mmoja.

Hatua hiyo ya kukatwa mshahara wa mwezi Aprili ni jitihada za pamoja katika kupambana na virusi vya corona nchini humo.

Maofisa wa serikali wanaoangaliwa na hatua hiyo ni takriban 260, wote kwa ujumla mshahara wao wa mwezi ni takriban dola za Marekani 74,000.

Wiki iliyopita Shirika la Fedha Duniani (IMF), uliidhinisha mkopo wa dola za Marekani 109 kwa serikali ya Rwanda kupiga jeki uchumi wa Rwanda unaoyumba kutokana na ugonjwa wa virusi vya Corona.

Mwandishi wa BBC aliyeko mjini Kigali, Yves Bucyana, alisema hatua hiyo imekuja wakati taifa la Rwanda limetangaza kupona kwa wagonjwa wanne wa corona, ambapo raia wa Rwanda ni watatu na raia mmoja ni kutoka Burundi.

Raia huyo wa Burundi, Fabrice Nahimana aligundulika na virusi vya Corona Machi 18, kwenye uwanja wa ndege wa Kigali alipokuwa safarini kwenda Burundi akitokea mjini Dubai.

"Ujumbe mwingi niliotumiwa na jamaa na marafiki kwanza ndio ulinitia uoga sana. nilipokea ujumbe mwingi, baadhi wakilia, wengine wakiona kwamba mwisho wa maisha yangu umefika, lakini Mungu alionyesha nguvu zake," alisema Nahimana na kuongeza:

"Wengi niliwakuta hapa na bado wako hapa, ila nina matumaini kwamba watapona. Kinachofuata sasa mimi nina hamu ya kurudi nyumbani Burundi, familia wananisubiri, marafiki zangu, wazazi wote wananisubiri ili tuweze kumshukuru Mungu kwamba ameniokoa miongoni mwa wengi walioambukizwa virusi vya corona"

Serikali ya Rwanda iliwapatia vyeti wananchi waliopona ugonjwa huo. **BBC**

# Waziri Mkuu Uingereza augua corona, alazwa hospitalini

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, amelazwa hospitalini ili kufanyiwa vipimo vya ugonjwa wa virusi vya corona, siku 10 baada ya kukutwa ameambukizwa katika ofisi yake.

Johnson alikimbizwa katika hospitali moja ya mjini London siku ya Jumapili akionyesha dalili za virusi hivyo ikiwamo kiwango cha juu cha joto mwilini.

Waziri Mkuu wa Uingereza ndiye msimamizi wa serikali, lakini waziri wa mambo ya nje nchini humo anatarajiwa kuongoza mkutano wa virusi vya corona.

Hatua hiyo inajiri baada ya Malkia Elizabeth kulihutubia taifa akisema kwamba Uingereza itafanikiwa katika vita vyake dhidi ya mlipuko wa virusi hivyo.

Katika hotuba yake, Malkia Elizaberth aliwashukuru raia kwa kufuata maelezo ya serikali kusalia nyumbani huku akiwapongeza wale waliojitolea kuwasaidia wengine.

Pia, aliwashukuru wafanyakazi muhimu akisema kuwa kila saa la kazi linazidi kuirejesha Uingereza katika hali yake ya kawaida.

**Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Johnson atafanyiwa vipimo kifuani na mapafu yake iwapo amekuwa akipata tatizo la kupumua.**

Hotuba hiyo inajiri huku idadi ya watu waliofariki kutokana na virusi hivyo nchini Uingereza ikipanda na kufikia 4,934.

Akizungumza katika jumba la kifalme la Windsor, Malkia Elizaberth alisema: "Tumekumbwa na changamoto nyingi katika siku za nyuma, lakini hii ni tofauti. Wakati huu tutaungana na mataifa mengine duniani kwa kutumia hatua za kisayansi zilizopigwa ili kujiponya, tutafanikiwa na kwamba ufanisi huo utakuwa wa kila mtu".

Msemaji wa ofisi ya waziri mkuu alisema: "Waziri mkuu anaendelea kuwa na dalili za virusi vya corona siku chache baada ya kukutwa na virusi hivyo, ameishukuru sana idara ya afya NHS kwa kazi nzuri na kuwaomba raia kuendelea kufuata ushauri wa serikali wa kusalia nyumbani, kuwalinda wafanyakazi wa afya na kuokoa maisha".

Naye Rais wa Marekani, Donald Trump, alimtumia ujumbe wa kumtakia heri njema Johnson katika vita vyake dhidi ya virusi vya corona huku akisema "Wamarekani wote wanamuombea".

"Ni rafiki yangu mkubwa , mtu muungwana na kiongozi mzuri", alisema bwana Trump na kueleza kuwa ana uhakika kwamba waziri huyo mkuu atapona kwa kuwa ni mtu mkakamavu.

Kiongozi wa chama cha Lebour, Keir Starmer, pia alimtakia Johnson heri njema akisema alitumai kwamba atapona haraka.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Johnson atafanyiwa vipimo kifuani na mapafu yake iwapo amekuwa akipata tatizo la kupumua.

Alisema pia huenda akafanyiwa vipimo vya moyo wake pamoja na vipimo vingine kuhusu kiwango cha oksijeni mwilini na kile cha seli nyeupe za damu , ini na figo kabla ya kutolewa hospitalini.

Johnson alikuwa akifanya kazi kutoka nyumbani tangu alipotangazwa kwamba amekutwa na virusi vya corona Mchi 27, mwaka huu.

Alionekana hadharani mara ya mwisho akiwasifu wafanyakazi wa huduma ya afya na wafanyakazi wengine muhimu katika nyumba yake huko Downing street siku ya Alhamisi jioni kabla ya kuongoza mkutano wa virusi vya corona akiwa karantini siku ya Ijumaa. **BBC**



Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta akiwa na baadhi ya mawaziri akizungumzia na vyombo vya habari kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona nchini humo. **PICHA: REUTERS**

# Rais Kenyatta afunga majiji manne kisa corona

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, ametangaza amri ya kuifunga miji ya Nairobi, Kilifi, kwale na Mombasa huku idadi ya maambukizi ya virusi vya corona ikiongezeka kwa visa 16 zaidi.

Taarifa zilizotolewa na idara ya afya nchini humo zinaeleza kuwa idadi ya watu walioambukizwa ugonjwa wa virusi vya corona hadi jana imefikia jumla ya watu 158.

Imesema mbali na idadi hiyo ya maambukizi, idadi ya vifo ni sita, huku Rais Kenyatta akisema kuwa watu 4,277 wamefanyiwa vipimo vya virusi vya corona.

Rais Kenyatta pia amewaagiza Wakenya wote kuvaa barakoa katika maeneo yote ya umma, na kuepuka maeneo yenye mikusanyiko ya watu ili kuepuka maambukizi ya virusi vya corona.

Marufuku ya kusafiri katika Jiji la Nairobi imeanza rasmi jana saa moja usiku kwa saa za Afrika Mashariki, huku marufuku hiyo majimbo ya pwani, Kilifi, Kwale na Mombasa ikianza kesho ikitarajiwa kudumu kwa muda wa siku 21.

Hatua ya kuwekwa marufuku katika majimbo manne imetokana na majimbo hayo kuwa na 96% ya matukio ya maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona nchini humo.

Marufuku hiyo imewekwa dhidi ya safari zote za majini, ardhini na nchi kavu ili kuzuwia maambukizi ya corona yanayoongezeka kwa kasi nchini Kenya na maeneo mengine duniani.

Marufuku hiyo imetangazwa na Rais Kenyatta huku Wakenya wakiendelea kutekeleza amri ya kutotoka nje kuanzia saa moja za jioni hadi saa 11 asubuhi iliyotangazwa wiki iliyopita.

Rais Kenyatta alisema janga na corona likiendelea kuikumba Kenya na mataifa mengine duniani, Wakenya wanapaswa kubadili tabia kwa kunawa mikono na kutosogeleana. Alisema iwapo janga hilo litaendelea kusababisha maafa zaidi Wakenya wajiandae kwa hatua zaidi za kudhibiti maambukizi ya virusi hivyo.

Maambukizi ya ugonjwa wa corona yalianzia katika jimbo la Hubei katika mji wa Wuhan nchini China na kusambaa katika nchi mbalimbali duniani.

Hadi sasa maambukizi ya ugonjwa huo yameshaua watu takribani 60,000 duniani huku idadi kubwa ya watu wakiwa wameambukizwa.

Katika nchi za ulaya, Italia ndiyo inayoongoza kwa maambukizi, ikifuatiwa na Hispania na Ujerumani wakati Marekani ikiongoza kwa maambukizi kwa kasi.

Nchi za Afrika Mashariki, ugonjwa huo umeshika kasi katika nchi za Rwanda, Kenya na uganda huku Tanzania ikitangaza idadi ya watu 20 pekee walioambukizwa na kifo cha mtu mmoja. **BBC**

# Watoto wa kiume watajwa kuathiriwa zaidi na usonji

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

IMEELEZWA kuwa mtoto mmoja kati ya watoto 54 huwa na ugonjwa wa usonji ambao ni tatizo la kinafsi na la kihisia linalowatokea watu tangu utotoni na kuathiri uwezo wao wa kuwasiliana na wengine.

Aidha, watoto wa kiume wanatajwa kuathirika zaidi kuliko watoto wa kike, na kuwa watoto wenye umri wa kuanzia miaka miwili huugua ugonjwa huo.

Hayo yalibainishwa na daktari bingwa wa mishipa ya fahamu na magonjwa ya watoto katika Hospitali ya Rufani ya Bugando, Dk.Yusuph Jamnagwerala, alisema watoto wenye usoji hupata changamoto kubwa hasa katika mawasiliano.

Alisema watoto hao wanapata shida ya mawasiliano, kimatendo na lugha pamoja na shida ya kuhusisha ama kuchangamka na watu wengine.

Hivyo aliitaka jamii kujifunza na kuuelewa vyema ugonjwa huo unaowakumba watoto wadogo kuanzia umri wa miaka miwili ili kuepukana na mitazamo hasi kuhusiana na malezi na makuzi ya watoto wenye matatizo hayo katika jamii.

" Hakuna tiba maalum ya ugonjwa wa usonji zaidi ya kuelewa mapema tabia mbalimbali za watoto wenye ugonjwa huo, na kuwafundisha kisaikolojia namna ya kuyakabili mazingira,"alisema Dk. Jamnagwerala

Naye mtaalamu wa elimu kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Ilemel, mkoani Mwanza, Sarah Ulimboka, alisema halmashauri hiyo inakabiliwa na uhaba wa wataalamu wa kufundisha watoto wenye usoji, hali ambayo inasababisha watoto hao kutokuwa na uangalizi wa kutosha.

"Watoto wengi wanakuwa kwenye shule jumuishi kwa sababu siyo shule zote zenye wataalamu ambao wanafahamu kuhusiana na usonji, kwa sababu hiyo ni tabia ambayo kwa mtu ambaye hajapata mafunzo hayo inakuwa ni ngumu kumtambua mtu mwenye tatizo," alisema na kuongeza:

"Mtoto anaweza kuwa mtundu sana ama mkorofi, unaweza usimtambue, hivyo hatuna wataalamu kwenye shule ambao wamepata mafunzo ya kumfundisha mtoto mwenye usonji," alisema Ulimboka.

Elizabeth Wambura na Samuel Raphael, baadhi ya wazazi wenye watoto wenye usonji, walieleza namna wanavyokutana na changamoto ya kulea watoto hao.

Walisema wanapata changamoto kubwa katika malezi na wakati mgumu kwa jamii kuwaelewa wakati mwingine wanalazimika kuwa karibu na watoto muda wote ili kuwanusuru na majanga.

"Wazazi wenye watoto wenye usoji hukutana na changamoto nyingi ya kulea watoto hao...wapo wanakata tamaa, lakini siku zote furaha ya mama ni kumuona mwanae akiwa na afya njema, ndio inayowapa nguvu wazazi hawa kuendelea kupambania afya za watoto wao," alisema Wambura.



Mfanyabiashara Faraj Abri, akiwahudumia kuku wake katika shamba la Kibwabwa nje kidogo ya mji wa Iringa jana. Abri, aliwataka vijana nchini kuchangamkia fursa ya ufugaji wa kisasa kwani biashara hiyo inalipa. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mwanafunzi afariki kwa kunaswa umeme

**Na Robinson Wangaso,** MARA

MWANAFUNZI wa darasa la saba Shule ya Msingi Mrunyigo, Kijiji cha Kiemba mkoani hapa, Calvin Eranga (14) , amefariki dunia baada ya kunaswa akiwa amepanda juu ya mti uliokuwa umegusana na nyaya za umeme.

Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme (Tanesco), Mkoa wa Mara, Meshak Laurent, akizungumzia tukio hilo alisema, mwanafunzi huyo alifikwa na mauti mwishoni mwa wiki baada ya kupanda juu ya mti ambao ulikuwa jirani na nguzo zenye nyaya za umeme.

Aliwaambia waandishi wa habari kuwa, elimu kwa wananchi ya kuchukua tahadhari na kulinda miundombinu inatolewa kwa umma, lakini shughuli za kibinadamu na uzalishaji zinaendelea kandokando ya njia za umeme licha ya tahadhari kutolewa mara kwa mara.

Alisema ni jukumu la jamii wakiwamo viongozi wa serikali na kijamii kushirikiana kuhifadhi miuondombinu ikiwamo ukataji miti iliyopadwa jirani na njia za umeme kutokana na kutoruhusiwa kuikata isipokuwa Tanesco.

Baba mkubwa wa marehemu, Katekista Leo Ekingo, alisema mwanafunzi huyo alipanda katika mti wa mchongoma ambao ulikuwa unagusana na nyaya za umeme na kusababisha kifo chake.

"Miti ilikuwa inagusana na nyaya za umeme, kijana akiwa juu ya mti wa mchongoma akanaswa na akawa ananing'inia kwa muda kisha umeme ukamwachia akadondoka chini na kufariki dunia...," alisema.

Ofisa wa Baraza la ushauri la watumiaji wa huduma za nishati na maji (Ewura CCC), Mkoa wa Mara, Dennis Ndanu, alisema ofisi za baraza hilo limepata taarifa ya kifo cha mwanafunzi huyo na linafuatilia ili kuhakikisha haki na stahiki za muathirika zinapatikana kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

# Nape amfagilia Magufuli

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, amesema mabadiliko ya kuendesha siasa nchini yametokana na kazi iliyofanywa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Akichangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2020/21, Nnauye, alimsifu Rais John Magufuli kwa kufanya kazi kubwa kwenye utekelezaji wa ilani na kuwaomba Watanzania wampe nafasi tena ya kuongoza miaka mitano ijayo kwa kuwa anatosha.

Alisema amefanya mabadiliko na kuondoa utamaduni uliojengeka ikiwamo wa uendeshaji wa siasa.

"Ukienda siasa walishazoea hivyo hivyo, kuna kelele ndio, lakini ukiangalia namna tunavyofanya tumekuwa 'more serious' (makini zaidi) ukiangalia watani zangu Chadema wamefanya uchaguzi, wamefanya ACT angalia walivyofanya, kuna mabadiliko kwenye uendeshaji wa shughuli zetu,"alisema.

"Naamini mabadiliko haya ni kazi nzuri ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi, Magufuli na serikali yake wamefanya kazi vizuri, wametutendea haki Ilani ya uchaguzi hata mtaani watu wamebadilika wapo sasa 'serious (makini)."

Akizungumza kama Katibu Mwenezi mstaafu ambaye alisimamia utengenezaji wa ilani hiyo, alisema kazi nzuri imefanyika.

"Kazi ya kubadilisha utamaduni wa namna tunavyofanya mambo kwenye nchi yetu, tuliweka slogani ya 'Hapa kazi tu', ilitokana na utamaduni watu waliokuwa wamejijengea, kupata kipato kikubwa hakilingani na kazi inayofanyika, kwenye uchumi vyuma vinakaza, lakini vinakaza kwasababu tulizoea dili, dili zikifungwa kwa vyovyote vile vyuma vinakaza,"alisema.

Hata hivyo, alisema upungufu ya hapa na pale katika kutengeneza mambo hayo na kukanyagana vidole utumike vizuri kusaidia kurekebisha ili Tanzania iendelee kusonga mbele.

Alishauri suala la studio ya Bunge liwekwe kikanuni ili iwe sehemu ya uendeshaji wa shughuli za bunge.

**Upungufu ya hapa na pale katika kutengeneza mambo hayo na kukanyagana vidole utumike vizuri kusaidia kurekebisha ili Tanzania iendelee kusonga mbele.**

# Majaliwa afafanua waziri kuwekwa karantini

**Na Agusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikali ilimuondoa kwa nguvu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati wa Zanzibar, Salama Aboud Talib, katika Hospitali ya Mnazimmoja na kumuweka karantini.

"Ni kweli kulikuwa na Waziri ambaye alitakiwa kujitenga alikataa na hivyo serikali ikachukua hatua ya kumuondoa kwa nguvu, kwasasa yupo eneo la kutengwa, tumeweka haya maeneo kulingana na uwezo wa mtu, kila mtu ataenda kulingana na uwezo,"alisema.

Majaliwa alisema maeneo hayo yanaulinzi na upatikanaji wa vyakula kulingana na uwezo wa mtu.

### HUDUMA ZA MAKTABA BURE

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema kwa sasa serikali inatoa huduma ya upatikanaji wa vitabu vyote kuanzia shule za msingi na sekondari kwenye maktaba bila malipo yeyote kwa njia ya mtandao.

"Tunatambua kwamba wanafunzi wapo nyumbani na wanahitaji kuendelea kupata elimu hata wakiwa nyumbani, tunayohuduma ya maktaba inayotolewa na Taasisi ya Elimu Tanzania ambayo kiutaratibu ili uweze kupata vitabu ilipaswa mtu kulipa, sasa serikali inatoa huduma ya upatikanaji wa vitabu vyote kuanzia shule za msingi na sekondari bila malipo yeyote,"alisema.

Aliwataka wanafunzi kutumia muda wao kusoma vitabu ambavyo serikali imewapa fursa bila gharama yeyote badala ya kuzururura mitaani na kujiweka kwenye hatari ya kupata maambukizi ya corona.

### MBOWE AMALIZA KUJITENGA

Awali akichangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu 2020/21, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Bunge, Freeman Mbowe, alisema amemaliza muda wake wa kujitenga huku akisema suala la corona halijapewa uzito unaostahili.

Alishauri kuundwa kwa kikosi kazi cha Taifa kwa ajili ya kuangalia athari za uchumi za ugonjwa huo.

"Bado suala hili halijapewa uzito unaostahili kama mataifa mengine kwasababu bado kuna uzembe kwa kujua ama kutojua au kudhani liko mbali na halipo nchini, nilitegemea uwepo mpango maalum na kutoa taarifa iwapo kuna athari gani katika uchumi, lakini bajeti ziko pale pale,"alisema.

Alibainisha kuwa sekta ya utalii imeanguka kwa asilimia 99 na kwamba kuna kampuni zimefungwa huku mapato ya nchi yatapungua kwa asilimia 40 kwa miezi sita ijayo.

"Kumekuwa na kauli tofauti, mikusanyiko ambayo haifai na kwamba kuna mikusanyiko ambao wakuu wa mikoa ndio wamekuwa wakiifanya

Wanakusanya watu, wanahutubia watu kwamba ugonjwa uko mbali hii ni hatari," alisema.

Aliongeza: "Ningetamani tumsikilize Rais, Waziri Mkuu na Waziri wa Afya kama nchi ikienda kwa kila kiongozi kutoa taarifa ugonjwa huu utawafikisha mahali pabaya."

Alisema jambo hilo linahitaji kikosi cha Taifa kwa ajili ya kuangalia athari za uchumi na kijamii na pia kuangalia vipaumbe vya Taifa hivi sasa ni vipi.

"Tu suspend baadhi ya mipango ili kuwezesha kukabiliana na tatizo hili," alisema.

### 'ULIPAJI MADENI NJE USIMAMISHWE'

Mbunge Kigoma Kaskazini (CCM), Peter Serukamba, alimuomba Waziri wa Fedha kutafuta fursa kama nchi zinazoendelea kwa kuomba wahisani wanaoikopesha Tanzania kusimamisha ulipaji madeni ili fedha hizo zitumike kwenye athari za uchumi zinazosababishwa na Corona.

"Mimi naangalia corona kwa pande mbili suala la afya na utabibu na upande mwingine ambao ni mbaya zaidi ni suala la uchumi, dhahabu tunayo lakini hatuna sehemu ya kuuza, mazao tutavuna hatuna pakuuza wanunuzi hawawezi kuja ni hatari kwa uchumi wetu," alisema.

Alisema hali ni mbaya Waziri aongee na mabenki kwa kuwa wafanyabiashara nao wameyumba ili wasimamishe ulipaji mikopo.

"Kwamba kwa mtu mwenye baa au hoteli, mtu mwenye biashara ya maua, lakini amekopa benki, mabenki kwa miezi mitatu wasimamishe ulipaji mikopo, hapa tutapata tatizo jingine la Corona ya kiuchumi,"alisema.

### ATAKA WAZIRI ZANZIBAR ACHUKULIWE HATUA

Naye, Mbunge wa Konde (CUF), Khatib Said Haji, alitaka Serikali kumchukulia hatua Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, Salama Aboud Talib, ambaye alikataa kukaa kwenye karantini na kusababisha maambukizi kwa watu wawili ndani ya familia yake.

Pia alisema Waziri huyo alikaa Hospitali ya Mnazimmoja kwa siku tatu na alitolewa kwa nguvu baada ya kuona jambo hilo limekuwa kubwa sana.

"Baada ya malalamiko makubwa ndio alikubali kuwekwa kwenye karantini, alifanya hivyo kwasababu ya kiburi cha madaraka yake, nampongeza Makamu wa pilli wa Rais Zanzibar, kwa kukubali kukaa karantini alipotoka nje ya nchi bila kulazimishwa," alisema.

## Bajaji waomba wamiliki kupunguza hesabu

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

UMOJA wa Madereva wa Bajaji na Bodaboda mkoani Tabora, wamewaomba wamiliki wa vyombo hivyo vya usafiri kupunguza kiasi cha fedha ambacho madereva wamekuwa wakiwasilisha kwa wiki.

Hatua hiyo inatokana na kupungua kwa wasafiri wanaotumia vyombo hivyo, baada ya vyuo na shule kufungwa kutokana na ugonjwa wa Covid -19.

Ombi hilo lilitolewa jana mjini Tabora na Mwenyekiti wa Mkoa wa Umoja huo, Said Maganga, wakati wa mjadala wa kutoa elimu kupitia redio wa kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema hivi sasa fedha waliokuwa wakipata kwa siku imepungua kutokana na uwapo wa ugonjwa wa Covid 19, hivyo kushindwa kufikisha hesabu za wamiliki wa vyombo vya usafiri.

"Tunaomba wamiliki watusaidie kupungua kiwango katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya Covid 19 ili na sisi tubaki na fedha kwa ajili ya matumizi ya familia zetu… watu wengi wamekuwa waoga hawataki kupanda bajaji na wengine wameamua kutembea kwa miguu kwenda kazini," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Maganga alimuomba Mkuu wa Mkoa huo, Aggrey Mwanri, kuwachukulia hatua wamiliki wa vyombo vya usafiri ambao wamekataa kununua vitakatisha mikono kwa sababu wao wanapingana na juhudi za Serikali za kupambana na Covid -19.




Mkuu wa mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack (kushoto), akikabidhi sehemu ya vifaa vya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, vyenye thamani ya Sh. milioni 10.7, kwa Mganga Mkuu wa mkoa huo, Dk. Yudas Ndugulile, vilivyotolewa na wadau wa afya mkoani humo jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

## RC azuia mkutano wa Efatha

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani Mhandisi Evarist Ndikilo, amesitisha mkutano wa Kanisa la Efatha uliokuwa ufanyike kuanzia Aprili 7 hadi 12, katika eneo la Bungu wilayani Kibaha, ikiwa ni tahadhari ya kujikinga virusi vya corona.

Akiwa ameambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa huo jana, alitembelea eneo na kupokea taarifa ya maandalizi ya mkutano huo na walivyojipanga kuchukua tahadhari ya maambukizi ya virusi hivyo.

Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa Efatha, Vivian Mmari, alisema mkutano huo ni wa siku tano na ulilenga kujumuisha washiriki 3,000 ambao ni viongozi wa mikoa wa kanisa hilo wa hapa nchini.

Alisema wamejipanga kujikinga na maambukizi ya Covid 19 ikiwa ni pamoja na kufanya vipimo vya awali na kuweka vitakasa mikono.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Ndikilo, alisema baada ya kukagua mazingira ya kulala waumini, hawawezi kuafiki mkutano huo kuendelea.

"Mazingira tuliyoyakuta wingi wa watu unaokusudiwa, mazingira ya kulala, Kamati ya Usalama Mkoa inatilia shaka kukiukwa kwa maelekezo ya serikali yaliyotolewa ya kuchukua tahadhari na kuepuka mikusanyiko isiyokuwa na lazima," alisema Ndikilo.

Alisema lengo si kuzuia ibada ni kuchukua tahadhari madhubuti ya kujikinga na ugonjwa wa Corona unaoenea kwa kasi.

Alisisitiza kuwa waumini wa madhehebu yote Mkoa wa Pwani waendelee na ibada kwa siku zao za ibada huku wakichukua tahadhari.

# BERBATOV AMTAKA WERNER KWENDA BAYERN



**MANCHESTER,** England

NYOTA wa zamani wa Manchester United na Tottenham, Dimitar Berbatov, amemshauri Timo Werner kusaini Bayern Munich badala ya Liverpool kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Mjerumani huyo amekuwa na kiwango cha kuvutia pale RB Leipzig katika misimu ya hivi karibuni, na alifunga mabao 21 kwenye mechi 25 msimu huu kwa timu hiyo inayoshika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Werner amekuwa akihusishwa na klabu nyingi za Ulaya, ikiwemo Liverpool, lakini Berbatov anaamini atafanya jambo la maana kama akibakia nchini Ujerumani.

"Kumekuwa na ripoti kuhusu Bayern Munich kumuwania Timo Werner, na nikiwa nimecheza Bundesliga, Munich pale kuna majina makubwa kama Real Madrid, Manchester United, Barcelona, Manchester City, Juventus na nyinginezo," amesema akinukuliwa na gazeti la Daily Mail.

"Kila msimu, wapo kwenye ligi ya mabingwa Ulaya na wametawala soka la Ujerumani. Na pia ushindani wa namba hautakuwa mkubwa zaidi kwa upande wake pale.

"Kwa kuwa mkweli, unaonekana ni uhamisho wa busara kwa Werner, anaijua ligi, wanamjua yeye pale, itamfaa zaidi akibakia nchini Ujerumani na itakuwa rahisi kwa upande wake."

# Real Madrid yaongeza nguvu kwa Kane

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inawania kumsajili Harry Kane, kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu, kwa mujibu wa magazeti ya nchini Hispania.

Klabu hiyo inayotumia uwanja wa Santiago Bernabeu inajipanga kuimarisha kikosi chake baada ya kumalizika kwa msimu wa 2019-20 na anaamini mshambuliaji huyo wa Spurs ni mtu sahihi kumsajili kipindi cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa gazeti la nchini Hispania la OK Diario, wanajua kwamba itakuwa kazi ngumu kufikia bei ya kumnunua Kane kutoka kwa klabu yake hiyo ya London Kaskazini.

Lakini wanahitaji mshambuliaji mpya pale mbele baada ya Luka Jovic kutokuwa kwenye kiwango cha kuvutia tangu alipojiunga nao kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Na Zinedine Zidane anataka kukamilisha usajili huo – huku Florentino Perez akimuona Kane kama ndiye mtu anayefaa kumsajili kikosini hapo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 bado yupo kwenye mkataba na Spurs ambao unamalizika mwaka 2024 na mwenyekiti, Daniel Levy, anajulikana kwa kuwa mzuri mno katika majadiliano ya kupatana bei.

Kocha Jose Mourinho pia hataki Kane auzwe kwa sababu anamtegemea na ana mipamgo nae mikubwa fowadi huyo.






# AC Milan wajitosa kumuwania Icardi

**MILAN,** Italia

KLABU ya AC Milan, imeripotiwa kwamba ina matumaini ya kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina, Mauro Icardi kutoka kwa wapinzani wao wa jiji moja, Inter Milan.

Fowadi huyo mwenye umri wa miaka 27, kwa sasa anacheza kwa mkopo Paris Saint-Germain, ambako amekuwa kwenye fomu ya juu na amefunga mabao 20 msimu huu tangu alivyoondoka pale San Siro.

Klabu hiyo ya Ufaransa inakipengele cha kumnunua kwa pauni milioni 62, lakini taarifa za hivi karibuni zinabainisha kwamba, Icardi hana mpango wa kuendelea kucheza pale baada ya msimu huu.

Juventus imekuwa ikihusishwa nae kwa kiasi kikubwa kumsajili mshambuliaji huyo wa Argentina, lakini sasa ameanza mazungumzo na Milan.

Na gazeti la Corriere dello Sport limesema kwamba, Milan inaweza kujaribu kumsajili Icardi kipindi cha majita ya joto kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake.

Usajili huo unaonekana unaweza kutokea, kwani Luciano Spalletti anatajwa kwamba anaweza kuwa kocha mpya wa Rossoneri hao ambaye Icardi alicheza chini yake msimu wa 2017-18.

Hata hivyo, Milan itatakiwa kutumia kiasi kikubwa cha fedha, huku gazeti la Corriere dello Sport pia likiripoti kwamba wanaweza kutumia kiasi cha pauni milioni 75.

Msimu wa 2018-19, Icardi alikataa kusafiri na kikosi cha Inter kwenye mchezo wa kombe la ligi ya Europa dhidi ya Rapid Vienna akipinga kuvuliwa unahodha.

Akiwa Ufaransa, Icardi amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia msimu huu akifunga mabao 20 katika mechi 31.

HABARI MICHEZO

# Kiwango kumbakiza Smalling AS Roma

**ROMA,** Italia

CHRIS Smalling ameonyesha kiwango cha kuvutia akicheza kwa mkopo pale AS Roma msimu huu, na bosi wa klabu hiyo ya Italia, Paulo Fonseca anataka kumpa mkataba wa kudumu.

Akizungumza na gazeti la A Bola, Fonseca amesema yeye 'ni muhimu sana kwa klabu,' na 'angependa kumbakisha.'

Muingereza huyo alijiunga na AS Roma kwa mkopo Agosti mwaka jana na amecheza mechi 28 kwa timu hiyo, akichangia mabao mawili na asisti moja. Wapo nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

"Amenishangaza mimi," amesema Fonseca. "Ni mlinzi aliyeondoka England akiwasili na mbinu zake, amekuja sehemu anayotaka kuleta tofauti.

"Chris alizoea haraka soka la Italia. Ni mchezaji wa aina yake, ana akili sana. Ana vitu ambavyo kwa uhakika navipenda.

"Ana kasi na anauwezo mkubwa dimbani, ni mtu muhimu sana kwenye klabu.

"Kama inawezekana ningependa yeye abakie. Ni mchezaji wa aina yake na ni mtu mwenye hamasa kubwa zaidi dimbani, najiskia furaha kumuona akiwa na sisi na kuendelea kubakia hapa."

Roma imeripotiwa ipo tayari kumnunua Smalling, hata hivyo, hawapo tayari kufikia kiasi cha pauni milioni 25 ambayo ndio thamani yake.






# MAN CITY KUMPIGA FAINI KALI WALKER

**MANCHESTER,** England

KYLE Walker anakabiliwa na faini kali kutoka Manchester City, baada ya kuwa mchezaji wa hivi karibuni wa Ligi Kuu ya England kuvunja sheria ya kukaa ndani.

Beki huyo aliomba radhi Jumapili baada ya kuandaa sherehe nyumbani kwake na kualika marafiki zake aliowalipa pauni 2,200 kweye makazi yake mtaa wa Cheshire.

Jack Grealish alivunja sheria ya serikali ya kuwazuia watu kutoka ndani kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona na alipigwa faini na Aston Villa baada ya kuhudhuria sherehe nyumbani kwa mchezaji mwenzake wa zamani, huku fedha alizolipa zilichangiwa kwenye hospitali ya Birmingham.

City waliifanyia uchunguzi video ya sherehe hiyo iliyopostiwa kwenye mitandao ya kijamii na wakatangaza kumchukulia hatua, baada ya mchezaji huyo kuomba radhi.

Walker mwenye umri wa miaka 29 alisema: "Nataka kuchukua nafasi hii kuomba radhi hadharani kwa kile nilichokifanya kwa kuvunja sheria ya kukaa ndani wiki iliyopita.

"Naelewa nafasi yangu kama mwanasoka wa kulipwa natakiwa kuwa mfano wa kuigwa. Katika hilo nataka kuomba radhi kwa familia yangu, marafiki, mashabiki wa soka na jamii yote kwa ujumla kwa kuwavunja moyo."

# Sagna: Arsenal msifanye kosa kumuuza Aubameyang

**LONDON,** England

BEKI wa zamani wa Arsenal, Bacary Sagna, amesema klabu hiyo itafanya kosa kubwa sana kama itamuuza Pierre-Emerick Aubameyang, kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Mshambuliaji huyo amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa Ulaya na akiripotiwa kutokuwa na furaha na klabu yake hiyo kwa sababu haina nafasi ya kufuzu ligi ya mabingwa Ulaya msimu ujao.

Aubameyang amebakisha miezi 12 kwenye mkataba wake wa sasa pale Emirates na anaweza kuuzwa kama klabu itashindwa kumpa mkataba mpya.

Sagna amesema Arsenal haitaweza kuhimili kumpoteza mshambuliaji huyo na lazima waepuke kumuuza nyota mwingine kama walivyofanya wakati wake akicheza pale.

"Hawezi kwenda sasa kwa sababu wapo kwenye harakati za kuijenga timu imara," alisema akinukuliwa na Goal.

"Hivyo wasitumie pauni milioni 150, watumie pauni 50 na wampe yeye. Ni sawa na ilivyokuwa kipindi cha van Persie na nafikiri wanatakiwa kujifunza kutokana na hali ile.

"Auba anastahili kikubwa. Sisemi hivyo kwa sababu ya jina lake au kwa sababu amefunga mabao mengi. Yeye ni mshambuliaji bora kwenye Ligi."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR AFUNDWA KUMFIKIA MESSI, CR7

## ●●● Zico amchambua mwanzo mwisho na kueleza wanapompiku mastaa hao wa Barca na Juve...

**RIO,** Brazil

NEYMAR anahitaji kufikia taaluma ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi, kwa mujibu wa nguli wa Brazil, Zico.

**Nyota huyo wa Paris Saint-Germain, Neymar, amefunga mabao 69 katika mechi 80 alizocheza katika mashindano yote tangu alipotua Parc des Princes akitokea Barcelona kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia kiasi cha euro milioni 222 Agosti mwaka 2017.**

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ameshinda kila taji la ndani nchini Ufaransa, lakini majeruhi na sasa mlipuko wa janga la virusi vya corona, yamekwamisha jaribio lake la kuiongoza PSG kupata mafanikio kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Neymar amekuwa akihusishwa sana na kurejea Barca na kujiunga tena na Messi pamoja na Luis Suarez, kando yao ambapo kwa pamoja walitengeneza safu hatari ya kisasa ya ushambuliaji dimbani.

Zico hana shaka kuhusu kipaji cha Neymar, lakini anahisi hataweza kufikia daraja la Messi na nyota wa Juventus, Ronaldo - ambao wameshinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] mara 11 kati yao- bila ya yeye kubadili mtazamo wake.

"Ukweli ninampenda Ney, namna ya uchezaji wake ni wa kushangaza. Lakini anapaswa kuwa mtaalamu zaidi kama Ronaldo na Messi, ambao wanaishi kwa soka," Zico aliliambia gazeti la La Gazzetta dello Sport.

"Ney ana maoni mengi sana ambayo yanamtia wasiwasi. Nimezungumza naye hivi karibuni na kumtaka kuwa mtaalamu.

"Ana miaka 28 kwa sasa na kuna timu nzuri PSG. Wanaweza kutwaa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Itategemea ubora wake katika mashindano yote, na si kwa mechi moja tu. Kwa sasa Ney ana uzoefu zaidi na ukomavu."

Neymar alirudi Brazil kipindi hiki cha janga la corona ili kuwa karibu na familia yake. Alikosolewa sana Februari mwaka huu kwa kufanya sherehe ya siku ya kuzaliwa katika klabu ya usiku ya Paris ikiwa ni siku mbili tu kabla ya PSG kuivaa Nantes.

Neymar baadaye aliachwa nje ya kikosi katika mchezo huo kutokana na majeraha ya mbavu, ingawa klabu ilisisitiza kwamba aliyapata katika mchezo wa karibuni dhidi ya Montpellier.

## ZISIKUPITE

### KANE ATAKIWA MADRID

REAL Madrid inataka kumsajili mshambuliaji wa Tottenham na England, Harry Kane, 26. ***(Sport)***

### SANCHO ATAKA UEFA UTD

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, 20, atakataa kujiunga na Manchester United majira ya joto kama itashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Sun)***

### SAGNA: AUBAMEYANG ASIUZWE

BEKI wa zamani wa Arsenal, Bacary Sagna, amesema klabu hiyo itafanya makosa makubwa kama itamuuza mshambuliaji Pierre-Emerick Aubameyang, majira haya ya joto. ***(Daily Mail)***

### AC MILAN YAMGEUKIA ICARDI

AC Milan imeripotiwa kuwa na matumaini ya kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Mauro Icardi, kutoka kwa mahasimu wao, Inter Milan. ***(Daily Mail)***

### MORELOS AVUTIA KIBAO EPL

LEICESTER, Newcastle, Crystal Palace na Aston Villa, zinavutiwa kumsajili mshambuliaji wa Rangers na Colombia, Alfredo Morelos, 23. (Talksport)

### WEST HAM YAMTAKA SANCHEZ

WEST Ham imekuwa katika mawasiliano na wakala wa Alexis Sanchez, wakati ikizingatia uwezekano wa kwenda kumsajili mshambuliaji huyo wa Chile. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, kwa sasa anaichezea Inter Milan kwa mkopo akitokea Manchester United. ***(Sport Witness)***

### SILVA KUAGWA KIANGAZI CITY

KIUNGO wa Manchester City, Mhispania David Silva, 34, anaweza kupewa mechi ya kwaheri katika dimba la Etihad Stadium majira ya kiangazi kama janga la virusi vya corona vitamzuia yeye kuaga mashabiki wa klabu hiyo baada ya kuitumikia kwa miaka 10 10, ambayo imeshuhudiwa akishinda taji la Ligi Kuu England kwa mara nne. ***(Mail)***

### BERBATOV AMTOA WERNER

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United na Tottenham, Dimitar Berbatov anaamini straika wa RB Leipzig na Ujerumani, Timo Werner, 24, ingekuwa bora majira haya ya joto kujiunga na Bayern Munich kuliko Liverpool. ***(Mirror)***

### SPURS KWA SANTAMARIA

LEICESTER, Tottenham na Everton zote zinavutiwa na kiungo mkabaji Baptiste Santamaria, 25, ambaye anaichezea klabu ya Ufaransa ya Ligue 1, Angers. ***(Express)***

### AMSIKILIZIA SOLSKJAER

BEKI wa Manchester United, Mholanzi Timothy Fosu-Mensah, 22, anakabiliwa na hatma isiyo na uhakika wakati huu kocha Ole Gunnar Solskjaer akitafakari kumuongezea mkataba wa mwaka mmoja. ***(Mirror)***

### EPL KUTOIFUATA UBELGIJI

MSHAMBULIAJI wa Anderlecht, Kemar Roofe anatumai Ligi Kuu England, haitafuata nyayo za Ubelgiji na kujaribu kuhitimisha msimu. ***(The Sun)***

## Ambokile: Mazoezi Mazembe kwa WhatsApp

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa TP Mazembe ya DR Congo, Mtanzania Eliud Ambokile, amesema kutokana na janga la maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19), wanalazimika kupewa maelekezo kupitia mtandao wa simu kuepuka mkusanyiko.

Ambokile ameliambia Nipashe jana kwa njia ya simu kwamba, wapo katika wakati mgumu kufuatia kusitishwa mazoezi ya pamoja kutokana na hofu ya maambukizi ya vizuri vya corana hali inayowalazimu benchi la ufundi kufanya majukumu yao kupitia simu.

Alisema hadi sasa hawajajua hatma ya ligi nchini humo, hivyo benchi la ufundi kila siku hulazimika kutoa maelekezo ya mazoezi kupitia simu katika 'Group lao la WhatsApp' kwa kila mchezaji kufanyia nyumbani kwake.

"Tunapewa elimu ya kujikinga, ila hali si nzuri, tunaomba Mungu hili janga liondoke, hadi sasa hatujajua hatma ya ligi huku Congo, makocha wanaendelea kutoa maelekezo ya ufundi pamoja na mbinu za mazoezi kupitia group la WhatsApp," alisema Ambokile.

Alisema hakuna kwenda kufanya mazoezi, hivyo kila mchezaji anatulia nyumbani kwake kwa ajili ya kusubiri majukumu ambayo hutolewa na benchi la ufundi kupitia Group la WhatsApp.

## Black Sailor yajivunia usajili

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HUKU jumla ya michezo 113 ya Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inayoshirikisha timu 13 ikiwa imechezwa na mabao 281 yakifungwa, uongozi wa timu ya Black Sailor, umejivunia umakini wao katika usajili wa safu ya ushambuliaji na ulinzi.

Katika mabao hayo, Black Sailor inayoshika nafasi ya pili kwenye msimamo ikiwa na pointi 34 sawa na Taifa, imepachika mabao 24 na kuruhusu nyavu zake kutikishwa mara 10 katika mechi 17 ilizocheza hadi ligi hiyo inasimama kutokana na kuepuka kasi ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19).

Akizungumza na gazeti hili, Katibu wa Black Sailor, Issa Khatib Masiku, alisema msimu huu timu yao imecheza vizuri ikilinganishwa na msimu uliopita hali inayowapa matumaini ya kuendelea kufanya vizuri katika ligi hiyo ambayo ndiyo ligi ngumu kutokana na kila timu kuwania nafasi ya kupanda Ligi Kuu.

Alisema msimu huu viongozi wa timu hiyo walitulia katika kufanya usajili ambao umeonyesha umeisaidia timu hiyo kukaa katika nafasi nzuri na kujipa matumaini ya kupanda Ligi kuu msimu ujao. Alisema nafasi walizosajili kwa umakini zaidi ni ya ulinzi na ushambuliaji ambao usajili wao uliangalia zaidi vijana

"Msimu huu tuliangalia upungufu tuliokuwa nao na tukaona tatizo lipo kwa walinzi na washambuliaji, hivyo hata katika usajili nguvu zetu tulielekeza katika nafasi hizo hali inayosababisha kupata matokeo mazuri uwanjani," alisema.

# MATUMLA, USTADHI WAELEZA MABONDIA WANAPOTELEZA

**Na Somoe Ng'itu**

BONDIA mkongwe nchini, Rashid Matumla " Snake Boy", amesema mchezo huo unapoteza umaarufu kutokana na mabondia chipukizi kukosa msingi mzuri wa maandalizi kuanzia ngazi za chini.

**Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Matumla alisema kutokana na kukosekana mfumo sahihi, hali hiyo huwafanya mabondia chipukizi "kukurupuka" kujiunga na ngumi za kulipwa hali ya kuwa hawajapata uzoefu hivyo kuishia kufanya vibaya katika mashindano ya kimataifa wanayoshiriki ndani na nje ya Tanzania.**

"Mimi ninashauri ili kuwabana mabondia kujiunga na ngumi za kulipwa wakiwa hawana uzoefu wa kutosha, ni lazima zitolewe leseni maalumu, hii itasaidia kuwajenga na kutangaza vizuri jina la Tanzania," alisema Matumla.

Aliongeza kuwa siri ya familia yao kufanya vizuri katika mchezo huo ni kujituma kwenye mazoezi ambayo yalisimamiwa kwa kiwango kikubwa na baba yao mzazi ambaye sasa ni marehemu.

Bondia huyo wa zamani wa dunia, alisema pia pambano lake la kwanza dhidi ya Francis Cheka liliandaliwa baada ya bondia huyo kutoka Morogoro kumfuata nyumbani kwao Keko kumuomba wacheze.

"Cheka alifanikiwa kunipiga katika pambana la Morogoro baada ya kuanza kuumwa mgongo, ndio walipoanza kutoka madogo, Cheka alinipiga, Maugo (Mada), ilikuwa njia yao kupata majina," alisema Matumla.

Aliongeza sababu kuu iliyomfanya kuondoka kwa aliyekuwa promota wa ngumu, Jamal Malinzi na kujiunga na Alex Kajumulo, ni kukaa muda mrefu bila ya kutetea mikanda aliyokuwa anaishikilia.

Naye promota wa ngumi maarufu nchini, Yassin Abdallah "Ustadhi", alisema ili kupata mabondia wenye uwezo kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, ni mabondia husika kukubali kuanzia kwenye ngumi za ridhaa kwanza.

Ustadhi alisema mabondia wanapokimbilia kucheza ngumi za kulipwa hali ya kuwa hawajapata uzoefu, wanashindwa kung'ara na wachache ndio hufanya vizuri.

Alishauri serikali kuweka sheria za kuwabana mabondia kufuata misingi kabla ya kujiunga na ngumi za kulipwa kwa sababu mapromota hawana muda wa kuwaendeleza zaidi ya kufikiria maslahi yao binafsi.




Wachezaji wa timu ya Fedha FC, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Hospitali ya Kivule jijini Dar es Salaam, juzi, licha ya serikali kupiga marufuku shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwa ni pamoja na michezo kufanyika kwa kipindi cha mwezi mmoja, kuanzia Machi 17, mwaka huu, ili kuepuka maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19). **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga kujadili Ligi Kuu, FA Cup

**Na Saada Akida**

LICHA ya kutojulikana kwa hatma ya Ligi Kuu Bara kuendelea au kufutwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano wa Yanga, Hamad Islam, amesema wako katika mipango ya kukutana na wajumbe wenzake ili kujadili mwenendo wa timu yao kuelekea michezo iliyobaki na Kombe la Shirikisho la Soka nchini, maarufu FA Cup.

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Islam alisema wanampango wa kukutana na wajumbe wote wa kamati hiyo kwa ajili ya kujadili mwenendo wa timu yao ikiwamo malengo yaliyopo katika michuano ya FA na kuhakikisha timu yao inafanya vizuri kumaliza nafasi ya pili.

Alisema wajumbe wa kamati husika watahakikisha naweka mikakati ya michezo iliyobaki huku wakiipa kipaumbele michuano ya FA ambayo bingwa huiwakilisha nchi katika Kombe la Shirikisho Afrika.

"Kwa sasa kuna janga hili la virusi vya corona, tuombe Mungu limalizike maana kuna mambo mengi ya kimaendeleo yamesimama, pia tuna mpango wa kukutana na wajumbe kujadiliana mambo mengi," alisema Islam.


Alisema kwa sasa wapo makini kuweka mambo sawa kuhakikisha kikosi chao kinafanya vizuri katika michezo hiyo kwa kumaliza ligi katika nafasi ya pili na kutwaa taji la FA ambalo litawapeleka katika michuano ya kimataifa.

Aidha, kuhusu usajili, alisema hawataingilia majukumu ya benchi hilo la ufundi, linaloongozwa na kocha Mbelgiji Luc Eymael, kwa aina ya wachezaji ambao amewapendekeza katika ripoti aliyoiacha.

# Michezo

Jumanne Aprili 7, 2020

Nipashe

Neymar afundwa kumfikia Messi, CR7 UKURASA 30

KIKAZI ZAIDI...




Beki wa Kati wa Yanga, Kelvin Yondani, akiwa na kiungo wa timu hiyo, Papy Tshishimbi, katika moja ya mechi za Ligi Kuu. Yondani ametajwa na beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussen 'Tshabalala', kama mmoja wachezaji wanaomvutia. **PICHA: MAKTABA**

# Yondani avutwa Simba

## ●●● Tshabalala amjumuisha kikosini, pia aelezea bao lake bora kabisa huku akiliacha lile la...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI beki wa kati wa Yanga, Kelvin Yondani, akiwa miongoni mwa wachezaji wa timu hiyo waliokosa namba ya kudumu katika kikosi cha kwanza cha Kocha Mbelgiji Luc Eymael, beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', ametuma ujumbe kwa viongozi na benchi la ufundi la mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara kuwa anafaa kurejeshwa Msimbazi.

**Yondani kwa sasa amekuwa hana namba ya kudumu kwenye kikosi cha Yanga chini ya Eymael na hata mashabiki wa timu hiyo wameonekana hawana wasiwasi tena pindi anapokosekana uwanjani kutokana na kiwango cha kuvutia kinachonyeshwa na Mghana Lamine Moro.**

Akizungumza katika kipindi cha kuchati na mashabiki, kwenye channel inayorushwa na klabu ya Simba, Tshabalala alitaja kikosi chake bora huku kikiundwa na wachezaji karibuni wote wa timu yake ya Simba kasoro Yondani wa Yanga na Aboubakara Salum 'Sure Boy' wa Azam FC.

Aliowataja kutoka Simba ni Aishi Manula, Shomari Kapombe, yeye mwenyewe, Yondani na Erasto Nyoni, Jonas Mkude, Clautos Chama, Meddie Kagere, John Bocco na Ibrahim Ajibu.

Tshabalala alisema kuwa kati ya mawinga hatari ambao amewahi kukutana nao ni Simon Msuva, mchezaji wa zamani wa Moro United na Yanga, ambaye kwa sasa anacheza soka la kulipwa nchini Morocco katika klabu ya Difaa Hassani El Jadidi.

"Hata wachezaji wenzangu niliokuwa nacheza nao kina Hassan Isihaka, siku tunakwenda kucheza nao, wananiambia kalale mapema, ujiandae kwa sababu kesho una shughuli pevu na Msuva na kweli 'kinachimbika', mmoja ni lazima siku hiyo asalimu amri, iwe mimi au yeye," alisema.

Alimtaja mchezaji aliyemvutia zaidi hadi kufuata nyayo zake na kuiga staili zake za uchezaji ni Issa Rashid 'Baba Ubaya', ambaye aliwahi kuichezea Simba mwaka 2013, akitokea Mtibwa Sugar, lakini alicheza kwa misimu miwili kabla ya kurejea tena Mtibwa hadi sasa.

"Nilikuwa namfuatilia sana, kusema kweli niliiga vitu vingi kutoka kwake, wakati huo mimi niko kwenye akademi ya Azam FC, baadaye nikaenda Kagera Sugar, lakini kuna wakati fulani nikabahatika kucheza naye Simba," alisema mchezaji huyo ambaye pia anaichezea timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Kuhusu wakati wake bora kabisa kwenye soka, alisema kuwa ni ule ambao timu yake ya Simba ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, ikidhaniwa kuwa goli lake bora angeweza kulitaja lile la kusawazisha dhidi ya AS Vita ya DR Congo, Simba ikishinda mabao 2-1, Tshabalala alisema bao lake bora ambalo hatolisahau ni lile alilofunga dhidi ya Kagera Sugar, Septemba 26, mwaka jana, Simba ikishinda kwa mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

"Ni kwa sababu nilitumia akili sana kufunga; niliuchukua mpira nikawaacha mabeki, nikaingia ndani, nikampa Kagere, akanirudishia kwenye njia, nikaenda kufunga," alisimulia mithili ya mtangazaji.

Alipoulizwa kama siku moja anaweza kuwa kocha wa mpira wa miguu, alikataa na kusema kama akifanya kazi hiyo, ataishusha daraja timu anayoifundisha.

# Yikpe nje ripoti Eymael Yanga

**Na Saada Akida**

HUKU Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael akiwa tayari amekabidhi ripoti yake ya wachezaji anaotaka wasajiliwe na wale wa kutemwa kuelekea msimu ujao, jina la mshambuliaji Muivory Coast Gnamien Yikpe, ni miongoni mwa wachezaji ambao hawatakuwapo katika kikosi chake, imefahamika.

Taarifa za uhakika zilizolifikia Nipashe jijini jana kutoka kwa kiongozi mmoja wa ngazi za juu ambaye hakutaka kutajwa jina lake gazetini, zilieleza wanalazimika kumjadili mshambuliaji huyo kuwamo katika orodha ya kutemwa kutokana na kushindwa kufanya walichokitarajia.

Alisema nafasi ya kubaki ni ngumu sana katika kikosi cha timu yao kutokana na nyota huyo kushindwa kufikia malengo yao licha ya kupewa nafasi ya kucheza katika michezo mbalimbali ya Ligi Kuu.

"Yikpe hana nafasi kwa msimu ujao, kwani ukiangalia ripoti iliyoachwa na Luc ni ya kuhitaji washambuliaji wawili, hii inaonyesha kwamba mchezaji huyo hana nafasi ya kuendelea kutumikia kikosi hiki," alisema kiongozi huyo.

Wakati huo huo Kocha Msaidizi wa Yanga, Boniface Mkwassa, alisema hatma ya nyota huyo litajadiliwa na jopo zima la benchi la ufundi likiongozwa na Luc pamoja na kamati ya usajili na ufundi.

"Yikpe ameshindwa kwenda na mazingira hadi kushindwa kufikia malengo yaliyotarajiwa, kwani alivyokuja mwanzoni alifanya vizuri, lakini amebadilika ghafla, amekuwa akifanya vizuri mazoezi, lakini katika mechi ni tofauti na kile ambacho anaambiwa," alisema Mkwasa.

Alisema mpira ni mchezo wa kupanda na kushuka, benchi lilijitahidi kumpa nafasi katika baadhi ya michezo ya ligi, lakini akawa anafanya mambo tofauti na kile kinachotarajiwa kabla ya kusajiliwa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >